

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 16 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae.

Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. ISSA J. MTEMVU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

MHE. JERRY W. SILAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021,

NDG. PAMELA PALLANGYO:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaanza maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo Mbunge wa Handeni Mjini.

Na. 134

Ujenzi wa Miundombinu Mnada wa Nderema

MHE. REUBEN N. KWAGILWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu ya kisasa katika mnada wa Nderema?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Jimbo la Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi 287,194,890 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi na uboreshaji wa miundombinu katika mnada wa mifugo wa Nderema uliyopo Halmashauri ya Mji wa Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzabuni ameshapatikana na ameshakabidhiwa mradi mwezi Januari, 2022 na sasa ujenzi umeshaanza. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2022 kwa mujibu wa mkataba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Reuben.

MHE. REUBEN N. KWAGILWA: Mheshimwa Naibu Spika ahsante sana, naomba niulize swali moja la nyongeza kutokana na majibu ya swali langu la msingi. Mkataba aliopewa mkandarasi ambaye yupo *site* sasa kuujenga mnada wa Nderema, pamoja na kwamba unajenga miundombinu ya muhimu, bado kuna miundombinu ya msingi ambayo haijaa inishwa kwenye mkataba na haimo kwenye mkataba, lakini miundombinu hii ni muhimu sana kwa mnada ule. Mathalani vibanda vya kupumzikia, mahali pa kupandishia ng'ombe kwenye magari pamoja na machinjio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haifikirii pana umuhimu sasa wa kwenda kufanya marekebisho kwenye mkataba ule ili miundombinu hii iweze kuingizwa kwenye mkataba huu wa mkandarasi aliyepo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeleka milioni 287 na mkandarasi atajenga miundombinu ikiwemo uzio, ofisi, mazizi manne, maeneo ya kushushia mifugo, lakini pia vyoo na miundombinu mengine. Hii ni hatua ya kwanza, hatua ya pili tutakwenda ku-*consider* miundombinu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema ili tutenge bajeti kuhakikisha mnada ule unakuwa na miundombinu yote muhimu. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Justin Lazaro.

Na. 135

Kugawa Wilaya ya Kilolo kuwa Halmashauri Mbili

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuigawa Wilaya ya Kilolo kuwa na Halmashauri mbili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuanzisha eneo la utawala la wilaya unafanyika kwa Mujibu wa Sheria, Kanuni na kwa kuzingatia mwongozo wa kuanzishwa maeneo mapya ya utawala wa mwaka 2014. Aidha, maombi ya kuanzisha wilaya mpya yanatakiwa kujadiliwa na kupitishwa kwenye Vikao vya Kisheria ngazi ya Vijiji, Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Maombi hayo yanawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya uchambuzi na uhakiki na baadaye kuishauri mamlaka ipasavyo juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Iringa haujawasilisha mapendekezo yanayohusu kugawa Wilaya ya Kilolo ili kuwe na Halmashauri mbili. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kilolo kufuata utaratibu uliolekezwa hapo juu, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Nyamoga.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni zaidi ya miaka 10 sasa tangu Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula imeanzishwa, ningependa kujua ni tathmini gani au ni utaratibu gani unatumika ili kupandisha hadhi kutoka kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo kwenda kuwa Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ningependa kujua katika ugawaji wa halmashauri kipo kigezo cha idadi ya watu na katika maeneo yenye hifadhi kubwa ya misitu

na maeneo yaliyohifadhiwa na mbuga kama Kilolo kigezo hiki kinakuwa tishio kusababisha kuchelewa kugawa kwa halmashauri pamoja na ukubwa wake. Je Serikali iko tayari kuangalia kigezo hiki na kuangalia zaidi ukubwa ili wananchi waweze kufikiwa na huduma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, unazishaji wa mamlaka mpya zikiwepo halmashauri za miji zinategemea kukidhi vigezo vilivyowekwa ili halmashauri iweze kupewa mamlaka halisi ya kuwa halmashauri kutoka malmaka ya mji mdogo. Ni kweli kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula ina zaidi ya miaka 10 lakini taratibu za kuomba kuwa Halmashauri ya Mji ni zilezile ambazo zinatumiwa kuomba Halmashauri ya Wilaya. Kwa maana vikao vya kisheria katika vijiji na mitaa, kata ngazi ya wilaya pamoja na *DCC* na *RCC*. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na kuomba Wilaya igawiwe kuwa wilaya mbili lakini pia wafuate utaratibu huo kwa Halmashauri ya Mji wa Ilula ili tathmini ifanyike kuona kama kama inakidhi vigezo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na ukubwa wa kijografia wa Wilaya ambayo ina misitu mingi lakini wananchi wachache. Kigezo cha wananchi ni kigezo muhimu sana kwa sababu tunapeleka mamlaka mpya kuhudumia wananchi kwa hiyo idadi ya wananchi ndio sababu ya msingi zaidi ya kutenga halmashauri mpya badala ya eneo la misitu, lakini pia kwa maana ya ukubwa ambao hakuna idadi ya watu. Kwa hiyo, suala hilo ni muhimu na tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunalizingatia katika kugawa mamlaka mpya. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Tatizo la kugawa maeneo ya utawala lililokuwa limetolewa na Mheshimiwa aliyemaliza, linafanana sana na tatizo lililopo katika Jimbo langu la Kigoma Mjini na hasa kugawa maeneo ya utawala ya kata. Maombi tayari yamekwishapelekwa kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo kwenye Wizara husika. Je, ni lini Serikali itafikiria kufanya kazi hii ya kugawa kata. Zipo kata ambazo zina wakazi wengi, zina mitaa mingi, Kata kama za Mwanga Kaskazini, Mwanga Kusini, Buzebazeba na Kibirizi huko Kigoma. Je, ni lini Serikali itachukua hatua hii ili kuwarahasishia watu huduma za kiutawala?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe N'genda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri zimeendelea kuwasilisha maombi ya kugawa maeneo mapya ya utawala kwa maana ya kata na nikiri kwamba Serikali tumepokea zikiwepo Kata za Kigoma Mjini, tathmini zinaendelea na baada ya tathmini hizo na kuangalia mazingira hayo, tutashauri mamlaka husika kwa maana ya mamlaka inayoweza kugawa maeneo hayo ili tuweze kufikia hatua ambayo inahitajika. Kwa hivyo nimhakikishie Mbunge kwamba, suala hilo lipo linafanyiwa kazi. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Unaitwa Mheshimiwa?

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Kasalali Mageni.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Kwa kuwa taratibu za kuigawa Halmashauri

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ya Wilaya ya Kwimba kulipatikana Halmashauri ya Sumve ambayo ndio ina Jimbo la Sumve zimeshakamilika katika ngazi zote mpaka ngazi ya mkoa na tunasubiri tamko la ngazi ya juu kupatikana kwa Halmashauri ya Wilaya Sumve. Je, nini tamko la Wizara kuhusu upatikanaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumve ambayo ni tamanio kubwa la watu wa Sumve na itasaidia sana kusogeza huduma kwa wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kugawa maeneo mapya ya utawala tayari zimepokelewa kwa halmashauri zote ambazo zimewasilisha kupitia utaratibu wa kisheria na kanuni na tathmini inaendelea. Mara baada ya kukamilisha tathmini hizo mamlaka husika itafanya maamuzi ya kugawa ama kutoa muda kwa ajili ya kuboresha maeneo ambayo yatakuwa na upungufu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo lipo na linafanyiwa kazi. Niwaombe kuwa na subra ili muda ukifika basi mtapata majibu ya maamuzi ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Dkt. Charles Stephen Kimei.

Na. 136

Tathmini ya Urejeshwaji wa Mikopo Inayotolewa na Halmashauri

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kutoa tathmini ya urejeshwaji wa mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa Vikundi vya

Akinamama, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu katika kipindi cha angalau miaka mitatu iliyopita?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019, ilitoa mikopo kiasi cha shilingi bilioni 42.06 ambacho kiasi cha shilingi bilioni 12.88 kilirejeshwa sawa na aslimia 3.6; Mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi bilioni 40.73 kilitolewa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.65 kilirejeshwa sawa na asilimia 35.96; na katika mwaka wa fedha 2020/2021 kiasi cha shilingi bilioni 53.81 kilitolewa ambapo shilingi bilioni 29.85 kilirejeshwa sawa na asilimia 55.47.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshasanifu mfumo wa kieletroniki utakaowezesha usimamizi madhubuti wa mikopo katika usajili wa vikundi, utengaji wa fedha, utoaji wa mikopo, usimamizi wa marejesho na shughuli za vikundi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mwongozo wa usimamizi wa mikopo hii umeshaandaliwa na upo kwenye hatua za mwisho za uidhinishaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Wizara, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza; je, Wizara haioni umuhimu wa kuwawezesha halmashauri kutenga maeneo mahususi kwa wajasiriamali na kuyawekea miundombinu stahiki ili wale wanaopokea mikopo waweze kuanzia miradi yao na shughuli zao kwenye maeneo haya

ambayo yatakuwa kama *incubation center* na pia waweze kupewa ushauri nasaha?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kwa vile tunafahamu kwamba mikopo inayotolewa na *NEDF* chini ya *SIDO* inalipika, inarejeshwa kwa kiwango kikubwa cha zaidi ya asilimia 90. Je, Wizara haioni umuhimu wa kushirikisha *SIDO* kwenye kutoa mikopo ya halmashauri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri husika kubwa lao.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba halmashauri zetu lazima zitenge maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji na maeneo haya pia wanufaika vikundi ambavyo vinakopa asilimia zile 10 wawe ni moja ya wanufaika katika maeneo haya ambayo yanatengwa mahususi kwa ajili ya uwekezaji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hili tumeboresha zaidi, tumeshakaa na Wizara ya Kilimo kuangalia hata makundi ya vijana wasomi ambao wanapata asilimia 10 kwenye Halmashauri zetu, Majiji na Manispaa, kuangalia namna bora ya kuweza kuwasaidia maeneo mahususi kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo hili tunalifanyia kazi na nitumie nafasi hii kuzielekeza Halmashauri zote nchini, kuhakikisha maagizo ya Serikali ya kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji yanashughulikiwa. Tunashirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kuweza kuliratibu hili vyema kwa sababu yapo masuala ya fidia. Halmashauri nyingine zimekuwa na nia ya kutenga maeneo, lakini wanakosa fedha kwa ajili ya fidia. Kwa hiyo, yote haya tunayaangalia ndani ya Serikali ili kuhakikisha tunaratibu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu mikopo ya *SIDO* na mikopo kupokea, hili ni eneo lingine ambalo Wizara Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara tunaangalia namna ya ku-*link* pamoja ili zile asilimia 10 ambazo tunazitoa kwenye halmashauri na fedha kupitia Mifuko mengine ndani ya Serikali, tunakaa pamoja na kuangalia namna bora ya kuipeleka kwenye makundi ili iweze kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili kwenye suala la asilimia 10 mikopo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunafanya tathmini ya nchi nzima kuangalia namna bora tutakayoweza kutumia fedha hizi kwa sababu tumetathmini ni takriban zaidi bilioni 60 kila mwaka zinapatikana kupitia halmashauri kupitia vikundi.

Kwa hiyo, tungependa kuona mabilioni haya yanapokwenda kwenye vikundi yanaleta tija, yanasaidia vikundi, lakini vikundi hivi vinasaidia nchi katika kujenga uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tathmini hii kufanyika, tutaleta hapa Bungeni uchambuzi huo ili Waheshimiwa Wabunge waweze kushauri ili tuweze kwenda vizuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa kanuni ya 10(3) ya kifungu 37A cha Sura ya 290 ya Fedha za Serikali za Mitaa inayohusu asilimia 10; imeitaka Mamlaka ya Serikali za Mitaa kukabiliana na mkopaji namna bora ya kurudisha fedha zile za mkopo. Je, Serikali haioni kwamba Kanuni hii inatoa *loophole* kwa Watendaji kuingiza mambo kinyume cha utaratibu na hawaoni haja kuweka muda wa marejesho kulingana na kiwango cha fedha ambacho kikundi kile kitakuwa kimekopa? Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kanuni ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Kanuni ile inayoelekeza mikopo ya asilimia 10 imeweka nafasi ya Watendaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kukubaliana na vikundi vya ujasiriamali kuhusu utaratibu na muda wa marejesho ya mikopo hiyo. Dhamira yake ilikuwa, kwa kuwa mazingira haya ya wakopaji yanatofautiana sehemu moja na nyingine, lakini pia uwezo wa vikundi kurejesha unatofautiana kutoka kikundi kimoja na kikundi kingine, kwa hiyo, tunapokea ushauri wake. Tutafanya tathmini kuona uwezekano wa kuweka *standard* ya muda wa marejesho kwa kiasi fulani na pia tutaboresha njia hiyo kuhakikisha kwamba zile fedha hazipotei. Ahsante. (*Makoff*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Mtemvu ajjandae.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hizo pesa za 10% katika Halmashauri zote nchini Tanzania kwa miaka mitatu mfululizo CAG ametoa ripoti ya upotevu wa fedha hizo; haoni sasa ni wakati wa Serikali kusimamia fedha hizo zinazokopeshwa kwa vikundi zinarudi kwenye Halmashauri na zinakopesha tena vikundi vingine vingine?Ahsante kwa kunisikiliza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, bondia mwenzangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Ndugange kwa namna anavyojibu maswali vizuri na kwa ufasaha. Niendeleo kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kunipa Naibu Mawaziri ambao tunashirikiana vizuri katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunafanya tathmini nzima ya 10% ambazo zinaenda kwa vijana, akina mama na ndugu zetu, watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, *concern* ambayo Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ameisema, zikiwemo hoja za CAG, ni sehemu ya uchambuzi huu. Kama nilivyosema, baada ya kufanya uchambuzi, tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge ili mwelekeo wa matumizi ya fedha za 10% uweze kuwa na tija na matarajio ambayo wananchi wetu pamoja na Bunge hili tutayapata. Nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Mtemvu.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, majibu yanatuonesha kwamba yapo malalamiko mengi sana ya fedha hizi takribani shilingi bilioni 60 ambazo zinarudi kila mwaka zinapatikana kutokea kwenye fungu hili la 10% na mifano imeoneshwa; Dar es Salaam kwenye Wilaya mojawapo tayari kuna ubadhirifu mkubwa sana wa fedha hizi:-

Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kupeleka ukaguzi maalum kwa nchi nzima ili tupate tathmini ya kweli? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Ia Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya maeneo nchini kote kuhusiana na matumizi ya fedha za 10% na Serikali kama ambavyo Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Bashungwa ametoa maelezo mwanzoni, ni kwamba tunafanya tathmini ya kuona wapi kuna mafanikio, maeneo gani yana changamoto, na changamoto ni zipi; ili sasa baada ya tathmini hiyo, tuwe na *direction* ambayo itatuwezesha kuwa na fedha ambazo zinaleta tija kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kutakuwa na sababu ya kutazama uwezekano wa kufanya ukaguzi maalum tutalifanya kwa sababu kazi ya Serikali ni kudhibiti fedha hizo ili ziweze kuleta tija kwa watarajiwa. Kwa hiyo, tumelichukua wazo hilo na tutaendelea kulifanyia kazi. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud.

Na. 137

Usajili wa *NEMC* katika Mfuko wa *Green Climate Fund (GCF)*

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha usajili wa Taasisi ya *NEMC* katika Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa *Green Climate Fund (GCF)* ili kuipatia nchi fursa za fedha za mabadiliko ya tabianchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira),

naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Donge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni Ofisi kiungo ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi Kitaifa ililiteua Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ili liweze kuanza mchakato wa kupata Ithibati na kuwa mratibu wa fedha za Mfuko wa *GCF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Mei, 2021, *NEMC* iliwasilisha maombi rasmi kulingana na taratibu na baada ya *GCF* kujiridhisha mwezi Julai, 2021 walitoa *invoice* kwa ajili ya kulipa ada ya kufanyiwa Ithibati. Ada hiyo imelipwa mwezi Agosti, 2021 na hivi sasa *GCF* kwa barua ya tarehe 10 Januari, 2022 wameiarifu *NEMC* kwamba maombi yao yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwa sasa suala hili liko *GCF*, naomba tuwe na subira wakati *GCF* wanaendelea na taratibu zao za mapitio. Aidha, nitoe wito kwa taasisi zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuata taratibu ili ziweze kupata ithibati kwenye Mfuko huo wa *Green Climate Fund*. Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na yenye matumaini mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mchakato wa wenzetu hawa *NEMC* kujiunga na Mfuko wa Fedha wa *Green Climate Fund* umechukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa; na kwa kuwa sehemu ya mchakato huo ilishafanyika wakati *NEMC* wanajisajili katika Mfuko wa *Adaptation Fund*.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, *NEMC* wamejipanga vipi kuweza kuainisha vipaumbele vya miradi kwa kuzingatia maeneo ya kijiografia, Zanzibar na Tanzania Bara ili wakishapata usajili wasije tena kuchelewa kuwasilisha andiko la mradi kwenye sera hizi ambazo nchi mbalimbali zinaomba na hazijatengwa kwa ajili ya Tanzania peke yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa tunaenda kupata taasisi ya pili sasa kwa upande wa Tanzania Bara ambayo imepata *accreditation* kwa upande wa Mfuko wa Fedha wa *Green Climate Fund*: Je, Ofisi ya Makamu wa Rais imejipanga vipi kuisaidia Zanzibar angalau kuweza kupata taasisi moja ambayo itapata usajili kwa ajili ya Mfuko huu wa Mabadiliko ya Tabianchi ili Wazanzibar nao wawe na *direct access* ya kuomba hizi fedha za mabadiliko ya tabianchi? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Soud maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Soud kwa kazi nzuri anayoifanya hasa ya kutoa elimu kwa wananchi katika masuala mazima ya uhifadhi wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maeneo ambayo tumeshayaainisha au tunayafanya kabla hatujaanza kufanya uteuzi wa hiyo miradi. Kwanza huwa tunatembelea maeneo ambayo tunaweza tukaiibua hiyo miradi ambayo tunaweza kuiingiza huko. Kingine tunachokifanya ni kukusanya taarifa ambazo zinaweza kusaidia na baadaye tunaenda kuziandikia *project proposal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyokuwepo hapo ni kwamba mara nyingi miradi hii inakuwa inasuasua. Kwa hiyo, nataka nichukue fursa hii nitoe wito kwa

Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini, wajitahidi wasimamie vizuri miradi hii, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo fedha zimepelekwa, lakini bado miradi hii inasuasua haijamalizika utekelezaji wake wakati bado kuna baadhi ya maeneo miradi hii imeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuisaidia Zanzibar kupata angalau taasisi; Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ipo wazi, kikubwa ni kwamba tunawaomba waje, tutawaelekeza, tutawafahamisha, tutawaambia namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wakaingiza hizo taasisi. Kikubwa ni kwamba wanaweza wakaandaa pia miradi ili wakija kwetu inakuwa rahisi kuifanyia utekelezaji. Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ambaye anahusika na Mazingira katika Kikao cha Bunge kilichopita alitoa ahadi ya kuja kutembelea Kisiwa cha Pemba ili kuona athari ya mabadiliko ya tabianchi hasa katika Kisiwa cha Mtambwe Mkuu, Kojani na Kisiwa Panza.

Je, ni lini hasa atakuja kuona athari hiyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini unakwenda?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Khalifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge hili tukijaaliwa tutajitahidi tupange ziara kwa ajili ya kwenda Kojani na maeneo

mengine ya Mtambwe Mkuu kwenda kukagua maeneo hayo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Jackson.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi yamesababishwa sana na uharibifu wa mazingira; na mara nyingi ukipita katika milima hii ya Kitonga, Nyang'oro pamoja na kule Makombe unakuta kwamba watu wamekuwa wakichoma mkaa ovyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ulinzi sasa kwenye misitu hii ili uharibifu wa mazingira usiendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mikakati mingi tunayoipanga katika kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira, hasa katika maeneo hayo. Moja ni kwamba tunaendelea kutoa taaluma kwa wananchi kama sehemu ya wajibu wetu kuhakikisha kwamba wananchi hawaendelei na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kine kine kikubwa tunachokifanya, tunayo majeshi yetu kule au walinzi wetu ambao tunashirikiana nao na vikosi vingine vya ulinzi pamoja na Jeshi la Maliasili ambao mara nyingi huwa tunajitahidi kushirikiana nao kulinda mazingira katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

Na. 138

Ujenzi wa Hospitali ya Kanda - Tabora

MHE. JACQUELINE K. ANDREA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Kanda ya Magharibi kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga fedha za ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Magharibi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na tayari kazi ya kuandaa michoro ya hospitali hiyo imeshaanza na upembuzi yakinifu wa eneo ambalo itajengwa kwa kuzingatia ukaribu wa wananchi wote katika mikoa inayounda Kanda ya Magharibi. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu zuri la Serikali, lakini kutokana na umuhimu wa hospitali hii ya Kanda ambayo inajumuisha mikoa mitatu; Kigoma, Katavi na Tabora; nataka majibu ambayo yataweza kutuonesha Wana-Kanda ya Magharibi ni lini hasa hospitali hii itaanza

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kujengwa kutokana na kwamba eneo lilishatengwa kama ambavyo amesema na katika Kata ya Magili kwa hekari 200? Hii itasaidia wananchi wasianze kufanya shughuli za maendeleo kwa kuzingatia ni muda mrefu mchakato huu walishasema utafanyika lakini bado haujafanyika.

Je, Serikali inaweza kutueleza ni lini hasa kazi hii inaweza ikafanyika? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ambavyo nimeshaeleza kwenye swali la msingi kuhusu tathmini; kwanza fedha za kwanza ambazo makadirio ya kuanza, kwa sababu ni fedha ambazo hazitamaliza, lakini zimeshatengwa shilingi bilioni 10 za kuanza, lakini kazi inayofanyika ni kuangalia kwenye mikoa hiyo kuhusu umbali, kwa sababu hatuangalii tu Hospitali ya Kanda kwamba tunaweka Magharibi au wapi, tunaangalia ni mikoa ipi na ni mkoa upi upo mbali na *facillities* kama hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukiangalia kutoka Tabora kuja Benjamin Mkapa ni Kilomita ngapi? Tabora kuja hospitali nyingine ya Kanda ni Kilomita ngapi? Hii itasaidia tuweze kuamua eneo sahihi ambalo huduma itawasogelea wananchi walio wengi na tuangalie eneo ambalo vile vile huduma nyingine ziko mbali na wananchi ambazo wengine wako karibu nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, upembuzi bado unafanyika ili kutambua eneo ambalo hospitali itaenda kuwekwa kwa kutumia busara kusogezea huduma wananchi walio wengi zaidi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Prof. Ndakidemi.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa. Shida ya kujengewa hospitali katika Kanda ya Magharibi inafanana kabisa na shida tuliyonayo Wilaya ya Moshi.

Je, ni lini Serikali itatujengea Hospitali ya Wilaya ya Moshi kwa sababu tayari tumeshapata eneo la ekari 38?
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Mimi mwenyewe nimetembelea eneo hilo ambalo anasema limetengwa, nimellona. Kikubwa ni kwamba tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ili kwenye bajeti ya mwaka huu tuweze kuona ni namna gani utekelezaji wa hilo hitaji lao litafanyika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suma Fyandomo.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwetu kule Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Rungwe kuna hospitali kubwa sana ambayo ilikuwa ikiwatibu watu wenye ugonjwa wa ukoma na watu kutoka nchi mbalimbali walikuwa wakitibiwa ikiwa ni pamoja na Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali ile, ukoma ulifungwa rasmi mwaka 2002. Majengo yale ni hospitali kubwa ambayo ina wodi ya wanaume, wanawake na watoto, ina mochwari, bwalo, jiko kubwa, mpaka machine ya kuchomea takataka na Makanisa yapo pale, pia heka zaidi ya 100 ziko pale, lakini yamekaa bila kufanyiwa kazi yoyote:-

Je, Serikali ina mpango gani na majengo yale?
Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujibu swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, ameeleza kwamba kuna hospitali yenye *facillities* hizo. Sasa niweke tu vizuri kwamba suala la ukoma, bado tunaenda kuongeza nguvu kwa sababu tunataka mwaka 2030 ukoma uwe umeisha kabisa Tanzania. Ila wazo lake hilo ambalo anasema kuna *facillity* hiyo ambayo inaweza kutumika kwa namna nyingine;

baada ya Bunge tarehe 24, nitakuwepo Njombe, nitapitia Songwe kuangalia Hospitali ya Mkoa wa Songwe halafu tutaenda pamoja kutembelea hilo eneo na watalaam ili tuweze kuamua kwa kuangalia mazingira halisi na kuleta majibu ambayo yatakuwa sahihi kulingana na hali halisi ya kule. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu unakwenda. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla.

Na. 139

Tatizo la Kukatika kwa Umeme Wilaya ya Urambo na Kaliua

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza mchakato wa Wilaya ya Urambo na Kaliua kutumia *line* yake ya umeme ili kupunguza au kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme katika Wilaya hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya za Urambo na Kaliua zinapata umeme kwa njia moja inayoanzia Kituo cha Kupooza Umeme kilichopo Tabora Mjini. Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kupooza Umeme katika Kijiji cha Uhuru, Wilayani Urambo, kitakachopokea umeme mkubwa (*Kilovolt 132*) kutoka Tabora Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi unaendelea, jengo la kupokelea Umeme (*Control Building*)

limekamilika, upimaji wa njia ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo umekamilika, uthamini wa mali za wananchi watakaopitiwa na mradi umekamilika na mikataba ya wazabuni watakaoleta vifaa vitakavyotumika kwenye ujenzi (wa njia na vifaa vya umeme) imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hicho kitakuwa na njia za usambazaji umeme (*distribution lines*) zinazojitegemea kwa kila Wilaya, yaani Urambo moja na Kaliua moja na hivyo kufanya ziwe na Umeme wa Uhakika zaidi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu haya mazuri ya Serikali tunaomba yasiishie kwenye maandishi, tunataka kwa vitendo na kwa muda husika, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitutangazia bei, hasa sisi watu wa vijijini kwamba, gharama ya kuunganisha umeme ni 27,000/= lakini haikuweka wazi hiyo 27,000/= inajumlisha nini na nini. Sasa tunataka tufahamu;

Je, Serikali inaposema 27,000/= inajumuisha na nguzo bila kuangalia umbali wa mlaji wa mwisho? Kwa sababu, maeneo mengi unalipa 27,000/= lakini hawapelekewi umeme na kila wakiuliza wanaambiwa tatizo ni nguzo, tunataka leo utupe maelezo yanayojitoshleza kuhusu hili tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili. Kumetokea mabadiliko ya ghafla sana na ya kimyakimya kuhusu bei ya umeme kulingana na *units* ambazo mnazitoa. Hapo nyuma wananchi walikuwa wakilipa 10,000 wanapata *units* 78, lakini sasa hivi mabadiliko haya yameasababisha 10,000 hiyo hiyo wanapata *unit* 28. Sasa je, tunataka tufahamu nini kimesababisha haya mabadiliko ya kimyakimya kwa hizi *units* ambayo inawatesa sana hawa wananchi wetu ambao ni masikini? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rehema, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza niombe kutoa maelezo mazuri kabisa fasaha kwa niaba ya Serikali kwamba, ukilipa 27,000/= utaletewa umeme ulipo pale kijijini, hata kama ni kwa nguzo 20, ni nguzo moja, ni bila nguzo, maelekezo ya Serikali, gharama ya kuunganisha umeme kwa kijijini ni 27,000/=. Na mara nyingi unapounganisha umeme utahitaji mita, utahitaji nguzo, utahitaji waya, utahitaji *transformer* pia, ni 27,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna maeneo ambapo tunapata matatizo Waheshimiwa Wabunge, basi tuwasiliane ilki msimamo huu wa Serikali uweze kutekelezwa katika maeneo ambayo yanahusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika eneo la pili, kwa taarifa zilizopo, mabadiliko ya bei za umeme ya mwisho yalifanyika mwaka 2016 kwa kanuni zilizotolewa na msimamizi wa bei ambae ni *EWURA*. Mpaka sasa hatuna taarifa na hatuna maelekezo na hatuna mabadiliko yoyote yale kwenye gharama za umeme. Lakini wale watumiaji wadogo, tunawaita *Domestic 1*, maarufu *D 1*, ukiwa na 9,150/= utapata *unit 75*, lakini kama utatumia zaidi ya *unit 75* kwa mwezi unakidhi kutoka kwenye *D 1* kwenda *T 1* hivyo, 9,150/= haiwezi kununua tena *unit 75* unakuwa ume-*graduate* kwenda kwenye matumizi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kama kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wananchi wao bado wanatumia *unit 75* na pungufu kwa mwezi, lakini gharama za ununuzi wa umeme zimebadilika kwao, basi tuwasiliane ili tuweze kubaini tatizo ni nini, tuondoe hilo tatizo, lakini hakuna mabadiliko ya wazi wala ya kimya ya gharama za umeme. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, nami niulize swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkansi ni miongoni mwa wilaya ambazo zinapata umeme kwa muda mfupi sana. Wizara ya Nishati ilisema wanaweza kuondoa tatizo hilo kwa kutuunganisha kwenye gridi ya Taifa kwa hiyo, tunatumia umeme kutoka Zambia.

Nataka kujua kama Wizara bado inaamini mpaka leo kwamba, kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa ndio suluhisho, ni lini mtatuunganisha kwenye gridi ya Taifa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza miradi miwili kwa pamoja ya kupeleka gridi ya Taifa katika Mkoa wa Katavi na Kigoma kwa pamoja. Na gridi hiyo ya Taifa inatarajiwa kufika maeneo hayo ifikapo Oktoba mwaka huu. Na itakapokuwa imefika Katavi ndio sasa tutakamilisha mpaka maeneo mengine ya Jirani ambayo hayana gridi ya Taifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leah, jandae Mheshimiwa Mtenga.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isiiondoe Wilaya ya Meatu kuchukulia umeme katika Kituo cha Mabuki, Mwanza, chenye umbali wa kilometa 200 ikairejesha Wilaya ya Meatu ilikokuwa mwanzo inachukulia Ibadakuli, Shinyanga, umbali wa kilometa 100 ili kuondoa tatizo la

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kukatikakatika kwa umeme, ambalo linasababishwa na umeme kusafiri umbali mrefu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka eneo moja kupata umeme kutoka sehemu nyingine ni jambo la kitaalamu na sio kwa kuangalia umbali peke yake, lakini pia na uwezo wa kituo fulani kuhudumia watu wetu walioko jirani, lakini naomba nikiri kwamba, nachukua jambo hilo na nitaenda kuliwasilisha kwa wataalam ili walichakate na kuona kama kwa sasa tunaweza kuhama kutoka upande hu una kwenda kwingine, kwa ajili ya kuboresha huduma hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtenga.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mtwara Mjini ni jimbo ambalo kwa sasa linaongoza kwa ukatikaji wa umeme kwa kila siku, mikatiko inaweza ikafika zaidi ya 30 kwa siku. Je, ni lini Serikali itaiingiza Mtwara na Lindi kwenye gridi ya Taifa na sisi tukafaidika na umeme wa gesi ambayo inatoka Mtwara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru wana-Mtwara kwa kuwa, sehemu kubwa sana ya umeme ambayo inalisha nchi hii kwenye gridi ya Taifa inatokea katika Mkoa wa Mtwara. Na nimuahidi kwamba, katika mipango ambayo

Serikali ikonayo ni kuhakikisha kwamba, sasa umeme ambao unazalishwa tayari kwenye gridi ya Taifa na kwenyewe uweze kufika. Niseme kwenye mipango tuliyokuwanayo kufikia 2025 itakuwa imefikia hatua sasa ya kuamua ni lini gridi ya Taifa itafika katika Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi kwa ajili ya kufikisha huduma nzuri zaidi.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mkundi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Wilaya ya Ki-TANESCO ya Ukerewe inapata umeme kutoka kwenye kituo cha kupoza umeme kilichoko Bunda, ambako ni umbali mrefu, hali inayosababisha kutokuwa na umeme wa uhakika. Na kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga vituo kadhaa vya kupoza umeme kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini sasa Serikali isiweke Ukerewe kama moja ya maeneo ambayo yatajengewa kituo cha kupoza umeme, ili kurahisisha umeme wa uhakika kwenye eneo la Ukerewe? Nashukuru sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kulichukua jambo hili, ili wataalam waende wakachakate na kuona *economic feasibility* ya kuweka kituo pale Ukerewe na uwezo wa kukitumia katika mahitaji tuliyonayo, ili kuweza kuboresha huduma ya umeme katika eneo la Ukerewe.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea Wizara ya Madini, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika.

Na. 140

Kuwawezesha Wachimbaji Wadogo wa Madini – Njombe

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuwasaidia Wachimbaji wadogo wa madini katika Mji wa Njombe kama inavyofanya kwenye maeneo mengine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwasaidia wachimbaji wadogo Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa imeandaa mkakati maalumu kwa ajili ya kuwasaidia na kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini ikihusisha wachimbaji waliopo Mkoani Njombe, pia. Mkakati huo ambao umeanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2021/2022 umejikita kwenye maeneo manne muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni Mpango wa Mafunzo (*Training Calendar*) kwa mwaka mzima ambao utafanyika nchi nzima. Mpango huo uliandaliwa kwa kushirikisha wachimbaji wadogo kupitia uwakilishi wa vyama vyao (*FEMATA*) na ambao kwa sasa upo tayari kwa utekelezaji. Mafunzo haya yatatotelewa kwa kuhusisha Taasisi mbalimbali zinazohusika na utozaji wa kodi na tozo mbalimbali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Tume ya Madini pamoja na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa pili ni Mpango wa kuwawezesha wachimbaji wadogo kukopesheka katika taasisi za fedha ambapo tayari Shirika limeishaingia

makubaliano na Taasisi za fedha za ikijumuisha *CRDB*, *NMB* na *KCB* ambazo zipo tayari kuwakopesha wachimbaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Tatu ni Kuingia makubaliano na *GST (Geological Survey of Tanzania)* taasisi yetu ya jiojio, ambayo itawasaidia wachimbaji wadogo kujua taarifa za mashapo katika maeneo yao kabla hawajaanza kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Nne ni Kupata mitambo ya uchorongaji mahususi kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kwa kuanzia Shirika limeagiza mitambo 5 ya uchorongaji mahususi kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwanza, kwa vile wananchi wachimbaji wa Njombe, kupitia chama chao cha wachimbaji kinaitwa WANANJO, walishafikisha kilio kwa Mheshimiwa Waziri na Waziri akatoa maelekezo kwa Katibu Mkuu kwamba, watafutiwe na watengewe maeneo kama inavyofanyika maeneo mengine katika nchi yetu. Na kwa vile mchakato huo ulishafanyika na *RMO* alishafikisha hayo mapendekezo ya maeneo wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, ni lini sasa wananchi hawa watapelelewa hayo maeneo ambayo tayari yameshatambuliwa kwamba, ni muhimu kwa uchimbaji wa wachimbaji wadogo wa Njombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, ameongelea kuwasaidia kwa kupitia *training* mbalimbali pamoja na mikopo. Wananchi, wachimbaji wale, hawana Habari na hiyo *training* ni kalenda ambayo Wizara wamejipangia. Naomba tupate uhakika na wao wasikiae,

ni lini mafunzo haya yatafanyika katika Mkoa wa Njombe?
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la kwanza ambapo anataka kujua kwamba, wachimbaji wadogo walioahidiwa maeneo ya kuchimba makaa ya mawe, na ninafahamu ni katika eneo la Ludewa, ni lini watapewa hayo maeneo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia kwamba, taasisi yetu husika ambayo ni Tume ya Madini walishakwenda kupima maeneo hayo na mpaka sasa wameshapata kilometa za mraba 10.33 ambazo zinatoshia kutoa leseni za wachimbaji wadogo 120. Na wanaendelea kutafuta maeneo ya ziada ili kuwapatia wachimbaji wote wadogo maeneo ya kuchimba kulingana na maombi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, napenda kumhakikishia Mbunge, Ndugu yangu Mwanyika ambaye nampongeza sana kwa jinsi anavyowapambania wachimbaji wake wadogo kule katika jimbo lake ya kwamba, ratiba ilishapangwa. Taasisi yetu husika imeanza kuzunguka katika Kanda ya Ziwa tunavyoongea wanatoa mafunzo mbalimbali. Na mwaka huu wa fedha kabla haujaisha watakuja pia na Mbeya na GST nao wale wanaofanya mambo ya jiolojia watakuja kutoa semina katika mwaka ujao wa fedha ya jinsi ya kuchukua sampuli na jinsi ya kutambua maeneo yenye madini kwa ajili ya kunufaisha wachimbaji wadogo. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

Na. 141

Serikali Kununua Magari ya Zimamoto

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itanunua Magari ya kisasa ya Zimamoto ili kunusuru maisha ya raia na mali zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mpango mkakati wa kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji nchini kwa kuimarisha na kuongeza vifaa vya kisasa vya utendaji kazi katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Vifaa hivi vya kisasa vitaenda sambamba na upelekaji wa huduma ya zimamoto na uokoaji katika wilaya zote ambazo hazina huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini imetenga bajeti ya maendeleo ya shilingi bilioni 2 katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kununua magari mapya ya kisasa ya zima moto. Lengo la ununuzi wa magari haya ni kuongeza ufanisi kwenye shughuli za kuokoa maisha na mali za wananchi, pindi patokeapo ajali za moto na nyingine. Taratibu zote za ununuzi zikikamilika, magari ya kuzima moto yatapelekwa mikoa isiyokuwa na huduma ya zimamoto na uokoaji. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuliwezesha vitendea kazi stahiki Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza niseme nasikitishwa na majibu ya Serikali:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu jinsi Taifa letu linavyokumbwa na majanga mbalimbali ya moto, kama kuungua kwa masoko, shhule, nyumba binafsi na hata kwenye biashara mbalimbali kama hoteli na vinginevyo, ambayo inasababisha hasara kwa mali za raia, lakini hata uhai wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, magari ya kisasa, *on average*, ni kuanzia milioni 500 na kuendelea. Na bajeti ya Serikali imeonesha kutenga bilioni mbili tu kwa maana ya kwamba, watanunua walao magari manne tu tena hayo ni ya wastani. Ni kwanini sasa Serikali isione umuhimu wa kutenga fedha kwa udharura, ili waweze kununua magari walao mawili katika kila halmashauri, kama ambavyo wanafanya kwenye magari ya washawasha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, sote tumeshuhudia wakati wa chaguzi ambazo zinafanyika kila baada ya miaka mitano kwenye majimbo yetu kunakuja magari ya washawasha zaidi ya mawili matatu, ambayo gari moja la washawasha ni takribani milioni 500, kama ilivyo kwa gharama za gari la zimamoto. Je, kipaumbele cha Serikali ni kipi kati ya kulinda mali ya raia na uhai wao dhidi ya kudhibiti wapinzani wakati wa uchaguzi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. Serikali inatenga fedha mwaka huu, imetenga mwaka jana bilioni mbili na nusu, mwaka huu

imetenga bilioni mbili. Tutaendelea kutenga fedha hizo au zaidi kutegemea upatikanaji wa fedha ili kuimarisha jeshi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikumbushe. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halifanyi kazi peke yake, hushirikisha majeshi mengine na vituo vingine kama viwanja vya ndege, bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tunathamini mali na wananchi wetu kwa hiyo, mfano anaoutoa wa washawasha hauna uhusiano wa moja kwa moja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi, ajiandae Mheshimiwa Mafuwe.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ilikuwa na gari zuri la zimamoto, gari ambalo lilikuwa ni la kisasa. Kwa bahati mbaya lilipata ajali mwaka 2015, toka Serikali imelichukua kwa ajili ya matengezo, gari hilo halijaweza kurejeshwa Mpanda. Swali langu, ni lini Serikali itaturejeshea gari hilo zuri na la kisasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *interest* na Tanga kutokana na miradi mingi mliyonayo ya kiuchumi ikiwemo bandari na bomba la mafuta linalopita pale. Tutafuatilia baada ya Bunge hili kuona kwamba, matengenezo ya gari hilo yanakamilika lirejeshwe Tanga kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mafuwe. Jiandae Mbunge wa Temeke.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchakavu wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Hai, lakini Wilaya ya Hai ina watumishi 149, hakuna nyumba hata moja ya watumishi hawa, kiasi kwamba, *OCD, OC-CID* na Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Hai anakaa mbali sana kwa hiyo, wanashindwa kutoa huduma pale. Ni lini sasa Serikali itajenga walao hata nyumba moja tu ya Mkuu wa Kituo Wilaya ya Hai?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuweka mazingira bora ya utendaji wa kazi wa vyombo vyetu vya ulinzi, hasa vya usalama, ikiwemo Polisi, Zimamoto, Magereza, n.k. Kama nilivyosema katika jibu nililotoa juzi, tunaendelea kutenga fedha na mwaka huu zipo fedha zimetengwa kwa ajili hiyo. Lengo ni kuhakikisha kwamba, maeneo yote ambayo hayana nyumba yanapewa kipaumbele ikiwemo wilaya yako ya Hai. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kilavi.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, swali langu mimi ni, kule Temeke Kata ya Sandali, kuna jengo kubwa sana ambalo mmelijenga la zimamoto, lakini mpaka sasa halijamaliziwa wala hakuna vifaa vyovyote ambavyo vimeingizwa kwa ajili ya zimamoto.

Je, ni lini sasa vifaa hivi pamoja na jingo lile litamalizika kwa ajili ye Serikali yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, anazungumzia eneo la Mchicha.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nalifahamu amelizungumzia suala hilo la eneo la Mchicha majuzi, tutalipa kipaumbele kwa *interest* ya watu wa Dar es Salaam, uchumi wao na shughuli nyingi za kiviwanda zinazotekelezwa ili kuwawezesha *Fire* kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi.

Na. 142

Uzalishaji wa Madume Bora ya Ng'ombe

MHE. KENNETH E. NOLLO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha uzalishaji wa madume bora ya ng'ombe Wilayani Bahi ili kuleta tija kwa wafugaji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuimarisha mashamba yake ya uzalishaji wa madume bora ya Mabuki, Mwanza; Kitulo, Njombe; na Sao Hill lililopo Mkoani Iringa ili yaweze kuzalisha madume mengi na bora kwa lengo

la kuyasambaza kwa wafugaji wote wanaohitaji ikiwa ni pamoja na wafugaji wa Wilaya ya Bahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali inaendelea kusisitiza matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji katika kuboresha kosaafu za ng'ombe ili kuwa na kundi la mifugo yenye tija katika kuzalishaji nyama na maziwa na hivyo kukidhi mahitaji ya soko.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nollo.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika Wilaya ya Mpwapwa kuna idadi kubwa sana ya mifugo, lakini changamoto yetu kule ni ukosefu wa mfumo rasmi wa upatikanaji wa madawa kwa ajili ya kutibu mifugo yetu. Wafugaji kule wanategemea sana walanguzi ambao wakati mwingine wamewauzia dawa feki na zimewasababishia hasara. Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu rasmi wa kuhakikisha kwamba wafugaji wetu wanapata dawa za kutibu magonjwa ya mifugo katika maeneo yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwenye vitengo vyetu vya Baraza la *Veterinary* Tanzania na *TMDA* kwa pamoja tunafanya *operations* za mara kwa mara za kufuatilia dawa zisizo na viwango. Kwa mwaka jana tulikamata na hatua za kisheria zilichukuliwa na mwaka huu pia vile vile Mkoani Mwanza tayari yuko mzalishaji na msambazaji wa dawa feki ambaye tumemkamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wetu sasa kupitia Baraza hili ni kuhakikisha kwamba uhibitaji wa dawa hizi unaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuzalisha dawa nyingi zaidi

zilizobora kupitia viwanda vyetu vya hapa nchini pamoja na kiwanda cha Serikali kilichoko pale Kibaha kwa maana cha TV ili wafugaji wetu waweze kupata uhakika wa chanjo na dawa zenye kukidhi viwango.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, hivyo tunaendelea na Wizara ya Maliasili Mheshimiwa Manase Njenzu Oran.

Na. 143

Mgogoro wa Ardhi Kati ya TFS/TANAPA na Wananchi

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa muda mrefu wa ardhi kati ya TFS/TANAPA na wananchi wa Kata za Inyala, Itewe na Ilungu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa Kitulo haina mgogoro na vijiji vya Kata za Inyala, Itewe na Ilungu. Changamoto iliyopo ni kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kwa wananchi wa maeneo hayo kwa ajili ya kufanya shughuli za kiuchumi. Maeneo hayo yalikuwa yanatumwa kinyume cha sheria kwani kwa eneo ambalo ni Hifadhi ya Taifa Kitulo lilikuwa ni shamba la Serikali la mifugo ambamo ndani yake kulikuwa na (ng'ombe na kondoo wa sufu) lililojulikana kama Kitulo *Dairy Farm*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wa ardhi zaidi, wananchi wamekuwa wakidai

maeneo waliyo kuwa nayo wanatumia kabla ya Hifadhi ya Taifa Kitulo kuanzishwa mwaka 2005 yarudishwe kwao ili kukidhi mahitaji zaidi ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*) imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi na hifadhi za mazingira kwa ujumla ili kutatua changamoto hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Inaelekea kuna mkanganyiko kidogo kwenye majibu ya Serikali, kwa sababu mwaka 2007 wananchi wa Kata ya Ilungu hususan Kijiji cha Kikondo walifanyiwa tathmini ya kupewa fidia kwa yale maeneo yaliyochukuliwa na *DAFCO* ambayo sasa hivi ndiyo Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo wenzetu wa *TANAPA* walishindwa kuwafidia wale wananchi, kwa hiyo yale maeneo hasa Kijiji cha Kikondo bado yanatumika ni kijiji ambacho kina shule kina zahanati. Pia kuna maeneo ambayo yalichukuliwa na watu wa *TFS* kwenye Misitu ya Mwambalis na hayo maeneo yamekuwa yakitumiwa na wananchi hata kabla ya hapo na mpaka leo yanatumwiwa.

Sasa kutokana na mkanganyiko wa majibu, naomba Mheshimiwa Waziri apange ziara akayatembelee hayo maeneo ili afanye tathmini yeye mwenyewe ili kujua uhalisia, lakini hali siyo nzuri kuna mgogoro na wananchi kwa kweli wanapata shida sana. Nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto hizi ambazo mara nyingi wananchi wamekuwa wakihitaji ardhi wakati huo huo maeneo haya yalichukuliwa na Serikali. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto hizi tutaenda kuzifuatilia, lakini pia tutaenda kukutana na wananchi ambao wamekutana na kadhia hii na lengo ni kukaa pamoja ili kuweza kutatua changamoto hii. Hivyo nitafika kwake kwenda kutatua changamoto hii. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae Mheshimiwa Dennis Londo.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante hili suala la Hifadhi ya Kitulo liko pia Makete ambako ni wilayani kwangu. Kuna mgogoro mkubwa kati ya wananchi na Hifadhi ya Kitulo kwa sababu uwekaji wa *beacon* ya mipaka haukushirikisha wananchi kitu ambacho kimesababisha mgogoro mkubwa. Pia tuna hifadhi ya Mpanga Kipengele ambako kuna Vijiji vya Ikovo, Kimani na kwenye Hifadhi ya Kitulo mgogoro mkubwa uko kwenye Vijiji vya Chankondo, Misiwa kule Itelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bunge hili ilituahidi kwamba itakuja Makete kutatua hii kero na haijaja hadi leo. Ile timu ya Mawaziri Nane pia ilisema itafika Makete haijafika hadi leo.

Je, ni lini Serikali itakuja kutatua changamoto hii ya migogoro ili wananchi wangu waweze kupata maeneo kwa kufanya kazi kwa sababu ndiyo waliotumia kuhifadhi hii Hifadhi ya Kitulo hadi Serikali imekuja kuichukua mwaka 2005?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambaye aliandaa Kamati ya Mawaziri Nane ambao walikuwa wanapaswa kuzunguka nchi nzima. Zoezi hili tulilianza kipindi cha mwaka uliopita na tulizunguka kwenye baadhi ya maeneo. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Sanga kwamba zoezi hili bado ni endelevu tutafika kwenye maeneo yote yenye migogoro na tutatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale ambayo yameshapitiwa na kamati hii tutahakikisha kwamba yanarudishwa kwa wananchi. Yale ambayo ni migogoro mipya Mheshimiwa Waziri ameshaunda kamati nyingine ambayo tumeanza kupitia tena upya maeneo ambayo yana migogoro ili kuhakikisha kwamba wananchi na maeneo ya hifadhi yanahifadhiwa vizuri na wakati huo huo wananchi wanaendelea na shughuli zao za kila siku. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Londo.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama kuna mkoa ambao ulikuwa unasubiri kwa hamu ile Timu ya Mawaziri Nane ni mkoa wa Morogoro. Jimbo la Mikumi, Kata za Zombo, Muhenda, Kisanga na Mikumi zimekuwa katika changamoto ya muda mrefu ya mipaka kati yao na *TFS*, kati yao na *TANAPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna timu ambayo imeundwa na Waziri kuorodhesha migogoro hiyo. Je, kata hizo na vijiji hivyo vya kata hizo zinaenda kuingia katika orodha ndefu ya vijiji vyenye migogoro? Nawakilisha.

NAIBU SPIKA: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili naomba nilifafanue kwa ufasaha zaidi kuna ile migogoro ambayo inapitiwa na Mawaziri Nane. Hii migogoro Mawaziri Nane watapita kwenye maeneo nchi nzima na watatua hii migogoro. Hata hivyo, kuna migogoro mipya ambayo haikuwahi kupitiwa na Kamati ya Mawaziri Nane. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ameunda Kamati ndani ya Wizara imehusisha na maeneo mengine kwa maana ya watumishi wa ardhi na maeneo ya mazingira kupitia mapori ya hifadhi, kupitia ramani moja baada ya nyingine kuangalia huu migogoro unatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna migogoro mingine ni ya *beacon*, kuna migogoro mingine wamesogea kidogo, kwa hiyo kuna mabishano kati ya mipaka na mipaka. Kamati hii itapita tena upya na itaangalia pale ambapo pana migogoro tutautatua kwa pamoja na tutazisoma ramani tuta-*define* mipaka na baadaye tutatoa majibu sahihi ili wananchi waridhike na maeneo ya hifadhi, lakini wakati huo huo watendewe haki kuliko ilivyo sasa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza nianze kuipongeza Wizara ya Maliasili kwa kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Nyangh'wale kuweza kutokomeza wanyama wakali kama vile fisi ambao walipoteza maisha ya wananchi wangu wa Jimbo la Nyangh'wale. Sasa swali, je, ni lini Waziri atapanga ziara ya kuja kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Nyang'wale lakini pia kifuta machozi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein, Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuelezea changamoto hii ya fisi. Ni kweli kumekuwa na changamoto, fisi wanakuwa wamebaki kwenye maeneo ambayo siyo ya hifadhi na wamekuwa wakiwadhuru wananchi. Zoezi hili tulishaelekeza watendaji, pengine na hapa tena nitoe maelekezo kwamba watendaji walioko Kanda ya Mwanza, nikimaanisha magharibi tuandae *operation* ya kwenda kuwasaka wale fisi wote ambao hawako kwenye maeneo ya hifadhi na kuwarejesha kwenye maeneo ya hifadhi ili kunusuru hali za wananchi wa Jimbo la Nyang'wale. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

Na. 144

Ujenzi wa Barabara ya Lushoto – Mlalo

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Lushoto – Magamba – Lukozi – Mlalo hadi Umba Junction kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Lushoto – Magamba – Lukozi – Mlalo hadi Umba *Junction* ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometa 66.23 na inasimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*), Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 9.1 kati ya Lushoto na Mazinde Juu zimejengwa kwa kiwango cha lami. Mwaka huu wa fedha 2021/2022, jumla ya Shilingi milioni 420 zimetengwa ili kuendeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kipande chenye urefu wa mita 400. Kazi za ujenzi zilianza mwezi Januari, 2022 na kazi zinategemewa kukamilika mwezi Juni, 2022. Hadi tarehe 10 Februari, 2022 kazi zilikuwa zimefikia asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa awamu kulingana na upatikana wa Fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Husna.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Lushoto, Magamba, Lukozi, Mlalo mpaka Umba *Junction* ni uti wa mgongo wa shughuli za maendeleo na kujenga uchumi wa wananchi wa eneo hilo. Vilevile barabara hii ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya 2015 hadi 2025. Kwa kuwa ipo ahadi ya Serikali ya kuanza kujenga barabara hii kutoka kilometa moja moja inayofanywa sasa, kwenda katika kujenga kilometa 10, 10 kila mwaka. Je, ni lini sasa Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, imetengwa bajeti kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kutoka mwanzo mpaka kwenye *junction* ya mwisho ya barabara hii. Je, ni ipi *commitment* ya Serikali katika kufanya usanifu wa kina na upembuzi yakinifu katika barabara hii ili iweze kuwa mradi kamili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara iko kwenye ilani na ni ahadi ya viongozi, lakini nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Shangazi ambaye najua barabara hii inamhusu sana ameshahakikishiwa na Wizara kwamba katika mwaka huu wa fedha, barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kwa sababu ilikuwa haijafanyika hivyo ndiyo maana ilikuwa ni kusanifu na kujenga. Kwa hiyo tunahakikisha barabara hii itafanyiwa usanifu katika mwaka wa fedha ujao kwa barabara yote. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Gatiki Chomete.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kulikuwa na mpango wa ujenzi wa barabara ya Tarime kupitia Nyamwaga, Nyamongo mpaka Serengeti lakini kuna taarifa kuwa mpango huo haupo. Je, ni nini tamko la Serikali juu ya barabara hiyo kwa wananchi wale? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni swali lingine tena naulizwa, siku mbili zilizopita liliulizwa swali kwenye barabara hii hii. Naomba nimjibu Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mara kwa kumhakikishia tu kwamba, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, jana amekuja ofisini akiwa na madai haya haya, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na wananchi wa Tarime, mpango huu unaosemwa hakuna mpango uliofutwa. Nataka nimhakikishie kwamba tayari tuko kwenye hatua za kusaini mkataba kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia Tarime hadi Nyamwaga, kilometa 25 na zabuni inaandaliwa kuanzia Nyamwaga hadi Mugumu kilometa 61. Jumla kilometa hizo 82, kwa hiyo hakuna mpango uliofutwa na iko kwenye mpango.

NAIBU SPIKA: Ameshakuelewa Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa mAjibu mazuri. Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa changamoto iliyopo kwenye barabara ya Lushoto mpaka Mlalo inafanana na changamoto iliyo kwenye barabara ya kutoka Makofia – Mlandizi mpaka Vikumburu.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kipande hiki cha kutoka Makofia – Bagamoyo mpaka Mlandizi kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alice Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii iko kwenye ilani na imetengewa bajeti kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami mwaka huu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi utaanza mara tu fedha itakapokuwa imepatikana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Condester

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mloo - Kamsamba - Utambalila kupitia Chitete yenye kilometa 145.14 iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 kwenye ukurasa wa 75:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ni lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilishafanya maandali ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Tayari usanifu wa kina umeshafanyika. Changamoto iliyokuwepo ya Daraja la Momba, imejengwa kwa ajili ya kupokea barabara hiyo. Kwa hiyo, itategemea na fedha zitakapopatikana, kwa sababu taratibu zote za awali zimeshakamilika ili barabara hii ambayo inaunganisha Mkoa wa Songwe, Mkoa wa Rukwa hadi Katavi iweze kujengwa. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

Na. 145

**Ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto –
Chemba – Singida kwa Kiwango cha Lami**

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Chemba hadi Singida utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi wa ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo - Chemba – Kwa Mtoro hadi Singida ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometa 461 inayounganisha Mikoa ya Tanga, Dodoma, Manyara na Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa barabara hii umeanza ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2018. Zabuni ya kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Handeni – Mufulate (Kilometa 20) zilishatangazwa na Mkandarasi kupatikana. Rasimu ya Mkataba imepeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata idhini *(vetting)* ya kusaini Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya kutangaza zabuni ya ujenzi kwa sehemu ya kutoka Mafuleta – Kwediboma yenye urefu wa kilometa 30 yanaendelea na zabuni itakuwa imetangazwa kabla ya Juni, 2022. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, binafsi naomba kwanza kuipongeza Serikali kwa kuamua kuanza kujenga hata hizo kilometa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, inaunganisha mikoa minne, kwa maana ya Mkoa wa Tanga, Manyara, Dodoma na Singida. Kama hiyo haitoshi, ni kwamba barabara hii ni barabara ambayo Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanga ndiko linakopita. Sasa nataka kuuliza swali.

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa haraka na kuhakikisha kwamba kilometa zote 461 zinakamilika?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara ya kupita barabara hii mwaka 2021; na kipindi hiki mvua zinanyesha.

Je, yuko tayari kumwagiza Meneja Barabara Mkoa wa Tanga aweze kufanya marekebisho katika maeneo ambayo yameharibika?Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Kigua pamoja na Waheshimia wote ambao barabara hii inawagusa ambao wamekuwa wanaifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wameipitisha barabara hii kama ni barabara ya kipaumbele kutokana na umuhimu wake kwa ajili ya bomba la mafuta. Maana linapopita bomba la mafuta ndiyo barabara hii inakopita. Kwa hiyo, Serikali ina mpango kwa kushirikiana na nchi nyingine kutafuta fedha ili ikiwezekana kilometa zote hizi 461 ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, naomba tu kama tulivyotoa agizo kwa wakuu wote wa *TANROADS* wa Mikoa ahakikishe kwamba anakwenda kwenye madaraja na maeneo yote ambayo yamepata changamoto ya usafiri katika Mkoa wa Tanga; siyo tu kwa Mheshimiwa Kigua, ni pamoja na barabara zake zote ili kuhakikisha kwamba wananchi hawakwami katika kipindi hiki cha mvua. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Samweli.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka 2021 alifika kwenye Barabara ya Haydom - Katesh na amejionea hali ya ile barabara ambayo inategemewa na wananchi kwa shughuli za kilimo pamoja na huduma mbalimbali:-

Je, ni lini wananchi wa Jimbo la Hanang na Mbulu watawaona wakandarasi wakiwa kwenye kazi kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafuatilia na kuona kwamba wakandarasi hawa wanakuwepo *site* haraka inavyowezekana. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kwenye swali la msingi kulikuwa na hiyo barabara ya Kiberashi na imetengewa Kilometa 25 na *tender* imeshatangazwa; na Mbulu Vijijini, barabara ya Haydom – Mbulu kulikuwa na *tender* ya namna hiyo hiyo:-

Je, unataumbaje; tenda hiyo imetangazwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ziko nyingi, ikiwepo moja ya Mheshimiwa Flatei Massay ambayo iko kwenye hatua za mwisho za kusainiwa mikataba ili wakandarasi waanze kazi. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mohamed Maulid Ali.

Na. 146

Uhifadhi wa Maji ya Mvua

MHE. MOHAMED MAULID ALI aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kujikita zaidi kwenye uchimbaji wa Malambo ya kuhifadhi maji ya mvua na kujenga mabomba ya kuchukua maji toka kwenye maziwa na mito yote kuliko kuendelea kutumia gharama kubwa za kuchimba visima bila mafanikio?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Maulid Ali, Mbunge wa Kiembe Samaki, kama lfuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa uvunaji wa maji ya mvua kupitia mabwawa unatekelezwa kwenye maeneo mengi nchini ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, kazi ya ukarabati na ujenzi wa mabwawa na malambo inaendelea katika vijiji 20 vya Mlele, Kisarawe, Bunda, Kalambo, Mkinga, Handeni, Chalinze, Songwe, Chamwino, Chemba, Bahi, Kaliua, Kilindi, Itilima, Kishapu, Monduli, Kibaha na Kondoa. Aidha, kazi ya kuainisha maeneo 58 yanayofaa kujenga mabwawa madogo na malambo imefanyika na ujenzi utafanyika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali ni kuhakikisha miradi ya maji inajengwa kwa kutumia vyanzo vya uhakika ambavyo ni maziwa makuu na mito mikubwa. Mradi huo ni wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Shinyanga, Kahama, Tabora, Igunga na Nzega Bukoba, Musoma, Misungwi na Magu. Vilevile, Utekelezaji wa miradi ya Mugango, Kiabakari, Butiama, Tinde, Shelui, na mradi wa maji katika miji ya Busega, Bariadi na Lagangabilili unaendelea kupitia Ziwa Victoria na mradi wa maji wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kupeleka Kigoma Mjini, Kirando na Kabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, Serikali imeanza mpango wa kutekeleza miradi kupitia maziwa makuu ili kunufaisha maeneo ya pembezoni mwa maziwa hayo; kwa upande wa mito; mradi wa maji wa Kyaka - Bunazi ambao unatumia maji ya mto Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji yanayotokana na maji ya chini ya ardhi ni katika maeneo kame ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji juu ya ardhi. Haya maeneo ni kama vile Dodoma, Singida, Lindi, Simiyu, Kigoma na Katavi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Maulid.

MHE. MOHAMMED MAULID ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilitaka kumwuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango gani wa Serikali katika bajeti ijayo kuhusu suala zima la kutoa maji kwenye maziwa na kupeleka kwa wananchi? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Maulid Ali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Wizara, nimesema katika jibu langu la msingi, ni kuona kwamba tunakwenda kutumia vyanzo vya uhakika, ikiwemo maji ya maziwa makuu. Hivyo tuko kwenye mpango huo, lazima tutatekeleza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa muda wetu umekwisha, na ninajua watu wengi wanataka kuuliza masuala ya maji. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula.

Na. 147

Kuwawezesha Wakulima wa Mazao ya Viungo Mkinga

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima wa mazao ya viungo kama Iliki, mdalasini, pilipili manga na karafuu wa Kata ya Kigongoi, Mhindano na Boshu Wilayani Mkinga ili waweze kuongeza uzalishaji wa thamani ya mazao hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya viungo yanayojumuisha Karafuu, Pilipilimanga, Pilipili Kali, Mdalasini, Hiliki, Tangawizi na jamii hiyo ya mazao ya viungo, hulimwa zaidi katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Mbeya, Kilimanjaro, Kigoma na Ruvuma. Aidha, katika Mkoa wa Tanga Wilaya ya Mkinga na katika Kijiji cha Kigongoi na vijiji vidogo jirani yake ndiyo wanazalisha mazao ya viungo zaidi ikiwemo Hiliki, Mdalasini na Pilipilimanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuendeleza mazao ya bustani yakiwemo mazao ya viungo, inatekeleza Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani wa Mwaka 2021 - 2031 wenye lengo la kuongeza uzalishaji kwa kutumia teknolojia bora na kuimarisha usimamizi na uratibu. Aidha, mikakati mingine ni pamoja na kutoa mafunzo ya wataalam na wakulima kuhusu kanuni za uzalishaji wa mazao ya viungo, kuunganisha wakulima na wanunuzi wakubwa, na kuanzisha vitalu vya kisasa vya miche ya viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na chama cha wasindikaji wa viungo (*TASPA*) na wasindikaji wa mazao ya viungo wameanza kuwashirikisha wakulima wa viungo Wilaya ya Mkinga kwa kuanzisha vitalu vya kisasa vya viungo. Mfano, Kampuni ya *Trianon Investment Ltd* yenye Kiwanda cha Viungo Lusanga – Muheza tayari imeanza kununua mazao kwa wakulima wa viungo Mkinga na imedhamiria kugawa miche bora kutoka katika bustani bora ya kuzalisha miche iliopo kiwandani.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeanza kuhamasisha wakulima kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Msingi vya Ushirika ili kukuza uwezo wao wa kifedha kupitia mikopo na kuwa na nguvu ya pamoja katika soko; na pia Serikali kuweza kuwapatia mafunzo ya uzalishaji bora na uongezaji thamani wa mazao yao. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kitandula.

MHE. DUSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tija ya kilimo katika mazao haya ipo chini sana kwa sababu ya mbegu duni: Nini kauli ya Serikali katika kuwasaidia wakulima hawa kupata mbegu bora ili kuweza kuongeza tija katika kilimo chao?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Pili, Serikali iko tayari kushirikiana na Mkoa wa Tanga katika kuboresha mnyororo wa thamani wa kilimo cha mazao haya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kitandula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri, kama nchi kwa muda mrefu tulikuwa hatujayapa kipaumbele mazao haya ya viungo. Nataka tu nilihakikishie Bunge lako tukufu, kwamba kwanza tumeya-*cluster* kama sehemu ya mazao ya *horticulture*, kwa hiyo, yatasimamiwa kwa karibu na idara inayohusika na mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumekiagiza kituo chetu cha Mlionsano kwamba kianze kufanya kazi ya utafiti na uzalishaji wa mbegu na miche kwa ajili ya mazao ya Hiliki na mazao ya viungo pamoja na mazao ya matunda ya machungwa ambayo yanalimwa kwa wingi katika Mkoa wa Tanga ili kuondoa matatizo yanayowakabili wakulima wetu na kuyapa *center stage* mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kushirikiana na mkoa, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko tayari kama Wizara ya Kilimo kukaa nao ili tujadiliane ni namna gani tunaweza kuwasaidia wakulima hawa wadogo kwenye *value chain* ya mazao kama ambavyo tumeamua kuwasaidia wakulima wa mkonge kwa kuwapatia makorona; na Bodi ya Mkonge itanunua makorona matatu kwa ajili ya kuwapa wakulima wadogo wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Wizara tuko tayari kukaa nao. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi.

Na. 148

Hitaji la Chuo cha VETA – Malinyi

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Malinyi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Jimbo la Malinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa vyuo vya mafunzo na ufundi stadi katika Mikoa na Wilaya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa Serikali inakamilisha ujenzi wa Vyuo vya VETA katika Wilaya 25 na Mikoa minne nchini kwa lengo la kuwapatia vijana ujuzi katika fani mbalimbali utakaowawezesha kuajiriwa au kujijiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi ambacho Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Malinyi na maeneo mengine, wananchi wa Malinyi wanashauriwa kutumia Vyuo vya VETA vilivyopo katika Mkoa wa Morogoro ambavyo ni Mikumi, Dakawa, Kihonda, Ulanga pamoja na vyuo vingine vya VETA vilivyopo nchini kwa ajili ya kupata elimu na mafunzo ya ufundi. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Antipas.

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi ambao wanamaliza kKidato cha nne Wilaya ya Malinyi ambao hawaendelei na masomo ya Kidato cha Tano wako zaidi ya 600 kila mwaka; na wengi wao kimbilio lao lilikuwa ni kilimo; na sasa kutokana na mgogoro kati ya Wizara ya Maliasili (*TAWA* na wananchi wa Malinyi) kuna uwezekano mkubwa tukapoteza maeneo ya kulima. Wanafunzi hao wanahitaji ujuzi wa ziada kwa ajili ya kujikwamua nje ya kilimo:-

Je, Serikali haioni haja ya kuiingiza Malinyi katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA?* (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, anayoyazungumza Mheshimiwa Mbunge ni kweli, uhitaji wa vyuo hivi ni mkubwa sana sio tu kwa Malinyi. Kama nilivyozungumza kwenye jibu langu la msingi kwamba tunamalizi ujenzi wa vyuo hivi 25 katika wilaya 25 pamoja na mkoa minne nimuondowe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge katika bajeti ijayo iwapo Serikali tutapata fedha kipaumbele cha kwanza itakuwa ni eneo hili la Malinyi na maeneo mengine ambayo yenye uhitaji mkubwa ukilinganisha na maeneo mengine tayari yanavyuo karibu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa niwaombe radhi wale ambao hawajapata nafasi muda umekuwa kidogo.

Sasa maswali yamekwisha tuko kwenye wageni na matangazo mengine, wageni waliopo Bungeni mchana huu,

Wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni wawili wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambao ni familia yake kutoka Ukonga, Jijini Dar es salaam, Ndugu Miriam Bakari Makulo - mke wake na Ndugu Simba William Jerry Silaa, mtoto wake, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Jerry Silaa ni viongozi kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina Dodoma ambao ni Ndugu Mgonja Benedicto, Msajili wa Hazina, Ndugu Lightness Mauki - Mkurugenzi wa uwekezaji – Hazina, Ndugu Linus Kakwesiga - Msaidizi wa Msajili wa Hazina.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 3 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar Es Salaam Ndugu Tousif Bhojani, Ndugu Ali Abdullah na Ndugu Bobby Singh Sheinh, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Daktari Angelina Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ndugu Immaculate Mwalu muumini wa Parokia ya Anthony wa Padua Yasaka ya Jijini Mwanza.

Wageni watoto wa Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao ni wawekezaji kutoka South Africa, Belgium na Switzerland. Ndugu Andrew *Whiting -Vice President Corporate Affairs*, (South Africa), Ndugu Andrew Correa-Director Digital Innovation (Belgium) Ndugu Eric Jones -*Vice President Tax Stamps Innovation*, Wameambatana na wenyeji wao ambao ni Ndugu Mesiya Mwangoka - Mkurugenzi wa *TBL Tanzania*, Ndugu John Wanyancha - Mkurugenzi wa *Serengeti Breweries*, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza (Mbunge) ambaye ni Mpiga kura wake kutoka Jijini Mwanza, Ndugu Christopher Kilaja, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga kutoka Wilayani Mbozi Mkoani Songwe ambao ni Ndugu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Simoni Mboya – Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbozi, Ndugu Julius Mbwiga - Katibu wa CCM Wilaya ya Mbozi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Morogoro wakiongozwa na dada yake Ndugu Angelina Mgungusi, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Tadayo (Mbunge), ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga Mkoani Kilimanjaro Ndugu Salehe Mkwizu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Sillo (Mbunge), ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Babati Ndugu George Sanga na Ndugu Charles Mangwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaye ni Mtaalamu wa *IT* Kampuni ya *Kili Net* kutoka Klabu ya Yanga ya Jijini Dar es Salaam Ndugu Benard Manyama, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 47 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni Viongozi wa Bunge na Serikali wakiongozwa na Spika wa Bunge la Chuo hicho Ndugu Edward Lukumay, karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo la kwanza naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote, Ofisi imeandaa tafrija kwa Wabunge na watumishi kesho siku ya Alhamisi tarehe 17 Februari, 2022 mara baada ya kuahirisha Bunge kwa ajili ya kuwapongeza wanamichezo wetu wa *Bunge Sport Club* kwa ushindi walioupata kwenye mashindano ya michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 4 mpaka 17 Disemba, 2021 Jijini Arusha.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Aidha, inatarajiwa makombe tuliyoyapata yatatolewa rasmi wakati wa tafrija kwenye eneo letu maarufu Jirani na zahanat ya Bunge. Wabunge wote na watumishi wanaombwa kuhudhuria bila kukosa kwenye tukio letu hili muhimu kwa Bunge letu. Vilevile Wabunge mnaombwa msi-*park* magari katika eneo hilo.

Kampuni ya *Precision Air* imeanzisha huduma ya usafiri kutoka Dar es Salaam kupitia Dodoma hadi Tabora kwa siku za Jumatatu na Jumatano kwa bei nafuu ya shilingi 260,500 njia moja na shilingi 310,500 kwenda na kurudi.

Aidha kwa siku hizo hizo Dodoma hadi Tabora na Tabora Dodoma kwa bei ya shilingi laki moja thelathini na moja njia moja na shilingi laki mbili hamsini na tano kwenda na kurudi.

Mheshimiwa Seif Gulamali, Mwenyekiti wa Tawi la Klabu ya *Dar Young African* anawaomba... (*Makofi*)

Waheshimiwa order *please* anawaomba Wabunge wote wajisajili leo na kesho kutwa kadi zitapatikana kwa Wabunge wote watakaojisajili. Lakini haisemi wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa kwa utaratibu wa siku za nyuma ilikuwa ni chakonichako sasa nafikiri Waheshimiwa baadaye muwasiliane na Mwenyekiti atawapa taarifa ni wapi mtafanya usajili huu.

Katibu!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO- KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021 na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021

NAIBU SPIKA: Hoja za Kamati, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti.

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu Utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti katika kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022. Taarifa hii pia inatoa Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Mwezi Julai hadi Desemba 2021 na mwelekeo hadi Mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Taarifa Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano (5) zifuatazo: - Sehemu ya Kwanza inatoa Maelezo ya Jumla kuhusu Majukumu ya Kamati na shughuli zinazotekelezwa; Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa Majukumu ya Kamati; Sehemu ya Tatu inatoa Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Mwezi Julai hadi Desemba 2021 na mwelekeo hadi Mwezi Juni, 2022; Sehemu ya Nne inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na Sehemu ya Tano ni Hitimisho la Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu ya Kamati Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Nyongeza ya Nane, Fasili ya 9 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ina majukumu kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 97(2) na 136(3)(5)(8), and (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 kuhusu kukutana, ushirikishwaji wa Wadau kwenye shughuli za Kamati na uzingatiaji wa Bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 na 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia na mbinu zilizotumika ni kama inavyoonekana kwenye taarifa za kamati: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shughuli za Kamati zilizotekelezwa katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imetekeleza shughuli mbalimbali na baadhi yake ni kama zifuatazo: Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/21;

(i) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2020/2021;

(ii) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

(iii) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;

(iv) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

(v) pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(vi) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti za Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

(vii) pamoja na kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Mifuko hiyo Mwaka wa fedha 2021/2022;

(viii) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021 (*The Finance Act, 2021*), Muswada wa Mabadiliko ya Sheria mbalimbali Na 6 pamoja na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka 2022;

(ix) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023;

(x) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti. Tafiti zilizofanyika ni Utafiti kuhusu Faida na Hasara ya Michezo ya Kubahatisha Nchini pamoja na Utafiti kuhusu Uhimilivu wa Sera za Kibajeti Tanzania;

(xi) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2021/2022 kwa ajili ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi tajwa, Kamati za Kisekta zilizowasilisha Hoja mahsusi zilikuwa zifuatazo:- Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Viwanda Biashara na Mazingira, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Maliasili na Utalii, Katiba na Sheria na Utawala na Serikali za Mitaa;

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa shukrani kwanza kwako wewe Binafsi na Pili kwa Serikali na wadau wote kwa ushirikiano wao uliowezesha kukamilika kwa shughuli hizi za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Matokeo ya

Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati Maelezo Jumla baada ya kuelezea majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelewa kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati wa ikitekeleza majukumu yake. Masuala yanayotolewa taarifa ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 inakwenda sambamba na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla. Kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimetathminiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pato la Taifa Katika kipindi cha mwaka 2020, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7 mwaka 2019. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchukuzi na uchimbaji madini. Kiasi hiki ni kikubwa zaidi ya kile kilichokuwa kimekadiriwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) cha asilimia 2.5 ikiwa chini ya lengo la nchi la kukua kwa asilimia 5.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kupungua kwa kasi ya ukuaji katika kipindi husika kulichangiwa na mvua zilizozidi wastani zilizosababisha mafuriko ambayo yaliharibu miundombinu ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo nchini na kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Uviko 19) ulioenea katika nchi nyingi ambazo ni washirika wetu wakubwa kibiashara. Vilevile, homa hiyo ya mapafu ilisababisha kushuka kwa sekta ya utalii ambayo inachangia kiasi kikubwa cha mapato ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Serikali hadi Desemba, 2020, Deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 59.01, sawa na ongezeko la asilimia 7.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni

54.85 kipindi kama hicho mwaka 2019. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 42.83 na deni la ndani ni shilingi trilioni 16.18. Ongezeko la deni limetokana na Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na malimbikizo ya riba ya deni la nje, hususan kwa nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris (*Non-Paris Club members*) ambazo Serikali inaendelea kujadiliana nazo. Aidha, kwa viwango vyote vya kimataifa Deni letu ni himilivu na linalipika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2020/2021 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022 kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (5) (a) Bunge lilijadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/2022 – 2025/2026 wenye Dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu ulikuwa na maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Baadhi ya masuala yaliyobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Barabara ya miaka mingi kutokutekelezwa kikamilifu Kamati ilifanya uchambuzi wa barabara 38 zenye jumla ya Kilomita 8,575.29 zilizopo kwenye hatua mbalimbali na kubaini mambo yafuatayo: Kwanza, kuna barabara ambazo zina miaka zaidi ya 10 katika hatua ya upembuzi yakinifu na uchambuzi wa kina na hazijaanza kujengwa. Pili, kuna baadhi ya barabara zimejengwa kilomita chache na ujenzi haujaendelea kwa miaka mingi. Aidha, Barabara mpya zinaendelea kuibuliwa

ilihali barabara za zamani hazijakamilika na kuna ongezeko la malipo ya riba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wa Bunge Taarifa ya Bajeti ndiyo taarifa ya maswali yenu yote Wabunge na Mheshimiwa Mwenyekiti anazungumzia barabara ambazo kwa muda Zaidi ya miaka kumi bado hazijatekelezwa ninyi msikilizi yeye mnaanza kumsikiliza mambo ya vilabu na vitu vingine. Kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge sikilizeni taarifa ya bajeti ambayo ndiyo solution ya majibu yenu. Mheshimiwa endelea Samahani sana.

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie Kamati ilifanya uchambuzi wa barabara 38 zenye jumla ya Kilomita 8,575.29 zilizopo kwenye hatua mbalimbali na kubaini mambo yafuatayo: Kwanza, kuna barabara ambazo zina miaka zaidi ya 10 katika hatua ya upembuzi yakinifu na uchambuzi wa kina na hazijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna baadhi ya barabara zimejengwa kilomita chache na ujenzi haujaendelea kwa miaka mingi. Aidha, Barabara mpya zinaendelea kuibuliwa ilihali barabara za zamani hazijakamilika na kuna ongezeko la malipo ya riba kwa Serikali linalotokana na kutolipa wakandarasi kwa wakati kwa kigezo cha uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha ujenzi wa barabara zilizoainishwa kwenye Mpango na kuharakisha malipo ya wakandarasi pindi hati za malipo (*certificates*) zinapowasilishwa. Pia, endapo itabidi Serikali ifanye uhakiki usizidi siku 20 za kazi. Hatua hizi zitasaidia kupunguza hasara inayotokana na riba na kuleta maendeleo yaliyokusudiwa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishwaji hafifu wa Sekta Binafsi katika kutekeleza Mpango pamoja na kwamba Sekta

binafsi ni injini ya kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, ushirikishwaji wake katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo si wa kuridhisha. Sekta binafsi nchini bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:- Wingi wa Mamlaka za uhibititi zinazosimamia shughuli za sekta binafsi; Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi; Wingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja; na Ukiritimba katika kupata vibali vya kazi na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tangu kuanzishwa kwa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini "*Blue Print*" ni miaka mitano sasa. Hata, hivyo hadi hivi sasa hakuna Taarifa ya Serikali inayoonyesha katika kipindi cha miaka mitano imetetekezwa kwa asilimia ngapi. Kamati inaishauri Serikali katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2022/2023 na miaka inayokuja uwekwe utaratibu kwa kila sekta kuainisha hatua zilizochukuliwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kwa sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile imefika wakati sasa kufanya marejeo ya kina ili kuangalia ufanisi wa mpango huo. Kamati inaamini kwamba utekelezaji wa *Blueprint* ni mwarobaini wa kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Vipaumbele uchambuzi wa Kamati kuhusu maeneo ya Vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 ulibaini masuala yafuatayo:- Wingi wa Vipaumbele na hivyo kufanya mgawanyo wa rasilimali kuwa mgumu na kukamilisha vipaumbele vichache tu; na baadhi ya maeneo ya vipaumbele yamekuwepo tangu mpango wa kwanza wa maendeleo na havitekelezwi mfano ujenzi wa mabwawa ya Kidunda na Farkwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*) kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati iliwasilisha Bungeni taarifa yake ya maoni

na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021. Shughuli hii ilifanyika kwa kupitia kifungu kwa kifungu pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kupendekeza marekebisho pale ilipobidi. Sheria zilizowasilishwa na kufanyiwa kazi katika Muswada huo ni Sheria Kumi na saba (17) kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 kwa kipindi cha nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2022/2023 mwezi umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 mapendekezo ya Mpango yanaonyesha kwamba katika mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi tirioni 39.4 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 7.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/2022 na tirioni 36.68.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya ndani ukijumlisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za mitaa yanatarajiwa kuongezeka hayo kufika tirioni 28.567 ikiwa ni sawa asilimia 72.5 ya bajeti kati ya fedha hiyo mapato ya shilingi Trilioni 24.24, mapato yasiyo ya kodi shilingi Trilioni 3.39 na mapato ya halmashauri shilingi bilioni 937.05. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha shilingi Trilioni 7.444 zikiwa ni

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapitio hayo, Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mapendekezo ya Mpango huo. Maeneo mahsusi yafuatayo:- Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti sura ya 439 kinataka Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura *Contingency Fund*. Pamoja na uwepo wa takwa hilo la kisheria, bado Serikali haijaanzisha Mfuko huo badala yake imekuwa ikitenga fedha za dharura kupitia Fungu 21 – Hazina.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, uwepo wa Mfuko huu ungeisaidia sana Serikali yanapotokea majanga kama vile lilivyo Gonjwa la UVIKO-19. Kamati inaitaka Serikali katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kuanzisha Mfuko huu ili utusaidie tunapopatwa na majanga na kuondokana na utaratibu wa kuweka fedha za dharura katika Fungu 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa njia ya ubia (*PPP*); ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi. Miradi ya *PPP* iliyobainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/2023 ni ile ile ambayo imekuwa ikiainishwa kila mwaka na hakuna utekelezaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja mahsusi za Kamati za Bunge za Kisekta; katika Bunge la Bajeti la mwaka 2021, Kamati ilipokea jumla ya hoja mahsusi 12 zilizowasilishwa mbele yake kutoka kwa Kamati za Bunge za Kisekta. Kati ya hoja hizo, hoja sita zilihusu bakaa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mafungu mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; Hoja tano zilihusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na hoja moja ilihusu mapendekezo kuhusu sera, sheria na

mabadiliko ya kikodi na hivyo hazikuwa na athari ya kibajeti moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti ilikamilisha jukumu hili kwa kukutana na Kamati ya Uongozi pamoja na Serikali kwa lengo la kufanya mashauriano kuhusu hoja husika. Katika kikao hicho, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilishwa katika Kamati ya uongozi na baadaye Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizofanyiwa kazi na Serikali; baada ya majadiliano baina ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali hoja zilizofanyiwa kazi na Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi; kuhusu ujenzi wa majengo ya Ubalozi ambayo imekua hoja ya muda mrefu, Serikali ilishaanza kazi za awali katika ujenzi wa jengo la Ubalozi wa Tanzania nchini Oman. Aidha, Serikali iliahidi kuwa ujenzi wa majengo mengine ya Ubalozi kwa nchi mbalimbali utaendelea kutengewa fedha kwa miaka ijayo. Kamati inaendelea kusisitiza ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuanza ujenzi wa Ofisi za Balozi kwa kutumia mifumo mingine ya fedha kama *mortgage financing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *EPZ Development Kurasini*; kuhusu Mradi wa *EPZ Development Kurasini Logistic Centre* ambao licha ya Serikali kulipa fidia ya jumla ya Shilingi Biloni 101, lakini takribani miaka saba sasa mradi haujaanza kutekelezwa. Serikali ilikubali kutoa fedha za fidia shilingi milioni 556.79 kwa wananchi watatu waliobaki kwenye fedha za matumizi mengineyo ya mwezi Aprili, 2021. Fedha hizo zilitolewa mwezi Aprili na wananchi hao walilipwa na kubomoa makazi yao ili kupisha eneo la mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika hoja ambazo Serikali iliahidi kuzifanyia kazi; hoja nyingine ambazo zilihusu masuala ya sera na kisheria Serikali iliomba muda ili iweze kuzishughulikia zaidi.

Hoja hizo zilihusu utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mamlaka za *TAWA*, *TANAPA* na *NCA* pamoja na namna ambavyo matumizi yao yanaidhinishwa hasa ukizingatia mamlaka hizi zina Bodi zake pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina kama waangalizi wakuu. Ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali imeendelea kuzifanyia kazi hoja hizo kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara za Kamati za kutembelea taasisi, idara na mamlaka mbalimbali; katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022, kwa nyakati tofauti, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Malengo ya ziara hizo ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala muhimu yaliyojitokeza; kwa muhtasari naomba niwasilishe masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa ziara za Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*); Kamati ilipotembelea Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*) ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Mtaji mdogo hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

(ii) Utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya madawa aina ya *Polyvinyl chloride* pamoja na vipuri vya mashine pamoja na ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kwa Kiwanda cha *Keko Pharmaceutical*;

(iii) Utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na ile ya Maendeleo ya Reli kwenye mashine na vitendanishi vinavyotumika kutoa huduma za uchujaji damu na hivyo kuongeza gharama za huduma hizo nchini;

(iv) Mlolongo wa utaratibu wa ununuzi wa dawa unaosababishwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma na hivyo kuchelewesha ununuzi wa dawa; na

(v) Kiwanda cha *Keko Pharmaceutical Industry* kukabiliwa na deni la shilingi blioni 12 ambalo lilikopwa na mbia wa kiwanda hicho toka taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauri Serikali kwanza kuanzisha utaratibu wa utoaji wa fedha za dawa kwa miezi miwili kila mwanzo wa mwaka na Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR*) kushughulikia deni la Kiwanda cha Dawa cha Keko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutembelea Mpaka wa Tanzania na Kenya – Namanga; Kamati ilitembelea Mpaka wa Tanzania na Kenya – Namanga ili kuangalia jinsi Kituo cha Pamoja cha Forodha (*One stop Boarder Post*) kinavyofanya kazi. Katika ziara hiyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea upande wa Kenya na kujionea namna Kituo cha Kenya cha Forodha kinavyofanya kazi na hivyo kuweza kufanya ulinganishi sahihi na upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kwamba Kituo cha Pamoja cha Forodha kinavyofanya kazi kwa upande wa Tanzania kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa *Cargo Scanner* kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo;

(ii) Upungufu wa nyumba za makazi ya Maafisa wa Forodha na Uhamiaji;

(iii) Biashara ya magendo katika mpaka huo; na

(iv) Uhaba wa watumishi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizi hasa ya *cargo scanner* imesababisha ucheleweshaji wa uondoshaji wa mizigo katika mpaka huo kwa upande wa Tanzania na hivyo kuwa na msururu mrefu wa magari na gharama kubwa kwa wasafirishaji. Aidha, Kamati ilibaini mipaka yote rasmi nchini isipokuwa Bandarini na Uwanja wa Ndege wa Dar es

Salaam hakuna mashine za kukagulia mizigo mikubwa (*cargo scanner*). Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba inanunua na kusimika *cargo scanners* katika mipaka yote ya Tanzania ili kupunguza msongamano mipakani inayotokana wa ukaguzi kwa kutumia macho yaani *physical verification* ili kuondoa mianya ya rushwa na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa Kamati; katika kipindi husika, Kamati ilipata fursa ya kupata mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uwezo na ujuzi kwa Wajumbe wa Kamati. Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) pamoja na Programu za Miradi ya *LSP II* na *PFMRP* ziliratibu mafunzo hayo. Mafunzo hayo yaliwasaidia Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kusimamia Bajeti ya Serikali na hatimaye kuweza kushauri Serikali ipasavyo. Mafunzo ambayo Kamati ilishiriki ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati; katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali, Kamati ilifanikiwa katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuongeza mapato ya Serikali kupitia mabadiliko ya sheria mbalimbali. Katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021, Serikali ilileta mapendekezo huhusu kuanzisha tozo itakayotozwa kwenye miamala ya simu. Aidha, Serikali pia ilianzisha kutoza Kodi ya Ushindi kutoka kwenye mapato ghafi kwenye *virtual games*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ilifanya maboresho katika Sheria ya Ushuru wa Mafuta ili kuongeza shilingi 100 kwa ajili ya maji na barabara vijijini. Vyanzo vyote hivi vinatokana na ushauri wa Kamati kwa Serikali na baada ya kukubalika vimeongezea mapato ya Serikali ya takribani shilingi billioni 600 ambazo zimeelekezwa kwenye

miundombinu ya barabara, afya na elimu na matokeo yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za mkopo toka *IMF*; utakumbuka kwamba, baada Serikali kupokea mkopo wa shilingi trilioni 1.31. kwa ajili ya kugharamia mpango wa kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii kutokana na UVIKO-19, Kamati ya Bajeti ilikutana na Serikali tarehe 6 na 7 Oktoba, 2021 ili kujadiliana kuhusu mgao huo. Mafanikio ya majadiliano hayo yalikuwa kama ifuatavyo: -

(i) Serikali ilikubali kupunguza shilingi bilioni 40 kutoka kwenye fedha za miradi ya maji iliyopo mijini na kuongeza bajeti ya miradi ya maji iliyopo vijijini hadi kufikia shilingi bilioni 55.5;

(ii) Serikali ilikubali kufanya *reallocation* ya fedha zisizopungua shilingi bilioni 66 kwenye fedha zilizotengwa kwa shughuli mbalimbali za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya madarasa ya shule shikizi; na

(iii) Kupunguza ununuzi wa *advanced ambulances* 20 na kuongeza ununuzi wa *ambulance* za kawaida zaidi ya 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati; katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, changamoto ya kanuni ya uwasilishaji wa Taarifa za Kamati ya Bajeti; kwa mujibu wa Kanuni ya 69(C), Mwenyekiti anayewasilisha Taarifa ya Kamati anatakiwa kuiwasilisha kwa muda usiozidi dakika 30. Changamoto kubwa inayoikumba Kamati ya Bajeti ni Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali huwasilishwa kwa zaidi ya saa mbili Mpango wa Maendeleo ya Mwaka huwasilishwa pia kwa zaidi ya saa mbili, lakini Kamati ya Bajeti ambayo inachambua nyaraka zote hizo mbili inatakiwa kutoa

mapendekezo yake kwa dakika 30 tu. Hivyo, Kamati inashauri wakati wa kuwasilisha Taarifa yake inayohusu Bajeti Kuu ya Serikali na Mpango wa Maendeleo itengewe muda wa saa moja ili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kuelezewa ipasavyo uchambuzi uliofanywa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali pamoja na Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka husika; moja ya maeneo ambayo huwa yanachukua sura kubwa ya Hotuba ya Bajeti kila mwaka ni mabadiliko ya sheria mbalimbali za kodi. Hivyo, kiutaratibu ilitakiwa pindi Waziri wa Fedha na Mipango anaposoma hotuba yake, iambatane na Muswada wa Sheria ya Fedha kwa Mwaka husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, imekuwa haifanyiki hivyo na badala yake Muswada huletwa baadaye na hivyo kuipa Kamati muda finyu wa kuwaita wadau na kupata maoni yao. Hivyo, inashauriwa kwamba Waziri wa Fedha anapowasilisha Hotuba ya Bajeti iende sambamba na Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka kuanzia mwezi Julai hadi Desemba, 2021 na mwelekeo hadi mwezi Juni, 2022; sura ya bajeti na utekelezaji hadi Disemba 2021; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 36,681.9. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi bilioni 23,003.0 zilitarajiwa kutumika kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 13,678.9 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021, Serikali imetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya shilingi bilioni 16,505.2. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 11.143 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni 5.361 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa ujumla utekelezaji wa bajeti ni asilimia 49.5. Hivyo kwa kuwa ni utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaweza kufikia asilimia 85 hadi 90. Jambo hili si la kubeza

na inatakiwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake na mafanikio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mwenendo wa makusanyo ya mapato; katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021, Serikali iliweza kukusanya jumla ya shilingi trilioni 18,199.6, sawa na asilimia 49.6 ya makadirio ya kukusanya na kutumia shilingi trilioni 36.6. Hatua hii ni ya kupongeza kwa sababu inaonesha kwamba makusanyo ya mapato yanatarajiwa kufikia walau asilimia 80 hadi 90 ya matarajio na Jedwali Na.1 linaonesha mwenendo wa makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mwenendo wa matumizi; katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021 Serikali imetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya shilingi trilioni 16.199, sawa na asilimia 45.9 ya bajeti yote ya mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 11.14 zilitumika kwa matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 5.361 zilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 kwa kipindi cha nusu mwaka 2021/2022; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria 17 kupitia Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko hayo yalifanyika kwa malengo ya kutekeleza *blue print* ya uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini, uboreshaji wa mfumo wa kodi, kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kutoa msamaha kwa maeneo muhimu ili kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 maboresho hayo yalikuwa yamekusanya jumla ya shilingi bilioni 443.46 sawa na asilimia 28.35 ya kukusanya shilingi trilioni 1.563.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofikiwa kwa lengo kumetokana na sababu mbalimbali za msingi kama zifuatazo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(i) Uwepo wa biashara ya magendo katika mipaka yote ya Tanzania ya nchi kavu na mipaka ya majini;

(ii) Matumizi yasiyoridhisha ya mashine za *EFD*, na;

(iii) Kukosekana kwa elimu ya mlipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za mkopo kutoka *IMF*, shilingi trilioni 1.3; utakumbuka kwamba uliridhia Kamati ya Bunge ya Bajeti ikutane na Serikali mwezi Oktoba, 2021 kwa ajili ya kujadili mpango na mgawanyo wa fedha za mkopo kutoka *IMF* zenye jumla ya shilingi trilioni 1.31.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao hicho kilihusisha Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mgawanyo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasoma muhtasari wa taarifa nzima kwa hiyo naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye kumbukumbu zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo wa *IMF* umetoa mafunzo mengi kwa Serikali, kama ifuatavyo: -

(i) Fedha za maendeleo zikifuatiliwa kwa makini kama zinavyofuatiliwa fedha hizi za mkopo matokeo chanya yanaonekana;

(ii) Endapo kungekuwa na usimamizi thabiti kwenye fedha za maendeleo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kusingekuwa na ubadhirifu katika utekelezaji wa miradi ya Serikali;

(iii) Inawezekana kabisa kwa Serikali kulihusisha Bunge kwenye mgawanyo na matumizi ya mikopo ambayo Serikali inachukua ili kuleta uwazi na uwajibikaji; na

(iv) Lazima sasa Serikali iwe na maeneo ya vipaumbele kama ilivyofanya kwenye mkopo huu kwa kuchagua maeneo machache na kuyamaliza kabisa na sio kila mwaka kutenga fedha kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kama mafundisho haya yakitumika vizuri, Taifa litapata maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sillo, twende kwenye maoni, umebakisha dakika tatu tu.

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwa kuwa marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya *EPOCA* mwaka 2017, yalielekeza kampuni zote za simu kujiorodhesha kwenye soko la hisa na kuuza asilimia ishirini na tano ya hisa zake kwa umma na hatimaye kampuni hizo kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam;

Na kwa kuwa Kamati ilibaini kuwa kati ya kampuni zote za simu ni kampuni ya *Vodacom* tu ambayo imeweza kuingia kwenye soko, lakini siyo hisa zote zimeweza kununuliwa na bado gawio ni dogo lakini na kushuka kwa thamani ya hisa zake;

Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba kampuni za simu ambazo bado hazijaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ziorodheshwe ili Watanzania waweze kushiriki katika uwekezaji kwenye sekta ya mawasiliano kama sheria inavyoelekeza.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira na ufanyaji wa biashara nchini (*blueprint*);

Kwa kuwa kwa mujibu wa Taarifa ya Urahisi wa Ufanyaji Biashara na Uwekezaji inayoandaliwa *UNCTAD*, Tanzania inashika nafasi ya 141 mwaka 2020;

Na kwa kuwa utekelezaji wa *blueprint* ulitarajiwa kuwa mwarobaini wa tatizo la mazingira yasiyoridhisha ya biashara nchini, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua;

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu *blueprint* ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuweka vipaumbele vichache kwenye mpango;

Kwa kuwa kila mwaka Serikali inatoa vipaumbele vyake katika mpango wa mwaka ambavyo kwa uchambuzi wa Kamati vimeonekana kuwa vingi kutekelezwa kwa mwaka mmoja;

Na kwa kuwa wingi wa vipaumbele umekuwa unasababisha kutekelezwa nusu nusu au kutovitekeleza kabisa;

Hivyo basi Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwa na vipaumbele vichache walau kila sekta na kuvikamilisha kwa zaidi ya asilimia 90, hasa vile vinavyoweza kukamilika katika mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji:-

Kwa kuwa kumekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Bunge kuomba Serikali kuandaa sheria itakayosimamia masuala yote ya tathmini na ufuatiliaji bila kuwa na mafanikio;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba katika nusu ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 lazima Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji na endapo haitafanya hivyo, Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Bunge ya Bajeti litaandaa Muswada wa Sheria na kuuwasilisha Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa ili kuwe na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhuisha Mfuko wa Jimbo uendane na hali ya uchumi wa sasa:-

Kwa kuwa viwango vinavyotumika kutoa fedha kwa Mfuko wa Jimbo vilipangwa miaka karibia 20 iliyopita na havijawahi kurejewa mpaka hivi sasa;

Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba Serikali ifanye marejeo ya viwango vya fedha vya Mfuko wa Jimbo ili viendane na hali ya sasa ya uchumi. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la *Tanzanite*, Dar es Salaam:-

Kwa kuwa Daraja la *Tanzanite*, Dar es Salaam, lenye urefu Km 1.03 na barabara unganishi kilomita 5.2. lililojengwa kwa gharama ya Dola za Marekani million 107.4 sawa na shilingi bilioni 243.8;

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali kuangalia uwezekano wa daraja hilo kuwa la kulipia yaani *toll bridge* ili lisaidie kurejesha fedha za mkopo zilizotumiwa kujenga daraja hilo kama ambavyo inafanyika kwa Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya fedha za dharura kwa ajili ya ukarabati wa barabara vijijini zilizoharibika kwa mvua zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini:-

Kwa kuwa Wakala wa Barabara Vijijini *TARURA* umekamilisha tathmini ya mahitaji ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya urejeshaji wa mawasiliano ya barabara vijijini;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Na kwa kuwa kiasi kinachohitajika ni shilingi bilioni 111.375;

Hivyo basi Bunge linaishauri Serikali kutenga katika Bajeti ya mwezi wa Februari angalau bilioni 60 na mwezi Machi billioni 50 ili kunusuru barabara vijijini ili wananchi wetu wapate barabara zinazoweza kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba nihitimishe kwa kukushukuru kwanza wewe binafsi, lakini pia Mheshimiwa Spika kwa kuendesha Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nimpongeze Mheshimiwa wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, pamoja na aliyekuwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa *Eng.* Hamad Yussuf Masauni, pamoja na Naibu Waziri wa sasa, Mheshimiwa Hassan Chande, kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini, umahiri na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao pamoja na ushauri ambao umesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inasimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao na majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelewa Mwihambi *(ndc)*, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati; Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Ndugu Emmanuel Rhobi, Ndugu Maombi Kakozi na Ndugu Wilfred Akasi, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliyowezesha kufanikisha kazi za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa idara na vitengo katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati zinafanyika kama zilivyokuwa zimepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2021 HADI MWEZI JANUARI, 2022 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA, JULAI - DESEMBA 2021 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu Utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti katika kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022. Taarifa hii pia inatoa Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Mwezi Julai hadi Desemba 2021 na mwelekeo hadi Mwezi Juni, 2022.

1.1. Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano (5) zifuatazo: -

- i. Sehemu ya Kwanza inatoa Maelezo ya Jumla kuhusu Majukumu ya Kamati na shughuli zinazotekelezwa;
- ii. Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;
- iii. Sehemu ya Tatu inatoa Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Mwezi Julai hadi Desemba 2021 na mwelekeo hadi Mwezi Juni, 2022;
- iv. Sehemu ya Nne inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- v. Sehemu ya Tano ni Hitimisho la Taarifa.

1.2. *Majukumu ya Kamati*

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Nyongeza ya Nane, Fasili ya 9, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ina majukumu yafuatayo: -

- i. Kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi inazozisimamia;
- ii. Kuchambua na kutoa mapendekezo kuhusu Mpango wa tatu wa Maendeleo ya Taifa wa miaka 5;
- iii. Kujadili na kufanya mapitio kuhusu Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kila mwaka na kutoa maoni na mapendekezo Bungeni;
- iv. Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya kila mwaka yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;
- v. Kutoa ushauri wa jumla kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za kudumu za Bunge;
- vi. Kuchambua makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa, Mahakama na Bunge;

vii. Kupitia Bajeti ya Serikali na kutoa mapendekezo ya jumla kwa Bunge kuhusu masuala ya bajeti;

viii. Kufuatilia masuala yote ya bajeti yaliyo chini ya mamlaka ya Bunge chini ya Sheria ya Bajeti au Sheria nyingine na kutoa taarifa kwa Bunge;

ix. Kufuatilia utekelezaji wa Serikali na Taasisi za Umma ili kuhakikisha zinazingatia misingi ya matumizi ya fedha za umma, kama ilivyobainishwa kwenye Sheria hii na Sheria ya Fedha za Umma;

x. Kuchambua na kushauri kuhusu Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni yenye madhumuni ya kuongeza au kupunguza mapato na Bajeti ya Serikali;

xi. Kupitia taarifa za fedha za nusu mwaka na nyaraka mbalimbali zitakazowasilishwa bungeni na kutoa mapendekezo jinsi ya kuboresha usimamizi na uwajibikaji kuhusiana na fedha za Umma;

xii. Kufanya utafiti wa mara kwa mara kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali (sera za kiuchumi, kodi, na fedha) na kutoa mapendekezo kwa Bunge ya jinsi ya kuboresha;

xiii. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;

xiv. Kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali;

xv. Kuchambua hoja mahususi zinazojitokeza kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili na kuchambua Bajeti za Wizara mbalimbali kwa ajili ya kulishauri Bunge na Serikali;

xvi. Kupitia taarifa za fedha za robo mwaka na nyaraka mbalimbali zitakazowasilishwa bungeni na kutoa mapendekezo kwa Bunge jinsi ya kuboresha;

xvii. Kutekeleza shughuli nyingine zinazohusu usimamizi wa masuala ya bajeti kama zilivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa kadri Bunge litakavyoelekeza chini ya Sheria ya Bajeti au Sheria nyingine;

1.3. Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 97(2) na 136 (3) (5) (8), and (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 kuhusu kukutana, ushirikishwaji wa Wadau kwenye shughuli za Kamati na uzingatiji wa Bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2021/22. Njia na mbinu zilizotumika ni zifuatazo: -

i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi inazosisimamia;

ii. Kuwataka Mawaziri kutoa maelezo na ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi.

iii. Ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kimkakati, Maeneo ambayo kuna vyanzo vya mapato ya Serikali au yanahusiana na malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ili kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa Miradi husika na kisha kulishauri Bunge ipasavyo;

iv. Kuwaalika Wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni yao kwenye Miswada ya Sheria iliyoletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) na 136 (8) (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020;

v. Kupokea, kuchambua na kujadiliana na Serikali kupitia Kamati ya Uongozi ya Bunge kuhusu Hoja mahsusi zilizotokana

na uchambuzi wa Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Bunge za Kisekta katika Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2021/2022; na

vi. Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuongeza uelewa na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo.

1.4. Shughuli za Kamati zilizotekelezwa

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/21;

b) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2020/2021;

c) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

d) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;

e) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

f) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti za Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021; pamoja na kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Mifuko hiyo Mwaka wa fedha 2021/2022;

g) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021 (The Finance Act, 2021), Muswada wa Mabadiliko ya Sheria mbalimbali Na 6 pamoja na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka 2022;

h) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023;

i) Kuchambua Taarifa za utekelezaji na utendaji kutoka kwenye Wizara inayosimamiwa na Kamati pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo;

j) Kuchambua Taarifa ya utendaji kazi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

k) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea wajumbe wa Kamati uwezo wa kutekeleza majukumu yake; Mafunzo hayo yalihusiana na masuala ya kodi, fedha pamoja na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato;

l) Kukutana na wadau wa masuala ya kodi na kujadili changamoto zao zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria mbalimbali za kodi na zisizo za kikodi zinazoathiri sekta binafsi. Baadhi ya Wadau waliokutana na Kamati ni wafuatao: - Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA), Tanzania Private Sector Foundation (TPSF), Tanzania Mobile Network Operators Association (TAMNOA), Confederation of Tanzania Industries (CTI), Tanzania Horticulture Association (TAHA), Tanzania Bankers Association (TBA), Tanzania Houting Operators Association (TAHOA), Tanzania Tour Operators Association (TATOA), Tanzania Debt Coalliation (TDC), Tanzania Milk Producers Association (TAMPA), Tanzania Gender Network (TGNP) pamoja na Taasisi, Wakala, Mamlaka na Mashirika mbalimbali ya Umma;

m) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti. Tafiti zilizofanyika ni Utafiti kuhusu Faida

na Hasara ya Michezo ya Kubahatisha Nchini pamoja na Utafiti kuhusu Uhimilivu wa Sera za Kibajeti Tanzania;

n) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2021/2022 kwa ajili ya kuishauri Serikali; Kwa kipindi tajwa, Kamati za Kisekta zilizowasilisha Hoja mahsusi zilikuwa zifuatazo: - Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Viwanda Biashara na Mazingira, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Maliasili na Utalii, Katiba na Sheria na Utawala na Serikali za Mitaa;

o) Kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Taasisi mbalimbali pamoja na miradi ya Kimkakati. Miradi iliyotembelewa ni Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Tanzanite, Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Mradi wa Uboreshaji wa Vituo vya mpakani pamoja na Mradi wa Uboreshaji wa Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa shukrani kwanza kwako wewe Binafsi na Pili kwa Serikali na wadau wote kwa ushirikiano wao uliowezesha kukamilika kwa shughuli hizi za Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0. UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1. Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelewa kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati wa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakayotolewa Taarifa ni yafuatayo: -

- i. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021;
- ii. Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2020/21 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22;
- iii. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (The Finance Bill, 2021);
- iv. Mapendekezo ya Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023;
- v. Hoja Mahsusi za Kamati za Bunge za Kisekta;
- vi. Ziara za Kamati za Kutembelea Taasisi, Idara na Mamlaka mbalimbali;
- vii. Mafunzo kwa Kamati;
- viii. Mafanikio katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;
- ix. Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;

2.2. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 inakwenda sambamba na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla. Kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimetathminiwa kama ifuatavyo: -

2.2.1. Pato la Taifa

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2020, Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 4.8** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 7** mwaka 2019. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchukuzi na uchimbaji madini. Kiasi hiki ni

kikubwa zaidi ya kile kilichokuwa kimekadiriwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) cha **asilimia 2.5** ikiwa chini ya lengo la nchi la kukua kwa **asilimia 5.5**. Kupungua kwa kasi ya ukuaji katika kipindi husika kulichangiwa na mvua zilizozidi wastani zilizosababisha mafuriko ambayo yaliharibu miundombinu ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo nchini na kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Uviko 19) ulioenea katika nchi nyingi ambazo ni washirika wetu wakubwa kibiashara. Vilevile, homa hiyo ya mapafu ilisababisha kushuka kwa sekta ya utalii ambayo inachangia kiasi kikubwa cha mapato ya kigeni.

2.2.2. Mfumuko wa Bei

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo ulifikia wastani wa **asilimia 3.3** mwaka 2020, ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.4** mwaka 2019. Mwenendo huu uko ndani ya lengo la muda wa kati la **asilimia 5.0** na ndani ya wigo uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kiwango ambacho hakizidi **asilimia 8.0** na wigo uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya **asilimia 3.0** hadi **7.0**.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki cha mfumuko wa bei kilitokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha, bei ndogo ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, na sera madhubuti ya fedha na sera ya bajeti. Hata hivyo, hali ya upungufu wa chakula katika baadhi ya nchi jirani, iliyosababishwa na nchi hizo kufunga baadhi ya shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa UVIKO-19, inaweza kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka kwa kiasi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuchukua tahadhari ya suala hili ili kuondokana na adha ambayo inaweza kujitokeza hapo baadae ikiwa ni pamoja na kuwa na hifadhi ya kutosha ya mazao ya chakula hasa ikizingatiwa kwa sasa Wananchi wameruhusiwa kuuza mazao yao nje ya nchi.

2.2.3. Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni imeendelea kuwa tulivu. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumuko mdogo wa bei, utekelezaji thabiti wa sera ya fedha, usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, kuimarika kwa urari wa biashara, pamoja na bei ndogo ya mafuta katika soko la dunia. Katika kipindi cha Desemba 2020, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,309.19** ikilinganishwa na **shilingi 2,300.62** kipindi kama hicho mwaka 2019 sawa na kushuka kwa **asilimia 0.37**. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba njia pekee na ya uhakika ya kuhakikisha kwamba thamani ya Shilingi ya Tanzania ina imarika dhidi ya Dola ya Marekani ni kuwekeza katika maeneo ambayo yataongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

2.2.4. Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2020, Deni la Serikali lilifikia **Shilingi trilioni 59.01**, sawa na ongezeko la **asilimia 7.6** ikilinganishwa na shilingi trilioni 54.85 kipindi kama hicho mwaka 2019. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni **Shilingi trilioni 42.83** na deni la ndani ni **Shilingi trilioni 16.18**. Ongezeko la deni limetokana na Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na malimbikizo ya riba ya deni la nje, hususan kwa nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris (Non Paris Club members) ambazo Serikali inaendelea kujadiliana nazo. Aidha, kwa viwango vyote vya kimataifa Deni letu ni himilivu na linalipika.

2.3. Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2020/21 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (5) (a) Bunge lilijadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 uliowasilishwa Bungeni na Waziri

wa Fedha na Mipango. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/22 – 2025/26 wenye Dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ulikuwa na maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Baadhi ya masuala yaliyobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo: -

2.3.1. Uwepo wa Miradi ya muda mrefu ambayo haitekelezwi

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kwamba utekelezaji wa Miradi ya kimkakati ya muda mrefu umekuwa ya kusuasua. Miradi iliyochambuliwa ni Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas - LNG) – Lindi; Mradi wa Mkulazi II – Mbigiri Estate; Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa Standard Gauge Railway ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Mradi wa Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Mradi wa Chuma – Liganga; na Mradi wa Commuter Train Dar es Salaam. Kamati ilitaka Serikali kuanza kutekeleza miradi hii katika mwaka wa fedha unaokuja kwa sababu miradi hii haitegemei Bajeti ya Serikali na ina manufaa makubwa kwa Taifa.

2.3.2. Miradi ya Barabara ya miaka mingi kutokutekelezwa kikamilifu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa barabara 38 zenye jumla ya **Kilomita 8,575.29** zilizopo kwenye hatua mbalimbali na kubaini mambo yafuatayo: Kwanza, kuna barabara ambazo zina miaka zaidi ya 10 katika hatua ya upembuzi yakinifu na uchambuzi wa kina na hazijaanza kujengwa. Pili, kuna baadhi ya barabara zimejengwa kilomita chache na ujenzi haujaendelea kwa miaka mingi. Aidha,

Barabara mpya zinaendelea kuibuliwa ilihali barabara za zamani hazijakamilika na kuna ongezeko la malipo ya riba kwa Serikali linalotokana na kutolipa wakandarasi kwa wakati kwa kigezo cha uhakiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha ujenzi wa barabara zilizoainishwa kwenye Mpango na kuharakisha malipo ya wakandarasi pindi hati za malipo (certificates) zinapowasilishwa. Pia, endapo itabidi Serikali ifanye uhakiki usizidi siku 20 za kazi. Hatua hizi zitasaidia kupunguza hasara inayotokana na riba na kuleta maendeleo yaliyokusudiwa kwa haraka.

2.3.3. Mpango kutokufikiwa malengo kutokana na upatikanaji wa fedha

Mheshimiwa Spika, Moja ya changamoto kubwa ya kutofikia malengo ya utekelezaji ni kukosekana kwa fedha za maendeleo. Kwa mfano, katika mwaka 2020/21 matumizi ya maendeleo yalifikia **asilimia 83.5** ya lengo na hii ni kwa fedha zinazotokana na mapato ya Serikali tu. Utoaji huu wa fedha za kugharamia umekuwa ni wa kuridhisha ukilinganisha na miaka ya nyuma. Hivyo, Kamati iliisitiza Serikali kutoa fedha za matumizi ya maendeleo kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili mipango tunayojiwekea kila mwaka itekezwe kama ilivyokusudiwa.

2.3.4. Ushirikishwaji hafifu wa Sekta Binafsi katika kutekeleza Mpango

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Sekta binafsi ni injini ya kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, ushirikishwaji wake katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo si wa kuridhisha. Sekta binafsi nchini bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i. Wingi wa Mamlaka za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi;

- ii. Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi;
- iii. Wingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja; na
- iv. Ukiritimba katika kupata vibali vya kazi na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Tangu kuanzishwa kwa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini "*Blue Print*" ni miaka mitano sasa. Hata, hivyo hadi hivi sasa hakuna Taarifa ya Serikali inayoonyesha katika kipindi cha miaka mitano imetetekelezwa kwa asilimia ngapi. Kamati inaishauri Serikali katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2022/23 na miaka inayokuja uwekwe utaratibu kwa kila sekta kuainisha hatua zilizochukuliwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kwa sekta husika. Vilevile imefika wakati sasa kufanya marejeo ya kina Comprehensive review ili kuangalia ufanisi wa mpango huo. Kamati inaamini kwamba utekelezaji wa *Blueprint* ni mwarobaini wa kutatua changamoto hizi.

2.3.5. Uwekezaji hafifu katika utekelezaji wa Miradi ya Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inachangia Shilingi **Trilioni 44.08** sawa na **asilimia 26.9** ya Pato la Taifa la Shilingi **Trilioni 163.88**. Mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye uchumi umeshuka kutoka **asilimia 29** mwaka 2015 hadi **asilimia 26.9** mwaka 2019 na Sekta imekuwa ikikua chini ya **asilimia 5**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba sekta zinazokuwa kwa kasi kama vile ujenzi **asilimia 14.4** ni kutokana na uwekezaji wa Serikali katika sekta husika. Hivyo, ni wazi kwamba Serikali ikifanya uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo kwa kuhakikisha inaendeleza kilimo cha umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na viuatilifu kwa bei nafuu, upatikanaji wa mbegu bora za mazao na mifugo, na kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo. Aidha, kuna haja ya kuongeza kasi katika kuongeza thamani ya mazao pamoja na kutafuta masoko ya uhakika ya mazao ya chakula na biashara. Hatua hizo

zitachochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini kwa kiasi kikubwa ikizingatiwa kwamba sekta ya kilimo inatoa ajira kwa asilimia 66.3 ya watanzania.

2.3.6. Utekelezaji wa Vipaumbele

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu maeneo ya Vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/21 ulibaini masuala yafuatayo: -

- i. Wingi wa Vipaumbele na hivyo kufanya mgawanyo wa rasilimali kuwa mgumu na kukamilisha vipaumbele vichache tu; na
- ii. Baadhi ya maeneo ya vipaumbele yamekuwepo tangu mpango wa kwanza wa maendeleo na havitekelezwi mfano ujenzi wa mabwawa ya Kidunda na Farkwa.

2.3.7. Ukwepaji wa Kodi na Biashara ya Magendo

Mheshimiwa Spika, Ukwepaji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hususan kupitia biashara za magendo, uhamishaji wa faida (transfer pricing) kwa Kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD receipt) wakati mauzo yanapofanyika, husababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: Kwanza ni kuangalia uwezekano wa kuanza kutoa mashine za EFD bure ili zitumiwe na wafanyabiashara wengi zaidi na pili ni kuimarisha Kitengo cha Kodi za Kimataifa cha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kupunguza ukwepaji wa kodi kupitia makampuni ya kimataifa. Aidha, TRA inashauriwa kufanya utafiti ili kubaini namna bora ya kupata mapato kutokana na uchumi wa kidijiti.

2.4. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (The Finance Bill, 2021)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati iliwasilisha

Bungeni taarifa yake ya maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (The Finance Bill, 2021)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021. Shughuli hii ilifanyika kwa kupitia kifungu kwa kifungu pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kupendekeza marekebisho pale ilipobidi. Sheria zilizowasilishwa na kufanyiwa kazi katika Muswada huo ni Sheria Kumi na saba (17) ambazo ni:-

- i. Sheria ya Makampuni, Sura 212 (The Companies Act, (Cap.212)
- ii. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura 306
- iii. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
- iv. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134;
- v. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
- vi. Sheria ya kodi ya Mapato, Sura ya 332;
- vii. Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura ya 289;
- viii. Shria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
- ix. Sheria ya Ardhi Sura ya 113, Sheria ya Ushuru wa Stempu Sura 189, Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Raia wa Kigeni Sura ya 436 Sheria ya Elimu, Mafunzo ya Ufundi Stadi Stadi Sura ya 82 na Sheria ya Rufaa za Kodi;
- x. Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418;
- xi. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
- xii. Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38;

xiii. Sheria ya Bandari Sura ya 166 na Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Sura 172

xiv. Sheria ya Uwakala wa Meli, Sura 415;

xv. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;

xvi. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; na

xvii. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 kwa kipindi cha nusu mwaka.

2.5. Mapendekezo ya Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2021 Serikali iliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza. Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadiliana na Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo na Mpango huo. Kimsingi, Mwongozo huo umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango yanaonesha kwamba katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni 39.4** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 7.4** ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2021/22 ya **Shilingi Trilioni 36.68**. Mapato ya ndani ukijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanatarajia kuongezeka hadi kufikia **Shilingi Trilioni 28,567.9** ikiwa ni sawa na **asilimia 72.5** ya bajeti. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni **Shilingi Trilioni 24.24**, mapato yasiyo ya kodi Shilingi **Trilioni 3.39** na mapato ya Halmashauri Shilingi

Bilioni 937.05. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha **Shilingi Trilioni 7.444** zikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapitio hayo, Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mapendekezo ya Mpango huo. Maeneo mahsusi yafuatayo:-

2.5.1. Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti sura ya 439 kinataka Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura (Contingency Fund). Pamoja na uwepo wa takwa hilo la kisheria, bado Serikali haijanzisha Mfuko huo badala yake imekuwa ikitenga fedha za dharura kupitia Fungu 21 – Hazina. Uwepo wa Mfuko huu ungeisaidia sana Serikali inapotokea majanga kama vile lilivyo gonjwa la UVIKO-19. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 kuanzisha Mfuko huu ili utusaidie tunapopatwa na majanga na kuondokana na utaratibu wa kuweka fedha za dharura katika Fungu 21.

2.5.2. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Njia ya Ubia (PPP)

Mheshimiwa Spika, Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi. Miradi ya PPP iliyobainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23 ni ile ile ambayo imekuwa ikianishwa kila mwaka na hakuna utekelezaji wa aina yoyote.

2.6. Hoja Mahsusi za Kamati za Bunge za Kisekta

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2021, Kamati ilipokea jumla ya hoja mahsusi 12 zilizowasilishwa mbele yake kutoka kwa Kamati za Bunge za Kisekta. Kati ya hoja hizo, hoja 6 zilihusu bakaa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka

wa fedha 2020/21, Hoja 5 zilihusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2021/22 na hoja 1 ilihusu mapendekezo kuhusu sera, sheria na mabadiliko ya kikodi na hivyo hazikuwa na athari ya kibajeti moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikamilisha jukumu hili kwa kukutana na Kamati ya Uongozi pamoja na Serikali kwa lengo la kufanya mashauriano kuhusu hoja husika. Katika kikao hicho, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilishwa katika Kamati ya uongozi na baadae Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati.

2.6.1. Hoja zilizofanyiwa Kazi na Serikali

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano baina ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali hoja zilizofanyiwa kazi na Serikali ni kama ifuatavyo: -

a) Ujenzi wa Majengo ya Balozzi za Tanzania Nje ya Nchi

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa majengo ya Ubalozzi ambayo imekua hoja ya muda mrefu, Serikali ilishaanza kazi za awali katika ujenzi wa jengo la Ubalozzi wa Tanzania nchini Oman. Aidha, Serikali iliahidi kuwa ujenzi wa majengo mengine ya Ubalozzi kwa nchi nyingine utaendelea kutengewa fedha kwa miaka ijayo. Kamati inaendelea kusisitiza ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuanza ujenzi wa Ofisi za Balozzi kwa Kutumia mifumo mingine ya fedha kama *Mortgage Financing*.

b) Mradi wa EPZ Development Kurasini

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa EPZ Development Kurasini Logistic Centre ambao licha ya Serikali kulipa fidia ya jumla ya **Shilingi Bilioni 101**, lakini takribani miaka saba (7) sasa Mradi haujaanza kutekelezwa. Serikali ilikubali kutoa fedha za fidia **Shilingi Milioni 556.79** kwa wananchi watatu (3) waliobaki kwenye fedha za matumizi mengineyo ya mwezi Aprili, 2021. Fedha hizo zilitolewa mwezi Aprili na wananchi

hao walilipwa na kubomoa makazi yao ili kupisha eneo la mradi.

c) Ulipaji wa Fidia wa Maeneo ambayo yamechukuliwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutokutolewa kwa fidia kwenye maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi kwa maeneo ya CSC Duluti, Kikombo, Chato na Nyabange, jumla ya **Shilingi Bilioni 10.9** zinahitajika. Serikali ilieleza kwamba Wizara ya Fedha na Mipango imepokea madai ya fidia kwa ajili ya Chato – Geita **Shilingi Milioni 972.2** na Nyabange – Mara **Shilingi Milioni 203.6** na fedha zilitolewa mwezi Aprili, 2021. Aidha, maeneo yaliyobaki ya CSC Duluti – Arusha na Kikombo - Dodoma, fedha zitatolewa baada ya uthamini kukamilika na madai kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango.

d) Utolewaji fedha kwa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1** fedha za ndani. Hadi kufikia mwezi Februari 2021 ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi Millioni 500** tu. Baada ya mashauriano Serikali ilitoa kiasi cha Shilingi Millioni 5000 kama ilivyokubalika katika mgao wa mwezi wa Mei, 2021.

e) Utengaji wa Fedha kwa ajii ya Miradi ya Mazingira

Mheshimiwa Spika, kwa muda sasa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira imekuwa ikitegemea fedha za maendeleo kutoka nje. Hivyo, Kamati ilisisitiza kwamba ni lazima sasa Serikali ianze kutenga fedha za ndani ili kurekebisha mazingira. Serikali ilifafanua kwamba ilikubaliana na ushauri wa Kamati kiasi cha **Shilingi Milioni 400** kiliongezwa katika Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 31 ya mwaka 2021/22 ikiwa ni *Commitment* ya Serikali katika kusimamia masuala ya mazingira kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 1**.

f) Athari za mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2019/20

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yaliyofanyika kupitia sheria ya Fedha ya mwaka **2019/20** yaliondoa jukumu la kukusanya na kutumia fedha zao kwa Mamlaka za Ngorongoro (NCAA), Wanyamapori (TAWA) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Hatua hii imeleta changamoto kubwa kwa jamii za Wanyamapori (WMA) kwa kutopata mgao wao stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Wanyama Pori kwa sababu fedha zote zinazokusanywa zinaenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

g) Mgao wa Fedha kwa Jamii za Uhifadhi WMA

Mheshimiwa Spika, Baada ya mashauriano, Serikali ilikubali kupeleka jumla ya **Shilingi Milioni 175.41** kwa wanufaika ambao ni Vijiji, WMAs na Wilaya. Aidha, Serikali iliahidi kufanya usuluhishi (Reconciliation) wa takwimu za malipo yaliyowasilishwa na WMAs ikilinganishwa na takwimu za mfumo wa MNRT Portal ili kuhakikisha kwamba WMAs zinapata stahiki zao kulingana na Sheria kabla ya mwisho wa mwaka 2020/21.

2.6.2. Hoja ambazo Serikali iliahidi kuzifanyia kazi

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ambazo zilihusu masuala ya Sera na kisheria Serikali iliomba muda ili iweze kuzishughulikia zaidi, Hoja hizo zilihusu utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mamlaka za TAWA, TANAPA na NCA pamoja na namna ambavyo matumizi yao yanaidhinishwa hasa ukizingatia Mamlaka hizi zina Bodi zake pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina kama waangalizi wakuu. Ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali imeendelea kuzifanyia kazi hoja hizo kama ilivyoahidi.

2.7. Ziara za Kamati za Kutembelea Taasisi, Idara na Mamlaka mbalimbali

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2021 hadi Januari, 2022, kwa nyakati tofauti, Kamati ilifanya ziara katika

mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Ziara hizo zilikuwa na lengo la: -

- i. kukagua shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati;
- ii. kukagua utekelezaji wa Mifumo mbalimbali ya kikodi inayosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);
- iii. kukagua utekelezaji wa Mfumo wa Akaunti Jumuiifu ya Fedha jinsi unavyofanya kazi katika ngazi tofauti Serikalini;
- iv. kutembelea na kukagua shughuli za viwanda pamoja na mashamba ya maua na mbogamboga mjini Arusha; na
- v. Kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kodi zinazochukuliwa na Serikali kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali na kuchochea uchumi wa nchi.

2.7.1. Masuala muhimu yaliyojitokeza

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari naomba niwasilishe masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa ziara za Kamati kama ifuatavyo: -

a) Bandari ya Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini masuala makubwa mawili; kwanza, ni kuhusu suala la mkataba wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Tanzania International Container Terminal Services Limited (TICTS). Kamati ilitoa maelekezo kwa Serikali kupitia kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kulifanyia kazi suala la Mkataba kati ya TPA na TICTS ili kuangalia maslahi ya Taifa kama yanazingatiwa. Aidha, kutokana na uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam ni vyema Mkataba wa TICTS ukafanyiwa mapitio. Vilevile, Serikali iangalie uwezekano wa kuipa TPA eneo la EPZA la Kurasini ili litumike kwa ajili ya kuendeleza Bandari kuliko ilivyo hivi sasa ambapo limekuwa maegesho ya malori kwa muda wa miaka 5.

b) Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ilibaini changamoto zifuatazo: -

i. Mtaji mdogo hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

ii. Utozaji wa Kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya madawa aina ya "Polyvinyl chloride" (PVC) pamoja na vipuri vya mashine pamoja na ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kwa kiwanda cha Keko Phamacetical;

iii. Utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na Ile ya Maendeleo ya Reli kwenye Mashine na Vitendanishi vinavyotumika kutoa huduma za uchujaji damu na hivyo kuongeza gharama za huduma hizo nchini;

iv. Mlolongo wa utaratibu wa ununuzi wa dawa unaosababishwa na Sheria ya manunuzi ya umme na hivyo kuchelewesha ununuzi wa Dawa; na

v. Kiwanda cha Keko Pharmaceutical Industry kukabiliwa na deni la Shilingi Bioni 12 ambalo lilikopwa na Mbia wa kiwanda hicho toka Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kwanza kuanzisha utaratibu wa utoaji wa fedha za dawa kwa miezi miwili kila mwanzo wa mwaka na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) kushughulikia deni la Kiwanda cha dawa cha Keko.

c) Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Kodi wa TRA

Mheshimwa Spika, Kamati ilitembelea Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kujionea mfumo wa kidigitali wa marejesho ya kodi (Electronic Filing of Tax Returns System). Mfumo umetengenezwa mahsusi kupokea marejesho ya kodi, kuchakata marejesho na kodi na kutatua migogoro ya kikodi. Mfumo huu utawasaidia Walipakodi kufanya marejesho ya kodi kidigitali, kuweka kumbukumbu sawa na kuhifadhi

nyaraka za marejesho ya kikodi na za kibiashara kwa wepesi zaidi kulingana na sheria za kikodi za nchi. Kamati ilishauri TRA kuuboresha Mfumo huu ili uweze kuwahudumia walipa kodi wa sekta zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata pia fursa ya kutembelea Mfumo wa Uingizaji na Uondoshaji wa Bidhaa Bandarini na Mipakani uitwao TANCIS, ambao unaendelea kufanya kazi vizuri.

d) Tanzania Horticulture Association (TAHA)

Mheshimiwa Spika. Kamati ilitembelea taasisi ya Tanzania Horticulture Association (TAHA) ambayo ni taasisi binafsi inayotetea ukuaji na ushindani wa tasnia ya Kilimo cha mbogamboga na maua nchini Tanzania. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua mashamba mbalimbali ya maua na kubaini changamoto mbalimbali kama kufungwa kwa mashamba ya maua 9 na mashamba ya mboga mboga 5 na hivyo Serikali kupoteza kiasi cha Dola za Marekani Milioni 24 kila mwaka, na kupoteza ajira za watu zaidi ya 1000.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, uwepo wa tatizo la kukosekana kwa mnyororo wa thamani wa baridi (Cold chain) madhubuti, husababisha mazao mengi kuharibika wakati wa kusafirishwa. Pia, sekta inakabiliwa na changamoto za kulifikia soko zinazosababishwa na mifumo mibaya ya kitaasisi, gharama kubwa za uzalishaji, huduma mbovu za kiugani zinazopelekea uzalishaji mdogo, kukosekana kwa utafiti na changamoto za kikodi zilizopelekea kufungwa kwa baadhi ya mashamba ya maua na mbogamboga.

e) Kiwanda Bia TBL na Kiwanda cha pombe kali aina ya K-VANT

Mheshimiwa Spika. Kamati ilitembelea viwanda viwili mkoani Arusha kiwanda cha bia cha TBL na kiwanda cha K-VANT ili kukagua Mfumo wa Kodi za Kieletroniki za (Electronic Tax Stemp-ETS) kiwandani. Viwanda vyote vina jumla ya mashine za ETS 18 kati ya hizo mashine 10 zimefungwa katika uzalishaji

wa bia na mashine 3 zimefungwa katika uzalishaji wa mvinyo na spiriti na 5 ni kwa ajili ya kinywaji cha K-VANT. Kamati ilibaini kuwa kila mwaka TBL huilipa ETS kiasi cha Dola za Marekani Milioni 9 sawa na Shilingi Bilioni 20 za kitanzania. Fedha hizo zote huenda kwa Mwekezaji moja kwa moja na hakuna fedha zinazopitia Serikalini. Hivyo, Kamati ilishauri Serikali kuangalia upya Mkataba wa SCIPA ambae ndiye Mmiliki wa Mfumo na TRA ili Serikali iweze kuongeza mapato.

f) Shirika La Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) na Kituo Cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)

Mheshimiwa Spika. Kamati ilitembelea Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) zilizoko Njiro Mkoani Arusha. Lengo la Kamati kutembelea taasisi hizi lilikuwa ni kuangalia ugunduzi unaofanyika pamoja na mahitaji ya kibajeti ya Taasisi hizi. Kamati ilibaini kwamba Taasisi hizi zinakumbwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhaba wa fedha za maendeleo, uhaba wa magari ya uendeshaji wa Taasisi, upungufu wa Wafanyakazi pamoja na uhaba wa zana za kiutendaji. Kamati ilishauri Serikali kutatua changamoto za Taasisi hizi muhimu kwa maendeleo ya Taifa hasa ile ya upatikanaji wa fedha za maendeleo.

g) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Makao Makuu ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA). Madhumuni ya ziara hii yalikuwa ni kuangalia utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021. Kamati ilielezwa kwamba utekelezaji wa Sheria hiyo kwa TANAPA umeleta athari kubwa sana za kiutendaji zifuatazo: -

- i. Fedha zinazokusanywa hazirejeshwi kwa wakati na hivyo kufanya shughuli za Shirika kukwama;
- ii. TANAPA inakuwa na takwimu halisi za wageni bila takwimu halisi za mapato;

- iii. TRA inakuwa na taarifa za fedha bila kuwa na idadi halisi ya wageni walioingia hifadhini;
- iv. TRA huchukulia fedha zote zilizoingia kwenye akaunti zao za benki kuwa ni mapato pasipokujua kuwa kuna fedha za huduma (Service Fees) ambazo hutolewa na wateja kama (upfront fee of the service);
- v. Ufanisi mdogo katika kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za utalii; na
- vi. Kukosekana kwa fedha za dharura za kudhibiti ujangili hifadhini.

h) Kutembelea Mpaka wa Tanzania na Kenya- Namanga

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mpaka wa Tanzania na Kenya- Namanga ili kuangalia Jinsi Kituo cha Pamoja cha Forodha (One stop Boarder Post –OSBP) kinavyofanya kazi. Katika ziara hiyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea upande wa Kenya na kujionea namna Kituo cha Kenya cha Forodha kinavyofanya kazi, na hivyo kuweza kufanya ulinganishi sahihi na upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba Kituo cha Pamoja cha Forodha kinavyofanya kazi (One stop Boarder Post – OSBP) kwa upande wa Tanzana kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- i. Ukosefu wa Cargo Scanner kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo;
- ii. Upungufu wa nyumba za makazi ya maafisa wa forodha na uhamiaji;
- iii. Biashara ya magendo katika mpaka huo; na
- iv. Uhaba wa watumishi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi hasa ya (cargo scanner) imesababisha ucheleweshaji wa uondoshaji wa mizigo katika

mpaka huo kwa upande wa Tanzania na hivyo kuwa na msururu mrefu wa magari na gharama kubwa kwa wasafirishaji. Aidha, kamati ilibaini mipaka yote rasmi nchini isipokuwa Bandarini na Uwanja wa Ndege wa Dar es salaam hakuna mashine za kukagulia mizigo mikubwa (Cargo scanner). Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba ianunua na kusimika (cargo scanner) katika mipaka yote ya Tanzania ili kupunguza msongamano mipakani inayotokana wa ukaguzi kwa kutumia macho yaani Physical Verification ili kuondoa mianya ya rushwa na kuongeza mapato ya Serikali.

2.8. Mafunzo kwa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika, Kamati ilipata fursa ya kupata mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uwezo na ujuzi kwa Wajumbe wa Kamati. Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na Programmu za Miradi ya LSP II na PFMRP ziliratibu mafunzo hayo. Mafunzo hayo yaliwasaidia Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia Bajeti ya Serikali na hatimaye kuweza kushauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Baadhi ya mafunzo ambayo Kamati ilishiriki ni yafuatayo: -

- i. Mafunzo juu ya majukumu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), pamoja na mifumo inayosimamiwa na TRA hasa TANCIS, ETS pamoja na ITAX;
- ii. Mafunzo kuhusu Akaunti Jumuiifu ya Fedha (Treasury Single Account);
- iii. Mafunzo kuhusu uhimilivu wa Deni la Taifa na Viashiria vyake;
- iv. Mafunzo kuhusu Mfumo Jumuiifu wa Uingizaji na Uondoshwaji wa Mizigo Tanzania (Tanzania Customs Integrated System –TANCIS);

v. Mafunzo ya Uelewa wa Sheria mbalimbali za Kodi na kupitishwa kwenye Sheria ya Ongezeko la Thamani ya Kodi (VAT Act CAP 147) na Sheria ya Utawala wa Kodi (Tax Administration Act, 2014);

vi. Mafunzo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE);

vii. Mafunzo ya namna ya kukokotoa viashiria muhimu vya uchumi ikiwa ni pamoja na Pato la Taifa, Mfumuko wa Bei, Fahirisi za Bei na hali ya umaskini;

viii. Mafunzo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Benki Kuu kuhusu usimamizi wa Sera za Mapato na Sera za Kibajeti (Monetary and Fiscal Policy);

ix. Mafunzo ya uelewa juu ya Sheria ya Msajili wa Hazina

x. Mafunzo kuhusu namna ya kuchambua na kuzitumia Taarifa za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

2.9. Mafanikio katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali, Kamati ilifanikiwa katika maeneo yafuatayo; -

2.9.1. Kuongeza Mapato ya Serikali kupitia mabadiliko ya Sheria mbalimbali

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021, Serikali ilileta mapendekezo huhusu kuanzisha tozo itakayotozwa kwenye miamala ya simu. Aidha, Serikali pia ilianzisha kutoza Kodi ya Ushindi kutoka kwenye mapato ghafi kwenye michezo ya (Virtual games). Aidha, Serikali ilifanya maboresho katika Sheria ya Ushuru wa Mafuta ili kuongeza Shilingi 100 kwa ajili ya maji na barabara vijijini. Vyanzo vyote hivi vinatokana na ushauri wa Kamati kwa Serikali na baada ya kukubalika vimeongezea mapato ya Serikali ya takribani Shilingi Billioni 600 ambazo zimeelekezwa

kwenye miundombinu ya barabara, afya na elimu na matokeo yanaonekana.

2.9.2. Mgawanyo wa Fedha za Mkopo toka IMF

Mheshimiwa Spika, Utakumbuka kwamba Baada Serikali kupokea Mkopo wa **Shilingi Trilioni 1.31**. kwa ajili ya kugharamia Mpango wa kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii kutokana na UVIKO-19, Kamati ya Bajeti ilikutana na Serikali tarehe 6 na 7 Oktoba 2021 ili kujadiliana kuhusu Mgao huo. Mafanikio ya majadiliano hayo yalikuwa kama ifuatavyo: -

i. Serikali ilikubali kupunguza **Shilingi Bilioni 40** kutoka kwenye fedha za Miradi ya Maji iliyopo Mijini na kuongeza Bajeti ya miradi ya maji iliyopo vijijini hadi kufikia **Shilingi Bilioni 55.5**;

ii. Serikali ilikubali kufanya reallocation ya fedha zisizopungua Shilingi Bilioni 66 kwenye fedha zilizotengwa kwa shughuli mbalimbali za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya madarasa ya Shule shikizi; na

iii. Kupunguza ununuzi wa *Advanced Ambulances* 20 na kuongeza ununuzi wa *Ambulance* za kawaida zaidi ya 40.

2.9.3. Kupungua kwa Ushuru wa Stempu za Kieletroniki (ETS)

Mheshimiwa Spika, Moja ya Changamoto kubwa iliyoletwa na Mfumo wa Stempu za Kieletroniki (ETS) ni gharama kubwa za mfumo huo. Tunakubaliana kwamba Mfumo huo ni muhimu katika kudhibiti udanganyifu na kuongeza mapato ya Serikali lakini umekuwa ukilalamikiwa sana na wafanyabiashara. Baada ya majadiliano ya kina kati ya Serikali na Kamati, Serikali ilikubali kupunguza gharama za mfumo huo kutoka **Dola za Marekani 20** kwa stempu 100 hadi **Dola za Marekani 18.5** kwa stempu 1000 katika kipindi cha mpito wakati wanatafuta mkandarasi mwingine atakaendesha mfumo huo kwa bei nafuu zaidi.

2.9.4. Kubadili Mfumo wa Utoaji wa Idhini ya Matumizi kwa TCRA, TPA TASAC

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa iliyoletwa na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 ni kuzilazimisha Mamlaka za Mawasiliano (TCRA), Bandari (TPA) na Wakala wa Meli (TASAC), ambazo zinajiendesha kibiashara, kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (Paymaster General) kabla hazijatumia fedha zilizotengwa kwenye Bajeti zao. Kimsingi, Mamlaka hizi si tu kwamba zinasimamiwa na Msajili wa Hazina na zina Bodi zake, lakini mamlaka ya matumizi yamepelekwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Baada ya mabadiliko ya sheria, changamoto ya uchelewesaji wa vibali na utoaji wa huduma kwa haraka ilionekana mara moja. Hivyo, Kamati ilishauriana na kukubaliana na Serikali kwamba idhini ya matumizi ya fedha iwe inatolewa kwa robo mwaka na sio kila mwezi kwa sababu kimsingi idhini za Mamlaka hizi zinatolewa kwa mujibu wa Bajeti zao zilizopitishwa. Hata hivyo, pamoja na makubaliano hayo, bado Kamati itaendelea kujadiliana na Serikali kuhusu uamuzi huu ili kuona kama una afya kwa maendeleo ya mashirika hayo.

2.9.5. Taarifa zilizowasilishwa Bungeni na Mdahalo kuhusu Maswala ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Katika Kipindi cha Mwaka mmoja, Kamati ya Bajeti imeweza kuwasilisha Bungeni jumla ya taarifa 8 zinazohusu Bajeti ya Ofisi ya Bunge, Mfuko wa Mahakama, Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na Mafungu 8 ya Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Kamati imeweza kuwasilisha Taarifa kuhusu Mpango wa tatu wa maendeleo ya Taifa wa miaka mitano (2020/2021 – 2025/2026), Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23 pamoja na Taarifa kuhusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22. Vilevile Kamati imefanikiwa kuandaa na kuwasilisha Bungeni Taarifa kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 na Muswada kuhusu Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na 6 wa mwaka 2021. Pamoja na mafanikio hayo, Kamati pia imeweza

kuandaa Mdahalo wa Masuala ya Uchumi mwezi Juni 2021 kabla ya kuanza majadiliano ya Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2021/22.

2.10. Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatavyo: -

2.10.1. Changamoto ya Kanuni ya Uwasilishaji wa Taarifa za Kamati ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 69(C), Mwenyekiti anaewasilisha Taarifa ya Kamati anatakiwa kuiwasilisha kwa muda usiozidi dakika 30. Changamoto kubwa inayoikumba Kamati ya Bajeti ni Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali huwasilishwa kwa zaidi ya masaa mawili na Mpango wa Maendeleo ya Mwaka huwasilishwa pia kwa zaidi ya masaa 2 lakini Kamati ya Bajeti ambayo inachambua nyaraka zote hizo mbili inatakiwa kutoa mapendekezo yake kwa dakika 30 tu. Hivyo, Kamati inashauri wakati wa kuwasilisha Taarifa yake inayohusu Bajeti Kuu ya Serikali na Mpango wa Maendeleo itengewe muda wa dakika 60 sawa na Saa 1 ili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kuelezewa ipasavyo uchambuzi uliofanywa na Kamati.

2.10.2. Uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali pamoja na Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka husika

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo ambalo huwa linachukua sura kubwa ya Hotuba ya Bajeti kila mwaka ni mabadiliko ya Sheria mbalimbali za Kodi. Hivyo, kiutaratibu ilitakiwa pindi Waziri wa Fedha na Mipango anaposoma Hotuba yake iambatane na Muswada wa Sheria ya Fedha kwa Mwaka husika. Hata hivyo, imekuwa haifanyiki hivyo na badala yake muswada huletwa baadae na hivyo kuipa Kamati muda finyu wa kuwaita wadau na kupata maoni yao. Hivyo, inashauriwa kwamba Waziri wa Fedha anapowasilisha Hotuba ya Bajeti iende sambamba na Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka husika.

2.10.3. Ziara za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 116(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Mwezi Machi ya kila mwaka Bunge hupokea Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata. Mara baada ya kuwasilishwa kwa Mpango na Ukomo wa Bajeti, Kamati ya Bajeti hulazimika kukaa na kuanza kuzichambua nyaraka hizo na kushindwa kwenda kufanya ziara ya Kamati ambazo zinatakiwa kufanyika kwa mujibu Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, Kwa msingi huo kila mwezi Machi, Kamati ya Bunge ya Bajeti hushindwa kufanya ziara za kukagua utekelezaji wa miradi ya Wizara na maeneo inayosimamia kabla ya kufanya uchambuzi wa Bajeti husika. Hivyo, Kamati inashauri kwamba kwa Bunge la Mwezi Machi kila Mwaka ni vyema ikapewa wiki moja ya ziada ili ifanye ziara za ukaguzi wa miradi kabla ya kipindi kilichopangwa cha vikao vya Kamati za Bunge na ili pindi Mpango wa Maendeleo unapowasilishwa ibaki ikifanya uchambuzi wakati Kamati nyingine za kisekta zikienda kufanya ziara.

SEHEMU YA TATU

3.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU MWAKA KUENZIA MWEZI JULAI HADI DESEMBA 2021 NA MWELEKEO HADI MWEZI JUNI, 2022

3.1. Sura ya Bajeti na Utekelezaji hadi Disemba 2021

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipanga kukusanya na Kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 36,681.9** Kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi bilioni 23,003.0** zilitarajiwa kutumika kwa matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 13,678.9** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021 Serikali ilimetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya Shilingi **bilioni 16,505.2**, kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 11.143** zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi trilioni 5.361**. Kwa ujumla utekelezaji

wa Bajeti ni **asilimia 49.5**. Hivyo kwa kuwa ni utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2021/22 unaweza kufikia asilimia 85 hadi 90. Jambo hili si la kubeza na inatakiwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua hii kubwa.

3.2. Uchambuzi wa Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai hadi tarehe 31 Disemba 2021 Serikali iliweza kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 18,199.6** sawa na **asilimia 49.6** ya makadirio ya kukusanya na kutumia **Shilingi trilioni 36.6**. Hatua hii ni ya kupongeza kwa sababu inaonyesha kwamba makusanyo ya mapato yanatarajiwa kufikia walau **asilimia 80 hadi 90** ya matarajio.

Jedwali Na. 1 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

| Na | Chanzo | Bajeti (2021/22) | Utekelezaji (2021/22) | Asilimia % ya bajeti |
|----|-----------------------------------|------------------|-----------------------|----------------------|
| 1. | Mapato ya Kodi | 22,471.1 | 10,316.8 | 46 |
| 2. | Mapato ya Halmashauri | 863,858.0 | 460.2 | 53 |
| 3. | Mapato yasiyo ya kodi | 3,049.8 | 1,108.9 | 36 |
| 4. | Misaaada na Mikopo kutoka nje | 2,955.9 | 1,367.8 | 46 |
| 5. | Mikopo ya ndani | 1,838.8 | 2,361.8 | 128.4 |
| 6. | Mikopo ya ndani roll over | 3,150.3 | 1,201.8 | 38 |
| 7. | Mikopo ya masharti ya kibia shara | 2,352.1 | 1,382.3 | 59 |
| 8. | Miradi ya nje | 2,955.9 | 0 | 0 |
| 9. | Jumla | 36,681.9 | 18,199.6 | 49.6 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.3. Uchambuzi wa Mwenendo wa Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021 Serikali imetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya **Shilingi trilioni 16.199**, sawa na **asilimia 45.9** ya bajeti yote ya mwaka Kati ya fedha hizo Shilingi **trilioni 11.14** zilitumika kwa matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 5.361** zilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

3.4 Utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 kwa Kipindi cha Nusu Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa 2021 Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria 17 kupitia Sheria ya Fedha. Mabadiliko hayo yalifanyika kwa malengo ya kutekeleza Blue Print ya uboreshaji wa Mazingira ya biashara nchini, uboreshaji wa mfumo wa kodi, kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kutoa msamaha kwa maeneo muhimu ili kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za Kiuchumi. Hadi kufikia mwezi Disemba 2021 maboresho hayo yalikuwa yamekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 443.46** sawa na **asilimia 28.35** ya kukusanya **shilingi trilioni 1.563**.

Mheshimiwa Spika, Kutofikiwa kwa lengo kumetokana na sababu mbalimbali za msingi ni kama zifuatazo: -

- i. Uwepo wa biashara ya Magendo katika mipaka yote ya Tanzania ya Nchi kavu na mipaka ya majini;
- ii. matumizi yasiyoridhisha ya mashine za EFD kwa wafanyabiashara kutotumia mashine za EFD katika ufanyaji wa biashara;
- iii. kutokana na utafiti wa Tanzania Economic Survey 2019, unaonyesha kwamba sekta isiyo rasmi nchini inakadiriwa kufikia asilimia 70 ya biashara yote nchini;
- iv. Walipakodi wengi kushindwa kulipa madeni yao halali ya kodi ambayo wanadaiwa kwa mujibu wa sheria; na
- v. Kukosekana kwa elimu ya mlipa kodi na hivyo wananchi wengi kutotambua kama kudai risiti ni haki yao na kwa kutokufanya hivyo wanamuongezea mfanyabishiashara fedha zisizo halali ambazo zilitakiwa ziwe za Serikali.

3.5 Mgawanyo wa Fedha za Mkopo kutoka IMF Shilingi Trilioni 1.31 pamoja na Utekelezaji wake

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba uliridhia Kamati ya Bunge ya Bajeti ikutane na Serikali mwezi Oktoba, 2021 kwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ajili ya kujadili Mpango na Mgawango wa fedha za Mkopo kutoka IMF zenye jumla ya shilingi Trilioni 1.31. Kikao hicho kilihusisha Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mgawanyo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali hapo chini: -

Jedwali Na 2. Mgawanyo wa Fedha za Mkopo kutoka IMF

| ENEO | USD MILIONI | SHILINGI BILIONI | ASILIMIA |
|---|--------------|------------------|--------------|
| Maji | 66.8 | 154.4 | 11.8 |
| Afya | 214.1 | 494.1 | 37.7 |
| Elimu | 125.7 | 290.4 | 22.2 |
| MoEST | 20.6 | 47.7 | 3.6 |
| PO-RALG | 105.1 | 242.7 | 18.5 |
| Uwezeshaji wa Vijana, Wanawake na makundi yasiyojweza | 4.3 | 10.0 | 0.8 |
| Mradi wa hifadhi ya jamii | 10.8 | 25.5 | 1.9 |
| Maliasili | 43.4 | 100.2 | 7.6 |
| Utawala | 2.2 | 5.0 | 0.4 |
| Zanzibar | 100.0 | 231.0 | 17.6 |
| JUMLA | 567.3 | 1,310.6 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, Mkopo huu wa IMF umetoa mafundisho yafuatayo kwa Serikali: -

- i. Fedha za maendeleo zikifuatiliwa kwa makini kama zinavyofuatiwa fedha hizi za mkopo matokeo chanya yanaonekana;
- ii. Endapo kungekuwa na usimamizi thabiti kwenye fedha za maendeleo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kusingekuwa na ubadhilifu katika utekelezaji wa miradi ya Serikali;
- iii. Inawezekana kabisa kwa Serikali kulihusisha Bunge kwenye mgawanyo na matumizi ya mikopo ambayo Serikali inachukua ili kuleta uwazi na uwajibikaji; na

iv. Lazima sasa Serikali iwe na maeneo ya vipaumbele kama ilivyofanya kwenye mkopo huu kwa kuchagua maeneo machache na kuyamaliza kabisa na sio kila mwaka kutenga fedha kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini mafundisho haya yakitumika vizuri Taifa letu litapata Maendeleo ya haraka.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

4.1 Utekelezaji wa Sheria ya Mawasiliano na Kielektroniki (EPOCA)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya EPOCA mwaka 2017, yalielekeza Kampuni zote za simu kujiorodhesha kwenye soko la hisa na kuuza **asilimia ishirini na tano (25%)** ya hisa zake kwa umma na hatimaye kampuni hizo kuorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es salaam,

NA KWA KUWA, Kamati ilibaini kuwa kati ya kampuni zote za simu ni kampuni ya Vodacom tu ambayo imeweza kuingia kwenye soko, lakini sio hisa zote zimeweza kununuliwa na inalalamikiwa kwa kutoa gawio dogo lakini na kushuka kwa thamani ya hisa zake.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Kampuni za simu ambazo bado hazijaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ziorodheshwe ili Watanzania waweze kushiriki katika uwekezaji kwenye Sekta ya mawasiliano kama sheria inavyoelekeza.

4.2 Utekelezaji wa Hoja Mahususi zilizofanyiwa maamuzi katika Kikao baina ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, katika utekelezaji wa shughuli za Kamati, imebainika kwamba Serikali imekuwa haitekelezi kikamilifu hoja mahususi ambazo zimeamriwa katika Kamati ya Uongozi.

NA KWA KUWA, kutotekelezwa kwa maazimio ya Kikao hicho cha Mashauriano huathiri kifedha na utendaji wa Taasisi mbalimbali za Serikali kama ilivyo sasa kwa Shirika la Utangazi la Taifa TBC kutopelekewa fedha zote za maendeleo.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali umuhimu wa kujiwekea utaratibu wa kushughulikia na kufuatilia makubaliano na maazimio ya kikao hicho muhimu.

4.3 Mwenendo wa Viwango vya riba na Mfumuko wa Bei

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, viwango vya riba katika sekta ya benki vimeendelea kuwa vya juu kuliko uhalisia. Kwa Mfano hadi kufikia Novemba 2019 viwango vya riba vilikuwa **asilimia 16.87** ilihali mfumuko wa bei ulikuwa kwa **asilimia 3.8**.

NA KWA KUWA, kutokana na uhusiano wa moja kwa moja kati ya mfumuko wa bei na viwango vya riba haitarajwi kiuchumi viwango vya riba vizidi mfumuko wa bei kwa zaidi ya mara mbili.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali kuangalia gharama za uendeshaji wa mabenki ili kuhakikisha viwango vya riba vinaendana na mfumuko wa bei.

4.4 Kushuka kwa Viwango vya Riba za Mikopo Binafsi

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, riba ya mikopo binafsi imeendelea kuwa na kiwango cha riba cha juu cha wastani wa **asilimia 17** hadi **20**. Aidha, Kamati ilipokutana na Umoja

wa Mabenki nchini ili kubaini ni kwanini wanatoza riba kubwa waleleza sababu zifuatazo: -

i. Ili kupata taarifa za mkopaji lazima wakusanya Taarifa kwenye Taasisi zaidi ya 6 za Serikali n azote wanalipia ada. Mfano NIDA, RITA, BRELLA, TCRA, CRB na TRA;

ii. Serikali inatoza ada ya asilimia 2 kwa kila mkopo kwa watumishi wa umma wanaokusanya; na

iii. Hatua ya Serikali kuandoa mifuko ya dhamana ambayo ilikuwa ikisaidia kupunguza vihatarishi na kutoza riba ya chini.

NA KWA KUWA, Benki Kuu imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba riba za mabenki zinashuka ikiwa ni pamoja na kutoa Shilingi Trilioni 1 kwa ajili ya Kilimo lakini bado riba hazishuki.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali iweke mikakati ya kushughulikia changamoto za Sekta za Kibenki kama nilivyobainishwa ili riba ipungua na kufikia kati ya **asilimia 9** hadi **12** ili mikopo ipatikane kwa gharama nafuu.

4.5 Utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mazingira na ufanyaji wa biashara nchini (Blueprint)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, kwa mujibu wa Taarifa ya Urahisi wa Ufanyaji Biashara na Uwekezaji inayoandaliwa UNCTAD, Tanzania inashika nafasi ya 141 mwaka 2020.

NA KWAKUWA, utekelezaji wa Blueprint ulitarajiwa kuwa mwarobaini wa Tatizo la mazingira yasiyoridhisha ya biashara nchini, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu Blueprint ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo inatekelezwa kwa kusuasua. Pia, Utekelezaji wa Blueprint utasaidia kuiwezesha sekta binafsi nchini kushiriki katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

4.6 Serikali kuweka vipaumbele vichache kwenye mpango

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, kila mwaka Serikali inatoa vipaumbele vyake katika mpango wa mwaka ambavyo kwa uchambuzi wa kamati vimeonekana kuwa vingi kutekelezwa kwa mwaka mmoja.

NA KWA KUWA, wingi wa vipaumbele umekuwa unasababisha kutekelezwa nusu nusu au kutovitekeleza kabisa.

HIVYO BASI, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwa na vipaumbele vichache walau kila sekta na kuvikamilisha kwa zaidi ya **asilimia 90**, hasa vile vinavyoweza kukamilika katika mwaka mmoja.

4.7 Miradi ya muda mrefu ambayo haitekelezwi

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, kumekuwa na miradi mingi ya muda mrefu ambayo haitekelezwi kama vile Mchuchuma na Liganga, Engaruka Magadi Soda, Ujenzi wa Mabwawa ya Farkwa na Kidunda, na Kurasini Logistic Hub.

NA KWA KUWA, Kamati za Kisekta na Kamati ya Bajeti zimekuwa zikifuatilia miradi hiyo.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali iandae Taarifa ya kina na kuiwasilisha Bungeni kuhusu utekelezaji wa miradi yote ya kimkakati ya muda mrefu na namna itakavyotekelezwa katika muda wa kati na mrefu.

4.8 Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Malengo ya Mpango wa Maendeleo

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Moja ya changamoto kubwa ya kutofikia malengo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kukosekana kwa fedha za maendeleo.

NA KWA KUWA, mafanikio ya Mpango yanapimwa kwa utekelezaji wa Malengo ya Mpango.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali kuandaa na kutumia njia nyingine za kugharamia mpango kama matumizi ya Hati fungani ya Miundombinu *“Infrastructure Bond”* ili fedha zipatiakane kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

4.9 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa njia ya ubia (PPP)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida na pia ni njia ya kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

NA KWA KUWA, tangu kuanzishwa kwa Sheria ya PPP mwaka 2010 hakuna mradi hata mmoja ulitekelezwa kwa njia ya PPP.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali kufanya tathmini na kubainisha sababu za msingi za kukwama kwa utekelezaji wa Miradi kwa njia ya PPP ili Taifa linufaike na njia hii ya utekelezaji wa miradi ambayo ina manufaa makubwa. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango iitische mjadala na wadau wa Sekta Binafsi ili kuangalia sababu za kukwama kwa utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP.

4.10 Sheria ya Bima kwa Wote

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuboresha huduma za Afya nchini ili huduma za afya ziwafikie wananchi wote.

NA KWA KUWA, changamoto kubwa iliyopo ni namna gani wananchi wanapata huduma hizo kwa gharama nafuu, ubora, haraka na uhakika.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Bima kwa wote *“Universal Coverage Health Insurance”*, katika Bunge la mwezi Aprili 2022 ili Sheria itakayotungwa ianze kutumika katika mwaka wa fedha 2022/23.

4.11 Utengaji wa Bajeti kwa ajili ya Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, sote tunatambua umuhimu wa sekta ya Kilimo katika utoaji wa ajira, maendeleo ya uchumi na utoshelevu wa chakula,

NA KWA KUWA, imekuwa ni kilio cha miaka mingi kwamba Serikali lazima iwekeze vya kutosha katika Sekta ya Kilimo ili kukabiliana na changamoto za utegemezi katika mvua, uhaba wa mbegu bora, upungufu wa pembejeo na zana za Kilimo, upatikanaji wa huduma za ugani pamoja na masoko ya mazao ya Kilimo.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Bajeti ya Maendeleo ya Kilimo iongezwe kutoka Shilingi Bilioni 294.1 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi **Shilingi Bilioni 500 kwa mwaka wa fedha 2022/23**. Ongezeko hilo likasaidie upatikanaji wa huduma za ugani, pembejeo za kilimo, mbegu, pembejeo na mbolea kwa bei nafuu. Pia, fedha hizo zikaboreshe huduma za umwagiliaji na ugani kwa maeneo yenye ukame.

4.12 Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji (Monitoring and Evaluation Act)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA kimekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Bunge kuomba Serikali kuandaa Sheria itakayosimamia masuala yote ya Tathmini na ufuatiliaji bila kuwa na mafanikio,

NA KWA KUWA, matatizo yanayohusu tahmini na ufuatiliaji bado yanaendelea kujitokeza katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Serikali na kuisababishia Serikali hasara kubwa kwa kutokuwa na mfumo thabiti wa tathmini na ufuatiliaji.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba katika nusu ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2022/23 lazima Serikali ilete muswada wa Sheria ya tathmini na ufuatiliaji na endapo haitafanya hivyo Basi Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Bajeti litaaandaa muswada na kuuwasilisha Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa ili kuwe na sheria.

4.13 Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA, mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki yanapitishwa na Bunge la Afrika Masharikii na yakisharidhiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nchi wanachama wanawajibika kutekeleza makubaliano hayo. Mapendekezo ya mabadiliko hayo yakishapitishwa yawezekana yakawa na madhara hasi kwa watanzania na wafanyabiashara wa Tanzania.

NA KWAKUWA, Bunge la Jamuhuri ya Mungano wa Tanzania huwa halipati fursa ya kuyapitia mabadiliko hayo na kuishauri Serikali kabla hayajaridhiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. **HIVYO BASI**, Bunge linashauri kwamba iwe ni lazima sasa kwa Serikali kulishirikisha Bunge ama Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Serikali kabla ya kuridhia mabadiliko hayo kabla hayajapitishwa na Bunge la Jumuiya ya Afrika Masharikia (EALA).

4.14 Kuhuisha Mfuko wa Jimbo uendane na Hali ya Uchumi wa Sasa

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA Viwango vinavyotumika kutoa fedha kwa Mfuko wa Jimbo vilipangwa miaka karibia 20 iliyopita na havijawahi kurejewa mpaka hivi sasa.

NA KWAKUWA Thamani ya Shilingi inaanguka kwa wastani wa asilimia 3 hadi 5 kila mwaka hivyo kupunguza uwezo wa fedha kununua bidhaa na huduma. Mfano mfuko wa Cement miaka 20 iliyopita ulikuwa kati ya **Shilingi 10,000 hadi 15,000** hivi sasa ni **Shilingi 18,000 hadi 25,000** hivyo ni wazi kwamba uwezo wa kufanya manunuzi wa fedha za Mfuko wa jimbo umepungua kwa takribani **asilimia 50**.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Serikali ifanya marejeo ya viwango vya fedha vya Mfuko wa jimbo ili viendane na hali ya sasa ya uchumi.

4.15 Uanzishwaji wa Ofisi ya Mpokeaji na Mshughulikiaji wa Malalamiko ya Kodi (Tax Ombudsman)

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA mwaka 2019 Bunge lako tukufu lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 (Tax Administration Act) yaliyokuwa na lengo la kuanzisha Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Kodi. Lengo la Ofisi hiyo ilikuwa ni kumshauri Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu malalamiko ya walipa kodi nchini.

NA KWAKUWA Imepita zaidi ya miaka mitatu Ofisi hiyo haijaanzishwa huku malalamiko ya walipa kodi yakiendelea kuongezeka bila kushughulikiwa kwa wakati.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba Ofisi hii ianzishwe kabla ya Mwezi wa 6 mwaka 2022 ili iweze kushughulikia malalamiko ya kodi ambayo ilianzishwa kwa ajili yake.

4.16 Daraja la Tanzanite Dar es Salaam na Barabara Unganishi

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA Daraja la Tanzanite Dar es Salaam lenye urefu **Km 1.03** na barabara unganishi **Km 5.2**. lililojengwa kwa gharama ya dola za Marekani **Million 107.4** sawa na **Shilingi Bilioni 243.8**.

NA KWAKUWA Daraja hilo ni mbadala wa Daraja la Sea lender la sasa ambalo lipo na linaweza kutumika kwa mtu ambae hatataka kulipa kwa ajili ya kupita daraja jipya la Tanzanite.

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba Serikali kuangalia uwezekano wa Daraja hilo kuwa la kulipia yaani Toll Bridge ili lisaidie kurejesha fedha za mkopo zilizotumiwa kujenda daraja hilo kama ambavyo inafanyika kwa Daraja la Kigamboni.

4.17 Stempu za Kodi za Kieletroniki (*Electronic Tax Stamp-ETS*)

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA tarehe 11 Mwezi 11 Mwaka 2021 Kamati ya Uongozi ilikaa na Serikali na kujadiliana kuhusu Umiliki, uendeshaji pamoja na gharama za Mfumo wa Kodi ya Stempu za Kieletroniki.

NA KWAKUWA katika kikao hicho maagizo kwa Serikali yalikuwa yafuatayo: -

i. Kutangaza zabuni ya kumpata mkandarasi atakaendesha mfumo wa ETS kwa Bei nafuu kuliko bei zilizopo hivi sasa; na

ii. Kulete Taaarifa kwa Kamati ya uongozi ni kwa namna gani Serikali inaweza kuendesha mfumo huo kwa sababu Wataalamu wa Kitanzania na Wamamlaka ya Mapato wana uwezo na ujuzi wa kutosha.

HIVYO BASI, Bunge linashauri mambo yafuatayo, Kwanza ni kuwasilisha mbele ya Kamati ya Uongozi ambayo uaniongoza wewe Mheshimiwa Spika, msingi wa Maamuzi ya Serikali kumuongezea Mkandarasi alieyepo Muda wa Mwaka mmoja na PILI ni kueleza namna ambayo Mamlaka ya Mapato imjipanga kuchukua na kuendesha mfumo huo badala ya kutafuta mkandarasi mwingine.

4.18 Kuwa na Kalenda ya Kufanya Ukaguzi wa Kodi kila mwaka (Tax Audit)

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA Mamlaka ya Mapato Tanzania ina utaratibu wa kukagua walipa kodi wake walau kila baada ya miaka mitatu na inapotokea kwamba mlipaji ana kosa basi huesabika kama ametenda kosa hilo miaka mitatu nyuma. Hali hii husababisha malimbikizo ya faini na adhabu kwa miaka mitatu na kusababisha madeni makubwa kwa walipa kodi.

NA KWAKUWA ukosefu wa watumishi kwa Mamlaka ya Mapato ndio unasababisha kuwa na ratiba ya kufanya ukaguzi wa mara moja kwa miaka mitatu.

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba Serikali lazima ijili watumishi wa kutosha kwa Mamlaka ya Mapato ili ukaguzi ufanyike kila mwaka badala ya miaka mitatu.

4.19 Mahitaji ya Fedha za Dharura kwa ajili ya Ukarabati wa Barabara vijijini zilizoharibika kwa Mvua Zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara vijijini.

Mheshimiwa Spika, KWAKUWA wakala wa barabara Vijijini TARURA amekamilisha Tathmini ya mahitaji ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya urejeshaji wa mawasiliano ya barabara vijijini.

NA KWAKUWA kiasi kinachohitajika ni **Shilingi bilioni 111.375** ambacho ni zaidi ya kiwango kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya matumizi ya dharura kwa **WAKALA**

HIVYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutenga katika Bajeti ya mwezi wa Pili walau Bilioni 60 na mwezi Machi **Bilioni 50** na kuzipeleka kwa Wakala wa Barabara vijijini ili kuwaondolea wananchi adha kubwa ya miundombinu ya barabara.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza kwanza wewe Mheshimiwa Spika Dkt Tulia Ackson kwa kuliendesha Bunge kwa weledi Mkubwa Vilevile nimpongeze Mussa Azzan Zungu Naibu Spika kwanza kwa kuteuliwa kwake na nimtakie kila la kheri katika majumu yake. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb Waziri wa Fedha na Mipango na aliyekuwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa Eng pamoja na Naibu Waziri wa Sasa Hamad Hassan Chande Mb. Hamad Yussuf Masauni, Mb kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao,

maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inasimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifautavyo: -

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb
4. Mhe. Issa Jummanne Mtemvu, Mb
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
6. Mhe. Josephati Sinkamba Kandege, Mb
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
9. Mhe. Shally Josepha Raymomd, Mb
10. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
11. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
12. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb
13. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb
14. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb
15. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb
16. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
17. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb
18. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb
19. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb
22. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb
23. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Maombi Kakozi na Ndg. Wilfred Akasi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliyoweza kufanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha

kwamba shughuli za Kamati zinafanyika kama zilivyokuwa zimepangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Daniel Baran Sillo, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
16 Februari, 2022

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma. *(Makofi)*

MHE. JERRY W. SILAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kufika siku ya leo. Kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka kwenye kitabu cha Kamati iingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe salamu za pongezi. Kwa niaba ya Kamati ya *PIC*, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Bunge letu Tukufu kuwa Spika wa Bunge hili. Aidha, naomba nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuchaguliwa na Bunge letu kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Kamati inaahidi kushirikiana nanyi katika

kuhakikisha kuwa Bunge linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (*PIC*) kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari, 2022 na kuiomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Umma yamefafanuliwa katika Kanuni 12 fasili ya (1) na ya (2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati pia imezingatia miongozo mingine mbalimbali kama inavyofafanuliwa kwenye ukurasa wa pili wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia zifuatazo: -

(i) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu uwekezaji unaotekelezwa na taasisi hizo;

(ii) Ziara za Ukaguzi katika baadhi ya Taasisi ya Umma ili kujiridhisha iwapo utekelezaji unaofanywa na taasisi hizo una tija; na

(iii) Semina za mafunzo kuhusu namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhtasari wa dosari zilizobainika katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Kabla ya kutoa maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, naomba kulidokeza Bunge lako Tukufu kwa muhtasari wa upungufu uliobainika katika utaratibu wa uwekezaji wa mitaji ya umma katika

kipindi hiki cha mwaka mmoja. Upungufu huo ni kama yalivyoonekana kwenye ukurasa wa tano na wa sita wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya *PIC* imeundwa ili kuwa jicho la Bunge katika kuangalia uwekezaji wa mitaji ya umma kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 12 fasili ya (1) na ya (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma umekuwa ukifanyika kwa njia mbalimbali zikiwemo uchambuzi wa taarifa za uwekezaji na ziara za ukaguzi wa miradi ya uwekezaji. Mambo ambayo Kamati imekuwa ikizingatia katika uchambuzi pamoja na kufanya uchambuzi wa viasharia mbalimbali vya kiutendaji wa taasisi kama uwiano wa mali kwa madeni, (*debtor asset ratio*), uwiano wa mapato kwa matumizi (*cost income ratio*), mtaji wa uendeshaji (*networking capital*), uwiano wa madeni ya muda mfupi na muda mrefu (*current ratio*), na kadhalika, kama yalivyoelezwa katika ukurasa wa saba na nane wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji uliofanywa na Kamati ulibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, Serikali ilifanya Uwekezaji katika jumla ya Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni 277 za ndani ya nchi na Taasisi 10 za nje ya nchi. Thamani ya Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika yao ulifikia jumla ya shilingi trilioni 67.06. Mchanganuo wa umiliki unaoneshwa katika jedwali Na.1 linalopatikana kwenye ukurasa wa tisa wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kamati imefanya uchambuzi thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma, pamoja na faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo (*Return on Investment*). Kwa kuangalia makundi makuu matatu ya Taasisi na Mashirika ya Umma kama yalivyogawanywa na Msajili wa Hazina ambapo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(i) Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, Serikali imewekeza jumla ya shilingi trilioni 9.7 na kupata faida ya shilingi bilioni 224 kwa Taasisi ya Mashirika ya Umma yanayofanya biashara, yanayotakiwa kutoa gawio na yanamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100;

(ii) Serikali iliwekeza jumla ya shilingi trilioni 2.6 na kupata faida ya shilingi bilioni 467.8 kwa Taasisi na Mashirika ya Umma yasiyofanya biashara pamoja na mamlaka za udhibiti ambazo zinatakiwa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na zinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100; na

(iii) Serikali iliwekeza shilingi bilioni 936.5 na faida yaani gawio ya shilingi bilioni 158.1 kwa tTaasisi ambazo zina umiliki wa hisa wa asilimia 50 na pungufu ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Serikali, gawio linachangia asilimia kubwa ikilinganishwa na vyanzo vingine. Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iendelee kufanya jitihada za makusudi katika kuzisimamia Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuboresha chanzo hiki cha mapato kwa maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imefanya uwekezaji katika mashirika 10 yaliyo nje ya nchi, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali katika mashirika hayo umefikia jumla ya shilingi bilioni 722.9. Orodha ya taasisi hizo pamoja na umiliki wa Serikali unaonekana katika Jedwali Na. 2, linalopatikana kwenye ukurasa wa 13 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa zilizowasilishwa za taasisi na mashirika ya umma ili kubaini iwapo dhumuni la Serikali kuwekeza katika taasisi na mashirika hayo linatimizwa. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitumia njia mbalimbali kama inavyoonekana kwenye ukurasa Na. 17 hadi 41 wa taarifa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ya Kamati. Kutokana na changamoto ya muda nizungumzie maeneo machache kama ifuatavyo: -

(a) Mashirika na taasisi za umma zinahitaji mtaji wa kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya kifedha, mashirika na taasisi nyingi zimeshindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji. Kamati imebaini changamoto hiyo ya upungufu wa mtaji katika Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*), Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (*TPDC*) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) kama taarifa ya Kamati inavyofafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini changamoto ya upungufu wa mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*), benki ilianza na mtaji wa shilingi bilioni 60 ingawa mtaji ulioidhinishwa (*authorized capital*) ni shilingi bilioni 800. Ili kukamilisha mtaji ulioidhinishwa, Serikali iliahidi kutoa katika bajeti yake ya kila mwaka kiasi cha shilingi bilioni 100.

Kamati inatambua juhudi kubwa za Serikali katika kuiwezesha benki kwa kuipatia kiasi cha shilingi bilioni 208 mnamo mwezi Desemba mwaka 2021. Kamati inapongeza juhudi za Serikali za kuiwezesha Benki ya *TADB*. Ni ushauri wa Kamati kuwa jitihadi za Serikali ziendee ili *TADB* iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

(b) Taasisi za Umma kutofanya kazi pamoja. Taasisi nyingi za umma zimekuwa zikifanya kazi kama nchi mbili zenye milengo tofauti. Hali hii limebainika kwa Taasisi za *STAMICO* na *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati majadiliano ya Kamati juu ya taarifa ya utendaji wa *STAMICO*, ilibaini changamoto ya kukosekana kwa umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo. Mgodi huu unaosimamiwa na Kampuni ya *STAMIGOLD* ambayo inamilikiwa na Shirika la Madini la Taifa *STAMICO* kwa 99%.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za uzalishaji katika mgodi huo zinategemea nishati ya umeme, lakini kutokana na kukosekana kwa umeme shirika linalazimika kutumia nishati ya mafuta ya dizeli ili kuendesha shughuli za uzalishaji. Mgodi unatumia kiasi cha mafuta kisichopungua lita 600,000 kwa mwezi, kwa bei ya wastani ya shilingi 2,500/= kwa lita. Inatumika shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli kila mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya umeme ya shirika kwa mwezi ni wastani wa *Unit* 1,300,000 sawa na shilingi bilioni 337.5 pindi Shirika la Umeme *TANESCO* litakapokamilisha kuunganisha mgodi kwenye gridi ya Taifa. Kwa muktadha huo, Kampuni ya *STAMIGOLD* itaokoa kiasi cha shilingi milioni 662 kwa mwezi kwa makisio ya chini ambayo ni sawa na shilingi bilioni nane kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa, iwapo changamoto ya kukosekana kwa umeme itatatuliwa, kupungua kwa gharama za uendeshaji wa *STAMIGOLD* kutaongeza faida kwa *STAMICO* na gawio kwa Serikali litaongezeka na mtaji wa kampuni utaimarika na mapato ya *TANESCO* yataongezeka kwa kuwa itakusanya shilingi bilioni 337.5 kwa kuuza umeme kwa *STAMICO*. Tatizo hili bado halijatatuliwa licha ya kuwa ni la muda mrefu na linapunguza mapato ya *STAMICO* pamoja na gawio katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(c) Katika uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji za Taasisi na Mashirika ya Umma, Kamati imebani kuwa imekuwa ni desturi baadhi ya Taasisi za Umma kutolipa madeni yake kwa wakati (*payables*) baada ya kupokea huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali na kusababisha ukuaji wa madeni hayo. Baadhi ya taasisi zilizobainika kuwa na changamoto hiyo ni pamoja na *DAWASA*, Kampuni ya Huduma za Meli, *GPSA*, *TEMESA*, *RUWASA*, *SIDO* na *EPZA*. Kutokana na changamoto ya muda, naomba nielezee upande wa Wakala wa Manunuzi Serikalini (*GPSA*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *GPSA* inadaiwa kiasi kikubwa cha fedha na madeni hayo yamekuwa yakiongezeka kutoka kiasi cha shilingi bilioni 50.3 mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni 84.8 mwaka wa fedha 2019/2020 sawa na ongezeko la 69%. Ongezeko hili linatokana na Wakala kuendelea kupokea fedha za wateja kwa ajili ya ununuzi wa magari huku ikichukua muda mrefu kuwapatia wateja magari hayo. Kamati inashauri Wakala kuharakisha mchakato wa utoaji wa huduma kwa wateja ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi ili kupunguza mzigo huo wa madeni. *(Makofi)*

(d) Kazi ya ufuatiliaji wa miradi ya uwekezaji inayofanywa na Kamati imebaini kuwa baadhi ya miradi ya uwekezaji inashindwa kutekelezwa kwa wakati kutokana na michakato mingi na muda mrefu unaochukuliwa na Serikali katika kufanya maamuzi pamoja na Serikali kutopeleka fedha za utekezaji wa miradi hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NDC* imepewa majukumu mazito ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati, lakini Serikali haijatilika mkazo katika uwekezaji kwa kuacha kupeleka fedha za kutekeleza miradi hiyo licha ya fedha hizo kuidhinishwa na Bunge. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 31.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya *NDC*. Hadi kufikia mwezi Juni, 2020, Serikali haijapeleka kiasi chochote cha fedha katika shirika hilo kwa ajili ya utekezaji wa miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, imebainika kuwa, baadhi ya miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na *NDC* inashindwa kutekelezwa kwa wakati kutokana na michakato mingi na muda mrefu unaochukuliwa na Serikali katika kufanya maamuzi. Mfano, mradi wa kimkakati wa Mchuchuma na Liganga ambapo umesimama kwa muda mrefu kutokana na timu ya Majadiliano ya Serikali *(GNT)* kuchelewa kukamilisha kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tatizo limeonekana pia katika mradi wa Kiwanda cha kuunganisha matrekta ya *Ursus* kinachosimamiwa na *NDC*, mkataba wa mradi huu

ulihusisha kuingiza matrekta 2,400, kujenga kiwanda cha kuunganisha matrekta na kujenga vituo nane vya kuhudumia matrekta. Mradi ulipaswa kuwa umekamilika kufikia Juni, 2018, lakini ni matrekta 822 tu yaliyopokelewa na hakuna kituo kilichojengwa mpaka sasa. *NDC* imeripoti kuwa majadiliano yanaendelea kati ya Serikali ya Tanzania na Poland kwa lengo la kuangalia njia sahihi ya kukwamua mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *NDC* ni shirika la kimkakati lililopewa jukumu kubwa la kuendeleza na kutekeleza miradi ya kiuchumi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Jitihada za makusudi zinapaswa kufanyika ili kulioko shirika hilo ili tuendele kupata faida ya ajira, ukuaji wa sekta ya viwanda na mchango wa Shirika katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, majadiliano yanaendelea kati ya Serikali ya Poland na Tanzania juu ya mradi wa matrekta yawekewe muda maalum wa kukamilika ili utekelezaji wa mradi huu uendele.

(e) Kamati imebaini mkwamo uliosababishwa Serikali kushindwa kutekeleza matakwa ya kimkataba kati yake na *NDC* ambalo linaendesha Kiwanda cha Viuwadudu cha Tanzania kilichopo Kibaha. *NDC* iliingia Mkatamba wa miaka mitano ya mauzo ya viwadudu na Wizara ya Afya ili kuwa na soko la uhakika la ndani. Hata hivyo, mkatamba huo haujatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kushindwa kutekeleza mkatamba huu kunasababisha kupungua kwa mapato ya shirika ambayo yangeongeza mchango wa *NDC* katika Mfuko wa Serikali.

(f) Bodi ya Wakurugenzi ndicho chombo kikuu cha maamuzi katika Taasisi na Mashirika ya Umma, lakini kuna ucheleweshaji wa kupata Bodi ambapo baadhi ya taasisi zimekuwa zikikaa kwa zaidi ya mwaka mzima bila kupata Bodi mpya jambo linalopelekea taasisi hizo kutokuwa na utendaji wa kuridhisha kwa kuwa hakuna usimamizi kwa niaba ya Serikali na pia hakuna chombo cha maamuzi.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mfano, Bodi ya *TIC* ambayo ilimaliza muda wake tangu Septemba, 2020 na bado haijaundwa mpaka sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, baadhi ya Bodi zina changamoto ya kimuundo ya Bodi za Wakurugenzi. Mfano, Bodi ya *EPZA* Wajumbe wake ni watendaji wa Serikali ambao wapo katika nafasi kubwa Serikalini ambapo Kamati imehofika upatikanaji wao kwa ajili ya vikao vya Bodi. Kamati inaishauri Serikali kufanya uteuzi wa Bodi pindi unapohitajika. Aidha, muda wa Wajumbe wa Bodi upishane ili kuwa mwendelezo (*succession plan*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kujiridhisha iwapo dhamira ya serikali kufanya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa, inatekelezwa kikamilifu na taasisi hizo na Serikali inapata faida stahiki kutokana na uwekezaji huo. Ni maoni ya Kamati kuwa:-

(i) Serikali iendeleo kuimarisha usimamizi wa mitaji yake, kubainisha na kuondoa changamoto zote za kifedha na kiutendaji ili bodi na menejimenti za taasisi zote za umma ziweze kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu. Kwa kufanya hivyo, Serikali itapata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wakati sahihi na kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni ya jumla ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa Mitaji ya Umma, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo: Mapendekezo ya Kamati yanapatikana ukurasa 47 hadi 55 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa mtaji katika taasisi za umma:-

Kwa kuwa, mashirika na taasisi za umma zinahitaji mtaji wa kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kufanya uwekezaji wenye tija;

Na kwa kuwa, baadhi ya mashirika na taasisi zimeshindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji kutokana na changamoto ya kifedha inayotokana na kukosekana kwa mtaji;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa, Serikali ihakikishe inaziwezesha taasisi zote zenye changamoto ya mtaji ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa wakati wa uanzishwaji wa taasisi hizo. Aidha, Serikali kupitia Msajili wa Hazina izishauri vema taasisi za umma na kuzisimamia katika kutumia fursa mbalimbali zilizopo na kukuza mitaji ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye viwanda na soko la hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa mtaji wa uendeshaji:-

Kwa kuwa, kumekuwa na taasisi na mashirika ya umma yenye mtaji hasi wa uendeshaji (*Negative Net Working Capital*) hasa kwa mashirika yanayojiendesha kibiashara;

Na kwa kuwa, kutokuwa kwa mtaji wa uendeshaji unaoridhisha kunazifanya taasisi na mashirika hayo kushindwa kutekeleza shughuli zake za msingi kwa wakati pamoja na kushindwa kulipa madeni yake bila ya kuathiri utendaji wake;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuhakikisha Bodi na Menejimenti za Taasisi za Umma zinasimamiwa kwa karibu na kuzitaka kuwa na utendaji wenye ufanisi na tija ili taasisi hizo ziwe na mtaji chanya wa uendeshaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za umma kutofanya kazi pamoja:-

Kwa kuwa, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya taasisi za umma kushindwa kusikilizana na kufanya kazi pamoja kwa maslahi mapana ya nchi;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Na kwa kuwa, kukosekana kwa ushirikiano katika utekelezaji wa baadhi ya miradi kunakwamisha utendaji wa taasisi nyingine na kuongeza gharama za uendeshaji, jambo hili limetokana na *TANESCO* kushindwa kupeleka umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo unaosimamiwa na *STAMIGOLD* ambayo inamilikiwa *STAMICO*;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuhakikisha kila taasisi inatekeleza wajibu wake kwa wakati na kwa ufanisi ili kurahisisha utekelezaji wa miradi au majukumu ya taasisi nyingine. Vile vile, Serikali ihakikishe *TANESCO* inaharakisha upelekaji wa umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo pamoja na miradi mingine ya kimkakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji:-

Kwa kuwa, imekuwa ni desturi kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kukiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na. 16 ya 2015 ya kutozidi ukomo wa gharama za uendeshaji wa 60%;

Na kwa kuwa, ukikukwaji wa matakwa ya sheria hiyo kumesababisha taasisi hizo kushindwa kuzalisha faida na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa, Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ihakikishe inazisimamia kwa karibu zaidi kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo na kuchukua hatua stahiki taasisi zote zinazozidisha matumizi yasiyoendana na uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kushindwa kukusanya Madeni (*Receivables*):-

Kwa kuwa, imekuwa ni changamoto kubwa kwa taasisi na mashirika ya umma kutokuwa na mikakati madhubuti wa ukusanyaji wa madeni pamoja na kuwa na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

uwezo mdogo wa kukusanya madeni yake baada ya kutoa huduma au kufanya biashara na taasisi nyingine;

Na kwa kuwa, tatizo hili siyo kiashiria kizuri katika utendaji wa taasisi hizo kwa kuwa kunapunguza mapato ya taasisi pamoja na kupunguza uwezo wake wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ihakikishe taasisi zote za umma zinakuwa na mkakati madhubuti wa ukusanyaji wa madeni yake ili kuongeza mapato yake na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa madeni (*payables*):-

Kwa kuwa, imekuwa ni desturi kwa baadhi ya taasisi za umma kutolipa madeni yake kwa wakati (*payables*), baada ya kupokea huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali na kusababisha ukuaji wa madeni hayo;

Na kwa kuwa, hali hii inatishia ukuaji wa mtaji wa taasisi kwa kuwa taasisi hizo zinaweza zikatengeneza hasara kutokana na fedha nyingi kutumika katika ulipaji wa madeni yakiwa pamoja na riba;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina:-

(a) Kuzikutanisha Taasisi zote za Serikali zinazodaiana ili kumaliza madeni yao na kuhakikisha madeni yote kutoka sekta binafsi yanalipwa; (*Makofi*)

(b) Kuandaa miongozo itakayozielekeza taasisi zote za umma kulipia huduma inazozipata kutoka katika taasisi nyingine kwa wakati; na

(c) Serikali ilipe madeni yake yote inayodaiwa na taasisi zake za umma. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi kutokuwa na mtazamo wa kibiashara:-

Kwa kuwa, imekuwa ni changamoto kubwa kwa taasisi za umma zinazofanya biashara, kushindwa kuwa shindani katika soko kutokana na kutokuwa na mtazamo wa kibiashara, kwa kukosa mbinu za kisasa za kibiashara;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa mtazamo wa kibiashara kwa kiasi kikubwa kunazifanya taasisi hizo kushindwa kuzalisha mapato ya kutosha na kushindwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa, Serikali kuhakikisha taasisi zote zinazofanya biashara zinakuwa na mikakati ya kibiashara pamoja na kuzalisha mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi kutokamilika kwa wakati:-

Kwa kuwa, miradi mingi ya uwekezaji inashindwa kukamilika kwa wakati kutokana na wingi wa michakato, Serikali kuchukua muda mrefu katika kufanya maamuzi, umakini wa Serikali katika kupata wawekezaji sahihi, pamoja na kutopeleka fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati;

Na kwa kuwa, kushindwa kutekelezeka kwa miradi hiyo kwa wakati kunaongeza gharama za uwekezaji hali inayoondoa tija ya uwekezaji huo pamoja na kuchelewa kupatikana kwa faida ya uwekezaji huo kama ilivyotokea katika miradi ya Liganga na Mchuchuma na mradi wa Matrekta ya *Ursus* inayotekelezwa na *NDC*;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa Serikali:-

(a) Wizara ya Fedha na Mipango inapeleka fedha za utekelezaji wa miradi yote kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

(b) Serikali iharakishe mchakato wa kupitia mkataba wa mradi wa mchuchuma na liganga ambao utekelezaji wake umekwama kwa muda mrefu, kutokana na kuendelea kwa majadiliano katika Kamati ya Majadiliano ya Serikali (*GNT*). Suala hili litafutiwe ufumbuzi au kuamua kuachana na Mbia aliyepo na kutafuta mwekezaji mwingine. (*Makofi*)

(c) Kabla Serikali haijaingia mkataba na mwekezaji yeyote ijiridhishe juu ya uwezo, ufanisi na tija itakayopatikana kutokana na mradi husika, ili kuepuka changamoto kama tulizokabiliana nazo katika miradi mbalimbali mfano mradi wa matrekta ya *Ursus*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhaba wa watumishi na vitendea kazi.

Kwa kuwa, baadhi ya taasisi za umma zimekuwa na changamoto ya uhaba wa watumishi na vitendea kazi kwa muda mrefu;

Na kwa kuwa, kutokamilika kwa lkama ya watumishi na kukosekana vitendea kazi muhimu inasababisha taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kufanya kazi chini ya kiwango,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina, Bodi za Wakurugenzi za Taasisi hizo kuhakikisha tatizo la upungufu wa watumishi na vifaa, linafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kukiuka matakwa ya kimkataba.

Kwa kuwa, Serikali imeshindwa kutekeleza makubaliano yake kimkataba iliyoingia na *NDC* kuhusu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mauzo ya viiadudu kwa muda wa miaka mitano *Bio larvicides offtake agreement* na Wizara ya Afya uliosainiwa tarehe 11 Machi, 2015 kuwa na uhakika wa soko la ndani,

Na kwa kuwa, kushindwa kutekelezwa kwa mkataba huo kumesababisha kupungua kwa mapato ya Shirika, fedha ambazo zingeongeza uwezo wa *NDC* kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na kuzalisha viaadudu kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa Serikali kuhakikisha:-

(a) Wizara ya Fedha na Mipango itenge fedha kwa ajili ya kuwezesha Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya *technical study* ya matumizi sahihi ya viaadudu na kushughulikia upatikanaji wa ithibati (*free qualification*) ya Shirika la Afya Duniani (*WHO*) kwa kiwanda cha viaadudu, ili kuwezesha Wizara ya Afya kutumia fedha zilizotolewa na wahisani katika ununuzi wa viaadudu vinavyozalishwa katika kiwanda hicho.

(b) Wizara ya Fedha na Mipango itenge fedha mahususi katika kifungu maalum *Ring-Fenced* kitakachotumika kulipia ununuzi wa viaadudu katika kiwanda cha Tanzania *Biotech Products*, ili kukiwezesha kiwanda hicho kupata soko la ndani na uhakika ikiwa ni pamoja na kuweza kurejesha mkopo uliotumika na Serikali katika ujenzi wa kiwanda hicho. *(Makofi)*

(c) Wizara ya Afya kuhakikisha inatenga fedha *own source* kwa ajili ya ununuzi wa viaadudu vinavyozalishwa katika kiwanda cha Tanzania *Biotech Product*, ikiwa ni pamoja na kuihuisha mkataba wake baina yake na *NDC* kuhusu ununuzi wa viaadudu. *(Makofi)*

(d) Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI ihakikishe inaziagiza na kuzisimamia halmashauri zake zote zenye uwezo wa kutenga bajeti ya ununuzi wa viaadudu, katika kiwanda cha Tanzania *Biotech*

kulingana na kiwango cha tatizo la malaria katika halmashauri zao. *(Makofi)*

(e) Kitengo cha biashara katika *NDC* kifanye kazi kutafuta masoko kwa kushirikiana na *TANTRADE*, ili dawa zinazozalishwa na katika kiwanda cha Tanzania *Biotech* zifahamike na kuuzika katika nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano usioridhisha wa gharama za uendeshaji kwa mapato.

Kwa kuwa, kumekuwepo na baadhi ya taasisi na mashirika ya umma...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa maliza maliza.

MHE. JERRY W. SILAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, inatumia kiasi kikubwa cha mapato kugharamia matumizi ya Taasisi.

Na kwa kuwa, kushindwa kudhibiti matumizi ya Taasisi hizo, kulingana na mapato yanayokusanya kumesababisha Taasisi hizo kutokuwa na bakaa kushindwa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Msajili wa Hazina izisimamie Taasisi zake na ihakikishe uwiano huu unaimarika na kutozidi ukomo wa asilimia 50, uliotolewa na Msajili wa Hazina ili Taasisi ziwe na fedha za kutosha kwa ajili ya uwezesaji wa shughuli zake na kuongeza mchango katika Mfuko huu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho.

NAIBU SPIKA: Toa hoja, toa hoja Mheshimiwa toa hoja.

MHE. JERRY W. SILAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI
YA UMMA (PIC) KWAKIPINDI CHA KUENZIA JANUARI, 2021
HADI FEBRUARI, 2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni
za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020)*

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niwasilishe salamu za pongezi kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) tunakupongeza kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Bunge letu Tukufu kuwa Spika wa Bunge hili. Aidha, nimpongeze pia Mheshimiwa Mussa Azan Zungu kwa kuchaguliwa na Bunge kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Kamati inaahidi kushirikiana nanyi katika kuhakikisha kuwa Bunge linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari, 2022 na kuliomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kujijadili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa.

1.1 *Majukumu ya Kamati*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 (1 & 2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ina majukumu yafuatayo: -

1) a) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

b) Kuchambua na kujadili Taarifa zinazohusu uwekezaji katika Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

2) Msingi wa kazi za Kamati utatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji katika Mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Kamati pia imefanya kazi zake kwa kuzingatia miongozo mingine kama ifuatayo: -

i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011;

iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001;

iv) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370;

v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992; na

vi) Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015

1.2 *Shughuli zilizotekelezwa*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao kwa kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu uwekezaji unaotekelezwa na Taasisi hizo. Aidha, Kamati imefanya ziara katika baadhi ya Taasisi za Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo una tija. Vile vile, Kamati ilipatiwa semina za mafunzo kuhusu namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati na mambo ya kuzingatia katika uchambuzi na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji wa mitaji ya Umma. Ufafanuzi kuhusu shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

a) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilipokea, ilichambua na ilijadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya umma yapatayo Kumi na Nane (18). Orodha ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

i) Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA);

ii) Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA);

iii) Wakala wa Umeme Vijijini (REA);

iv) Shirika La Maendeleo Ya Petroli Tanzania (TPDC);

v) Mamlaka Ya Udhibiti Wa Nishati Na Maji (EWURA);

vi) Mamlaka Ya Maji Safi Na Maji Taka Dar Es Salaam (DAWASA);

vii) Kampuni Ya Huduma Za Meli Tanzania (MARINE SERVICES);

viii) Shirika La Umeme Tanzania (TANESCO);

ix) Benki Ya Maendeleo Ya Kilimo Tanzania (TADB);

x) Shirika La Madini La Taifa (STAMICO);

xi) Shirika La Nyumba La Taifa (NHC);

xii) Shirika La Mawasiliano Tanzania (TTCL);

xiii) Shirika La Reli Tanzania (TRC);

xiv) Shirika La Taifa La Maendeleo (NDC);

xv) Wakala Wa Manunuzi Serikalini (GPSA);

- xvi) Mamlaka Ya Bandari Tanzania (TPA);
- xvii) Wakala Wa Ufundi Na Umeme Tanzania (TEMESA);
- xviii) Shirika La Uzalishaji Mali Jkt (SUMA JKT);
- xix) Bohari ya Madawa (MSD);
- xx) Wakala wa Misitu Tanzania (TFS);
- xxi) Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO);
- xxii) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF);
- xxiii) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF);
- xxiv) Mamlaka ya Eneo Maalumu la Uwekezaji (EPZA);na
- xxv) Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

b) Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Machi, 2021, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji inayotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya umma yaliyopo katika Jiji la Mwanza. Mantiki ya ukaguzi ni kuiwezesha Kamati kufanya tathmini ya ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo. Miradi iliyotembelewa na Ufafanuzi wake inaonekana katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii.

1.3 Muhtasari wa dosari zilizobainika katika uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya Umma, naomba kulidokeza Bunge lako tukufu kwa muhtasari wa mapungufu yaliyobainika katika utaratibu wa uwekezaji wa mitaji ya Umma katika kipindi hiki cha mwaka mmoja. Mapungufu hayo ni: -

i) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na mtaji wa kutosha hali inayosababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kisheria pamoja na kushindwa kufanya uwekezaji wenye tija;

ii) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma kushindwa kukamilisha miradi yake ya uwekezaji kutokana kushindwa kufanya maamuzi ya sahihi ya uwekezaji na kwa wakati;

iii) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma kushindwa kukamilisha miradi yake kutokana na Serikali kutopeleka fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu;

iv) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kushindwa kushirikiana katika kukuza uchumi wa Nchi kutokana na Taasisi moja ya Umma kukwamisha utekelezaji wa shughuli au miradi ya Taasisi nyingine ya umma;

v) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutolipia huduma wanazozipata kutoka katika Taasisi nyingine za Umma hali inayopunguza mapato ya Taasisi hizo na kukwamisha utendaji wa shughui zake za kila siku;

vi) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na madeni mengi ya muda mfupi zaidi ya mali za muda mfupi hali inayosababisha Taasisi hizo kushindwa kulipa madeni yote pindi inapohitajika kufanya hivyo na kuondoa imani ya watoa huduma wake;

vii) Baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamekuwa yakiendeshwa bila ya kuwa na Bodi ya Wakurugenzi licha ya kuwa Bodi ndicho chombo kikuu cha maamuzi. Aidha, muundo wa bodi za wakarugenzi kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma unaonekana kuwa na changamoto; na

viii) Baadhi ya taasisi na Mashirika ya Umma kutekeleza majukumu ambayo kwa namna moja ama nyingine yanashabihiana mfano TIRDO, CAMARTEC na TEMDO jambo linalopelekea kuongeza mzigo wa utegemezi wa ruzuku

kutoka Serikali, taasisi hizo zinawezekana zikaunganishwa na kuwa taasisi moja yenye idara kadhaa.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA NA MATOKEO YAKE

2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2021

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imelipa Bunge Mamlaka ya kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imeundwa ili kuwa jicho la Bunge katika kuangalia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 12(1 & 2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Ufuatiliaji wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma umekuwa ukifanyika kwa njia mbalimbali zikiwemo uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji. Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa kina kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu utendaji na uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuhakikisha kunakuwa na uwekezaji wenye tija na Taifa linanufaika. Uchambuzi wa Kamati hufanywa kwa kuangalia mambo ya msingi yafuatayo:-

- i. Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi;
- ii. Kufanya uchambuzi wa viashiria mbalimbali vya kiutendaji wa Taasisi kama uwiano wa Mali kwa Madeni, uwiano wa Mapato kwa Matumizi, Mtaji wa uendeshaji, Madeni ya Muda mfupi na muda Mrefu;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- iii. Utoaji wa Mitaji katika Taasisi za Umma;
- iv. Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali;
- v. Uzingatiaji wa nyaraka na miongozi mbalimbali ya kiutendaji kama Sera ya Uwekezaji, Mpango Mkakati, Mpango wa kibiashara, Sera ya Gawio;
- vi. Uteuzi na muundo wa Bodi za Wakurugenzi;
- vii. Utendaji kazi wa Bodi za Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi;
- viii. Kufanya mapitio ya miundo na mgawanyo wa majukumu;
- ix. Kuchambua Taarifa za uwekezaji wa Miradi;
- x. Kuangalia ufanisi wa Miradi ya Uwekezaji; na
- xi. Kuangalia ufanisi wa Taasisi na Mashirika ya Umma


Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022, uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji uliofanywa na Kamati ulibainisha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Serikali ilifanya Uwekezaji katika jumla ya Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni Mia Mbili Sabini na Saba (277) za ndani ya nchi na Taasisi Kumi (10) za nje ya nchi. Katika uwekezaji uliofanyika ndani ya Nchi, Serikali imewekeza katika jumla ya Taasisi na Mashirika **237** ambapo ina umiliki wa Hisa Asilimia 100 na Taasisi **40** ambapo ina umiliki wa Hisa pungufu ya Asilimia 51 na kufanya jumla ya Taasisi na Mashirika **277**. Jumla ya thamani ya uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika hayo kwa mwaka wa fedha 2020/21 ulifikia **Shilingi Trilioni 67.06 (67,068,301,722,882.10)** Mchanganuo wa umiliki unaoneshwa katika Jedwali Namba 1.

Jedwali Na. 1 Umiliki wa Hisa za Serikali

| NA | KIASI CHA UMILIKI KATIKA ASILIMIA (%) | IDADI YA TAASISI |
|------|---------------------------------------|------------------|
| 971. | 51-100 | 237 |
| 3. | 50 | 4 |
| 4. | Pungufu ya 50 | 36 |
| 5 | JUMLA | 277 |

Chanzo: Taarifa ya TR 2020/21

Picha halisi ya mchanganuo uliopo kwenye Jedwali Na. 01 inaonekana kupitia Chati Duara Na. 01 ya Taarifa hii.



Chati Duara Na. 01: Picha halisi ya Mchanganuo wa umiliki wa Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Msajili wa Hazina inayoishia tarehe 30 Juni, 2021, imebainisha kuwa, uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika **237** ambayo Serikali ina umiliki wa kuanzia Asilimia 51 mpaka 100 umefikia jumla ya **Shilingi Trilioni 66.27**. Vile vile, uwekezaji wa Serikali katika Makampuni 40 ambayo umiliki wake wa hisa ni Asilimia 50 na pungufu umefikia jumla ya **Shilingi Bilioni 959.36**.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Ofisi ya Msajili wa Hazina ni kukusanya mapato yasiyo ya kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali kama Gawio kutoka katika Mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chini ya Asilimia 51, Michango ya Asilimia 15 ya mapato ghafi kutoka katika Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika gazeti la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Asilimia 28 ya Mfuko wa kusimamia Mawasiliano ya simu (TTMS), Asilimia 70 ya ziada kutoka katika Mashirika ya Umma na rejesho la Riba na Mikopo iliyotolewa na Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Umma.

Hata hivyo, Serikali haipimi manufaa ya uwekezaji wake katika Taasisi hizo kwa kuangalia fedha taslimu zinazopatikana, na badala yake hupima manufaa yake kwa kuangalia huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi hizo kwa jamii. Kwa muktadha huo, baadhi ya Taasisi hususan za Elimu, Mifuko ya Hifadhi ya jamii, Afya, Kilimo na Utafiti hazitowi Gawio wala Mchango wa Asilimia 15 katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kamati imefanya uchambuzi wa kina juu ya thamani ya

| NA | KIASI CHA UMILIKI KATIKA ASILIMIA (%) | IDADI YA TAASISI |
|--------------|--|------------------|
| 971. | Uwekezaji huo (Return on Investment) kwa kuangalia makundi makuu matafu ya Taasisi na Mashirika ya Umma na | 250 |
| 3. | Makampuni ambayo Serikali ina hisa kama yaliivyogawanywa Punguru ya 50 | 30 |
| 5 | na Msajili wa Hazina. | 277 |
| JUMLA | | |

Mheshimiwa Spika, Kundi la kwanza ni Taasisi na Mashirika ya Umma yanayofanya biashara, yanatakiwa kutoa gawio na yanamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2021, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 9,780,390,355,239.25** na kupata faida ya **Shilingi 224,251,857,322.77** kutokana na uwekezaji huo. Aidha, Rejesho la Uwekezaji (Return on Investment) huo ni sawa na **Asilimia 2**.

Kundi la Pili ni Taasisi na Mashirika ya Umma yasiyofanya biashara pamoja na Mamlaka za Udhibiti ambazo zinatakiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na zinamilikiwa na Serikali kwa Asilimia 100 ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni,

2021, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 2,681,126,838,443.76** na kupata faida ya **Shilingi 467,889,055,169.56** Faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo (Return on Investment) ni sawa na **Asilimia 17**.

Kwa ujumla, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2021, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 12,461,517,193,683.00** katika Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo ina umiliki wa hisa Asilimia 100 na ambayo yanatakiwa kutoa gawio pamoja na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kupata faida ya **Shilingi 692,140,912,492.33** ambayo ni sawa na **Asilimia 6** ya rejesho la uwekezaji (Return on Investment).

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni uwekezaji wa Serikali katika Taasisi ambazo ina umiliki wa hisa Asilimia 50 na pungufu ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2021, uwekezaji uliofanywa na Serikali ulifikia jumla ya **Shilingi 936,554,203,874.76** na faida (gawio) ya **Shilingi 158,139,892,061.01** ilipatikana ambayo ni sawa na **Asilimia 17** (Return on Investment). Kimsingi Taasisi hizi zinatakiwa kutoa gawio kwa Serikali kulingana na kiwango cha uwekezaji wa Serikali katika Taasisi hizo.

Jumla ya uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa Taasisi zote 277 (zinazomilikiwa kwa Asilimia 100 na zile zenye Hisa Asilimia 50 na pungufu) ni **Shilingi Trilioni 67.23** na kupata faida ya **Shilingi Bilioni 850.28**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Serikali, Gawio linachangia asilimia kubwa ikilinganishwa na vyanzo vingine ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2021, Jumla ya **Shilingi Bilioni 637.66** zilikusanywa kupitia Akaunti ya Msajili wa Hazina kutoka katika vyanzo mbalimbali na **Shilingi Bilioni 212.62** ziliwasilishwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mchanganuo wa mapato yaliyopitia kwa Msajili wa Hazina ni kama ifuatavyo; -

i. Makusanyo yaliyotokana na Gawio yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 308.86 (48%)**;

ii. Michango ya Asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya Mashirika **Shilingi Bilioni 202.28 (32%)**;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- iii. Ziada na mapato mengineyo **Shilingi Bilioni 96.80 (15%)**,
- iv. Mawasilisho ya Mtambo wa TTMS **Shilingi Bilioni 10.38 (2%)**; na
- v. Marejesho ya Mikopo na Riba **Shilingi Bilioni 19.31 (3%)**.

Kutokana na mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa, Gawio limechangia Asilimia kubwa (48%) ya mapato yote ikifuatiwa na Michango ya asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya Mashirika. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufanya jitihada za makusudi katika kuzisimamia Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuboresha chanzo hiki muhimu cha mapato kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Taasisi na Mashirika yaliyopo ndani ya Nchi, Serikali pia imefanya uwekezaji katika Mashirika Kumi (10) yaliyo nje ya Nchi. Uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina umeonesha kuwa, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2021, thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika hayo umefikia jumla ya **Shilingi 722,946,454,573.16** Orodha ya Taasisi hizo pamoja na umiliki wa Serikali unaonekana katika jedwali Namba 2.


Jedwali Namba 2

| NA. | JINA LA TAASISI | UMILIKI WA SERIKALI |
|-----|--|---------------------|
| 1 | African Development Bank (ADB) | 0.76% |
| 2 | Shelter Afrique | 0.52% |
| 3 | East African Development Bank (EADB) | 24.98% |
| 4 | International Bank for Reconstruction and Development (IBRD) | 0.06% |
| 5 | International Development Association (IDA) | 0.26% |
| 6 | International Finance Corporation (IFC) | 0.04% |
| 7 | Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA) | 0.22% |
| 8 | PTA BANK (now Eastern and Southern African Trade and Development Bank (TDB)) | 8.36% |
| 9 | African Reinsurance Corporation (Africa Re) | 0.80% |
| 10 | African Trade Insurance Agency (ATI) | 8.37% |

Chanzo: *Taarifa ya TR 2020/21*

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma umeongezeka kwa **Asilimia 4** kutoka **Shilingi trilioni 64.45 mwaka 2019/20** hadi kufikia **Shilingi 67.06 mwaka 2020/21**. Aidha, Uwekezaji huo umefanyika kwa Taasisi 277 ambazo zimeandaa Taarifa za hesabu. Ongezeko la uwekezaji uliofanywa na Serikali umetokana na Sehemu kubwa ya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwasilisha Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa zinazotoa sura ya thamani halisi ya hisa na mitaji kwa sasa, Kuongezeka kwa hisa za baadhi ya Taasisi za kibiashara na mitaji ya baadhi ya Taasisi zisizo za kibiashara na ongezeko kubwa la fedha za hisa linalotokana na tathmini mpya ya hisa na mtaji. Mwenendo wa ukuaji wa uwekezaji kwa miaka Mitano umeoneshwa katika Chati Namba 1.

Mwenendo wa Ukuaji wa Uwekezaji wa Serikali




Aidha, mwenendo wa ukuaji wa uwekezaji wa mitaji na faida kwa miaka Mitano umeoneshwa katika Mchoro (Graph) Namba 1.

Mchoro (Graph) Na. 01: Sura ya ongezeko la thamani ya uwekezaji na faida kwa mwaka 2016/17, 2017/18, 2018/19, 2019/20 na 2020/21

2.2 Uchambuzi wa Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kifungu (2) cha Sheria ya



Aidha, na Serikali

mbalimbali kama Mapato yasiyo ya Kodi (Gawio na Mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali), Upatikanaji wa Huduma bora za Afya, Elimu, Maji, Nishati na Miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa zilizowasilishwa za Taasisi na Mashirika ya Umma ili kubaini iwapo dhumuni la Serikali kuwekeza katika Taasisi na Mashirika hayo linatimizwa ikiwa ni pamoja na kuangalia ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitumia njia zifuatazo: -

- i) Kupitia Taarifa za Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika na Taasisi za umma zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya Umma;
- ii) Kupitia Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji umezingatia Taratibu, Sheria na Miongozo mujarabu ya biashara;
- iii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu uchambuzi wa utendaji na uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kupokea maoni ya Msimamizi wa Taasisi na Mashirika yanayofanya uwekezaji wa mitaji ya umma; na
- iv) Kufanya mahojiano na Wenyevidi wa Bodi na Menejimenti za Taasisi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia njia hizo, Kamati ilifuatilia uwekezaji huo wa mitaji ya umma kwa kufanya uchambuzi na kubaini mambo makuu yafuatayo: -

- i) Upungufu wa Mtaji katika Taasisi za Umma;
- ii) Kupungua kwa Mtaji wa Uendeshaji;
- iii) Taasisi za Umma kutofanya kazi pamoja;
- iv) Kuongezeka kwa Gharama za Uendeshaji;
- v) Kushindwa kukusanya Madeni (Receivables);
- vi) Kuongezeka kwa Madeni (Payables);
- vii) Taasisi kutokuwa na Mtazamo wa Kibiashara;

- viii) Uwiano Usioridhisha wa Mali kwa Madeni ya Muda Mfupi;
- ix) Miradi kutokamilika kwa Wakati;
- x) Uhaba wa Watumishi na Vitendea kazi;
- xi) Serikali kukiuka Matakwa ya Kimkataba;
- xii) Uwiano Usioridhisha wa Gharama za uendeshaji kwa Mapato;
- xiii) Uwiano usioridhisha wa faida kwa Mali;
- xiv) Uwezo wa ukusanyaji wa mapato; na
- xv) Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi.

2.2.1 Upungufu wa Mtaji katika Taasisi za Umma

Mheshimiwa Spika, Mashirika na Taasisi za Umma zinahitaji mtaji wa kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya kifedha, Mashirika na Taasisi nyingi zimeshindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji. Kamati imebaini changamoto hiyo ya upungufu wa mtaji katika Shirika la Mawasiliano Tanzania, (TTCL), Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) ni Shirika la kibiashara hivyo linatakiwa kuwa na mtaji wa kutosha kwa ajili ya kufanya uwekezaji wenye tija na kulifanya Shirika liweze kushindana na Makampuni mengine yaliyo sokoni. Ukosefu wa Mtaji umelifanya Shirika kutofikia malengo ya Mpango Mkakati wa miaka mitano (2016 – 2021) kutokana na uwekezaji hafifu hasa kwenye huduma za simu za mkononi, uchakavu wa mitambo, na matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati. Vile vile, Shirika lipo katika hatari kubwa zaidi ya kunyang'anywa soko kutokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na kampuni nyingine za simu hapa

nchini hasa Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel. Ili TTCL iweze kufanya uwekezaji mkubwa (*full capacity*) inatakiwa na mtaji wa **Dola za Kimarekani Milioni 752**. Hata hivyo, Mpaka sasa TTCL ina Mtaji wa **Shilingi Bilioni 370.465** tu. Serikali iangalie namna bora zaidi ya kuongeza mtaji wa Shirika hili kwa kuwapatia kiasi cha **Shilingi Bilioni 360.09** kilichoombwa na Shirika kwa sasa ili Shirika liweze kufanya uwekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, Mtaji wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) umeendelea kuwa hasi ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/20, mtaji huo uliongezeka kutoka **mtaji hasi wa Shilingi Bilioni 354.8** mwaka 2018/19 hadi **mtaji hasi wa Shilingi Bilioni 331.2** mwaka wa fedha 2019/20 ambapo ni ongezeko la asilimia 6.7.

Licha ya ukweli kwamba, mtaji wa TPDC umeendelea kuwa hasi kutokana na hasara iliyopatikana katika mwaka wa fedha 2014/15 ambayo ilisababishwa na mkopo wa **Dola za Kimarekani Bilioni 1.194** zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Mkopo huo ulilingizwa kwenye hesabu za Shirika na hivyo kusababisha Shirika kupata hasara ya **Shilingi Bilioni 257.2** iliyotokana na matumizi ya gharama za riba na mikopo (interest expense) na hasara ya kubadilisha fedha (exchange loss) kutokana na mkopo husika. Kwa kiasi kikubwa mkopo huu ndiyo umesababisha mtaji wa Shirika kuwa hasi pamoja na faida ambayo Shirika limekuwa likipata katika mwaka wa fedha 2019/20 na 2018/19.

Mheshimiwa Spika, Shughuli zinazotekelezwa na TPDC ni muhimu sana kwa utekelezaji wa Dira yetu ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Katika kipindi ambacho Nchi ipo katika Uchumi wa Kati, nishati zitokanazo na mafuta na Gesi Asilia ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda hapa nchini na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Hivyo, Serikali iwekeze mtaji wa kutosha kwenye shughuli za utafutaji, usafishaji, usafirishaji na usambazaji wa gesi ili Taifa liendelee kunufaika na rasimali hizi ili uchumi wa nchi uendelee kuimarika.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kutatua changamoto hii kwa TPDC, Kamati inasisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa kugeuza mkopo huo kuwa mtaji wa Shirika kwa kuwa mpango huo utaleta manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na; Shirika kuongeza Mtaji kwa ajili ya uwekezaji katika miradi ya kimkakati; Hali ya kifedha ya Shirika itaimarika na kuwezesha Shirika kupata faida itakayoivezesha kulipa kodi ya mapato ya Kampuni (Corporate Income tax); Serikali itanufaika kwa ongezeko la malipo ya Gawio; na Kuimarika kwa Mtaji wa Shirika kutavutia wawekezaji kuwekeza katika miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini changamoto ya upungufu wa mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Benki ilianza na mtaji wa **Shilingi Bilioni 60** ingawa mtaji ulioidhinishwa (Authorized Capital) ni **Shilingi Bilioni 800**. Ili kukamilisha mtaji ulioidhinishwa, Serikali iliahidi kutoa katika Bajeti yake ya kila mwaka kiasi cha Shilingi Bilioni 100. Kamati inatambua juhudi mbalimbali za Serikali katika kuiwezesha Benki hii kwa kuipatia kiasi cha Shilingi **Bilioni 208**, mnamo Mwezi Disemba 2021. Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kuiwezesha TADB, ni ushauri wa Kamati kuwa jitihada za Serikali ziendeele ili TADB iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

2.2.2 Kupungua kwa Mtaji wa Uendeshaji

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yanatakiwa kuwa na mtaji wa uendeshaji (working capital) ambao utazisaidia Taasisi hizo kutekeleza shughuli zake za msingi kwa wakati na ulipaji wa madeni kufanyika bila kuathiri utendaji wake. Hata hivyo, hali hii imekuwa tofauti kwa baadhi ya Mashirika yaliyowasilisha taarifa zake mbele ya Kamati ambapo yameonekana kuwa na mtaji hasi wa uendeshaji (Negative Net working capital). Mfano wa Mashirika hayo ni TANESCO, NDC na EPZA.

Taarifa za kifedha za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) za Mwaka 2019/20 zimebainisha kuwa, Shirika lina Mtaji Hasi wa uendeshaji (Negative Working Capital) wa **Shilingi Trilioni**

1.33. Shirika kuwa na Mtaji Hasi kumetokana na mali za muda mfupi za Shirika za kiasi cha **Shilingi Trilioni 1.45** kushindwa kulipa madeni ya muda mfupi ya kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.78**. Uwezekano wa hali hii kuendelea ni mkubwa sana kutokana na utendaji wa Shirika kuwa na madeni mengi ya haraka (current liabilities) ikilinganishwa na mali zilizopo. Kamati inashauri Shirika kuwa na Mpango wa Biashara ambao utaainisha kiasi cha Mtaji kinachohitajika.

Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) limekuwa na mtaji Hasi wa uendeshaji hali inayotishia kuondoa ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa kuwa shughuli za uwekezaji kwa kiasi kikubwa zinahitaji uwepo wa mtaji wa kutosha. Pamoja na vigezo vingine, ufanisi wa Shirika unatokana na kuwa na mtaji Chanya wa uendeshaji. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo 2017/2018 hadi 2019/2020, NDC imekuwa na mtaji Hasi wa uendeshaji wa **Shilingi Bilioni 23.70**, **Shilingi Bilioni 20.0** na **Shilingi Bilioni 14.8** Mtawalia. Hali hii haileti picha nzuri ya kiutendaji katika Shirika na sio kiashiria kizuri cha uwekezaji wenye tija.

Vile vile, uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa mtaji wa Mamlaka ya EPZA umeshuka kwa **asilimia 14** katika kipindi cha miaka miwili ambapo kwa mwaka 2018/2019 mtaji wa EPZA ilikuwa shilingi **bilioni 158** na mwaka 2019/2020 ulishuka hadi kufikia **bilioni 152**. Kushuka kwa Mtaji kumetokana na mamlaka kuendelea kupata nakisi. Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kupunguza matumizi hususani yasio ya lazima ili kupunguza malimbikizo ya nakisi ambayo inadhofofisha mtaji wa Mamlaka.

2.2.3 Taasisi za Umma kutofanya kazi pamoja

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi za Umma zimekuwa zikifanya kazi kama Nchi mbili zenye milengo tofauti. Hali hii imebainika na kamati baada ya kuona Taasisi nyingi za Umma hazifanyi kazi kwa kushirikiana licha ya dhamira za Taasisi zote ni kujenga uchumi imara wa Tanzania. Kumekuwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa ushirikiano katika baadhi ya utekelezaji wa miradi hasa inapotokea kukamilika

kwa mradi wa Taasisi moja kunategemea kwa kiasi kikubwa utendaji kazi wa Taasisi nyingine. Tatizo hilo limebainika kwa Taasisi za STAMICO na TANESCO wakati Kamati inachambua taarifa za STAMICO.

Kamati ilipokea Taarifa ya uchambuzi wa Msajili wa Hazina pamoja na maelezo ya uongozi wa STAMICO kuhusu tija ya mitaji ya Umma iliyowekezwa katika Shirika hilo. Wakati wa majadiliano Kamati ilibaini changamoto kubwa ya kukosekana kwa umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo. Mgodi huu unasimamiwa na Kampuni ya STAMIGOLD ambayo inamilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa Asilimia 99.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za uzalishaji katika mgodi huo ambazo ni uendeshaji mitambo na vifaa vya uchimbaji (mining equipment) pamoja na uchenjuaji (processing) zinategemea kwa kiasi kikubwa nishati ya umeme, lakini kutokana na kukosekana kwa umeme Shirika linalazimika kutumia nishati ya mafuta ya dizeli. Ili kuendesha shughuli za uzalishaji (uchimbaji na uchenjuaji), Shirika linatumia kiasi cha mafuta kisichopungua **lita 600,000 kila mwezi**, ambapo mahitaji kwa ajili ya ufuaji umeme pekee ni takribani **lita 360,000**. Kwa bei ya wastani wa Shilingi 2,500 kwa litera, mgodi huitaji kiasi cha **shilingi Bilioni 1.5** kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli kila mwezi.

Mahitaji ya umeme ya Shirika kwa mwezi ni wastani wa **Unit 1,368,194** sawa na **Shilingi 337,571,836.94** pindi Shirika la Umeme (TANESCO) litakapokamilisha kuunganisha mgodi kwenye Gridi ya Taifa. Kwa muktadha huo, Kampuni ya STAMIGOLD itaokoa kiasi cha **Shilingi Milioni 662 kwa mwezi** (kwa makisio ya chini) ambayo ni sawa na **Shilingi Bilioni 8 kwa mwaka**.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa gharama za uendeshaji wa STAMIGOLD kutaongeza faida ya kampuni ambayo itaongeza faida kwa Kampuni mama ya STAMICO, faida hiyo itaongeza gawio kwa Serikali. Katika mwaka wa Fedha 2019/20 Shirika limeweza kuwasilisha gawio kiasi cha Shilingi Bilioni

1.1 kufuatia kutengeneza faida. Kamati inaamini kuwa, iwapo changamoto ya kukosekana kwa umeme itatatuliwa kiasi cha gawio kitakachotolewa na STAMICO kwa Serikali kitaongezeka na kutaimarisha Mtaji wa Kampuni. Vile, vile, kupatikana kwa umeme katika mgodi huo, kutaongeza mapato kwa TANESCO kwakuwa litakuwa na uwezo kwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 337,571,836.94** kwa kuuza umeme kwa STAMICO.

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika uunganishaji wa mgodi katika gridi ya Taifa, bado tatizo hili halijamalizwa na Serikali licha ya kuwa ni la muda mrefu na linapunguza mapato ya STAMICO pamoja na Gawio katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

2.2.4 Kuongezeka kwa Gharama za Uendeshaji

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikipima kiasi cha mapato kinachotumika kugharamia gharama za uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma. Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (A)(1) imeweka ukomo wa gharama za uendeshaji kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kutozidi Asilimia 60 ili Taasisi hizo ziweze kuzalisha faida na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya Taasisi ambazo zimekuwa zikishindwa kukidhi matakwa hayo mfano, STAMICO, GPSA, TEMESA, SUMA JKT, MSD na EPZA.

Taarifa za kifedha za Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) limebainisha kuwa, Uwiano wa gharama za uendeshaji wa Shirika (Operating Expenses) kwa mapato yatokanayo na shughuli za Shirika (Operating Revenue) umefikia Asilimia 71 mwaka 2019/20. Pamoja uwiano huo kuimarika kutoka Asilimia 107 kwa Mwaka 2018/19, bado matumizi ya Shirika yako juu ya ukomo uliowekwa wa Asilimia 60 uliowekwa na Msajili wa Hazina. Kamati inashauri Shirika kupunguza gharama za uendeshaji ili kuimarisha uwiano huo.

Kamati imechambua mwenendo wa mapato na matumizi ya Wakala wa manunuzi Serikalini (GPSA) na kubaini ongezeko kubwa la matumizi kutoka **Shilingi Bilioni 10.632**

mwaka 2018/2019 hadi **Shilingi Bilioni 14.014** mwaka 2019/2020, ongezeko hilo na sawa na **Asilimia 32**. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa gharama za matengenezo kwa **Asilimia 132**, gharama za kiutawala na ofisi kwa Asilimia 30 na gharama za uchakavu wa mali kwa Asilimia 21. Kamati inashauri Wakala idhibiti matumizi yake ili kuongeza kiasi cha faida.

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua taarifa za kifedha za Wakala Ufundi na umeme (TEMESA) na kubaini uwepo wa ongezeko la matumizi ambapo, matumizi ya TEMESA yameongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 52.34** mwaka 2018/19 hadi **Shilingi Bilioni 66.99** mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la Asilimia 27.98. Hali hii haileti picha nzuri ya utendaji wa Taasisi.

Vile vile, Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati zimebainisha kuwa, matumizi ya Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMA JKT) ni pamoja na gharama za watoa huduma na vifaa, mishahara, mafao ya watumishi, gharama za matengenezo, gharama za uchakavu na matumizi mengineyo. Aidha, uchambuzi wa kamati umebaini ongezeko la matumizi kwa Asilimia 31.1 ambapo mwaka 2019/20 matumizi yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 138.177** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi Bilioni 105.433** mwaka 2018/19. Kamati inashauri Shirika kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ili kuwa na faida na kuongeza kiasi cha gawio Serikalini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bohari ya Madawa (MSD) imekuwa na uwiano wa asilimia 91 wa gharama za uendeshaji kwa mapato. Uwiano huu sio mzuri kwani uko juu ya kiwango cha asilimia 60 kilichowekwa na Msajili wa Hazina na unaashiria kwamba matumizi ya shirika ukilinganisha na mapato uko juu ya uwiano uliowekwa. Kamati inaishauri Shirika kufanya jitihada za kupunguza matumizi ya uendeshaji hususani ya matumizi ya utawala na matumizi mengineyo yasiyo ya lazima ili kuyafanya yawe ndani ya kiwango kilichowekwa na kuweza kutengeneza faida itakayopelekea kuongezekwa kwa mchango wa MSD katika mfuko wa Serikali.

Taarifa za kifedha za Mamlaka ya EPZ imebainisha kuwa kiasi cha mapato kinachotumika kugharamia gharama za uendeshaji zilifika **asilimia 96** katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kiwango hichi kiko juu ya kiwango kilichowekwa na Msajili wa Hazina ambacho ni **asilimia 60**. Kamati inaishauri EPZA kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, jambo hili liende sambamba na kuandaa mkakati wa kuhamasisha sekta binafsi pamoja na mifuko ya hifadhi za jamii kuwekeza katika maeneo ya EPZA.

2.2.5 Kushindwa kukusanya Madeni (Receivables)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni pamoja na kuwa na uwezo mdogo wa kukusanya madeni yake baada ya kutoa huduma au kufanya biashara na Taasisi nyingine. Tatizo hili si kiashiria kizuri katika utendaji wa Taasisi hizo kwa kuwa kinapunguza mapato ya Taasisi hizo pamoja na kupunguza uwezo wake wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Uchambuzi wa kifedha wa Kamati umebaini tatizo hilo katika Taasisi nyingi zilizowasilisha taarifa zake mfano DAWASA, TANESCO, NHC, GPSA, TEMESA, SUMA JKT, MSD, SIDO na PSSSF.

Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) inakabiliwa na changamoto ya wateja wao kushindwa kulipa madeni yao yanayotokana na kupata huduma ya maji. Tatizo hilo linapunguza mapato ya Mamlaka na kukwamisha baadhi ya shughuli kutokana na kukosekana kwa fedha. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 malimbikizo ya madeni yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 422**. Kamati inashauri kuandaliwa kwa mkakati wa kukusanya fedha hizo ili kuongeza mapato ya Mamlaka.

Kwa upande wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Kamati imebaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 June 2020, Shirika lilikuwa linadai Taasisi za Serikali na watu binafsi jumla ya **Shilingi Bilioni 422.37**, kati ya deni hili **Shilingi Bilioni 238.06** zinadaiwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali na **Shilingi Bilioni 184.31** ni deni kwa watu na Kampuni binafsi. Kiwango

hiki ni kikubwa sana na Shirika linapaswa kuja na mkakati wa haraka unaotekelezeka wa ukusanyaji wa madeni haya. Hii itasaidia Shirika kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake za msingi kwa wakati.

Vile vile, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 June 2020, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lilikuwa linadai Taasisi za Serikali na watu binafsi jumla ya **Shilingi Bilioni 38.28**, kati ya deni hili **Shilingi Bilioni 5.3** zinadaiwa Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali na **Shilingi Bilioni 32.9** ni deni kwa watu na kampuni binafsi. Kiwango hiki ni kikubwa sana hivyo Kamati inashauri Shirika kuja na mkakati wa haraka na unaotekelezeka wa ukusanyaji wa madeni haya.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Manunuzi Serikalini (GPSA) imekuwa na ongezeko la madai (receivables) ambayo yanatokana na kutoa huduma mbalimbali kwa Taasisi mbalimbali kama ugomboaji wa mizigo na upangishaji wa maghala. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 madai hayo yaliongezeka na kufikia kiasi cha **Shilingi Bilioni 5** kutoka **Shilingi Bilioni 3** mwaka 2018/2019. Hali hiyo inapunguza mapato ya Taasisi kwa kiasi kikubwa kwakuwa fedha nyingi zipo nje ya mfumo wa Taasisi. Kamati inashauri Wakala kuwa na mkakati madhubuti wa ukusanyaji wa mapato yake.

Aidha, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ina majukumu mbalimbali ikiwemo Kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na Mitambo ya Serikali katika karakana ambazo zipo kila Mkoa, kufanya matengenezo na Usimikaji wa mifumo ya Umeme, Viyoyozi na Electroniki inayomilikiwa na Serikali. Taarifa zilizochambuliwa na Kamati zimebainisha kuwa, hadi kufikia Juni, 2020 Wakala ulikuwa unazidai Wizara na Taasisi za Serikali Jumla ya **Shilingi 38,779,777,535**

Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMA JKT) hutoa huduma ya ulinzi na huduma katika sekta ya ujenzi katika Taasisi mbalimbali, taarifa zilizowasilishwa zimebainisha uwepo wa madeni makubwa katika maeneo hayo ambayo Shirika linadai. Hadi kufika Septemba, 2021 sekta ya Ujenzi inadai **Shilingi 12,713,238,060.00** na Kampuni ya Ulinzi Binafsi inadai **Shilingi**

17,816,326,053.60, fedha hizi bado hazijakusanywa na zinapunguza mapato ya Shirika.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Bohari ya Madawa (MSD) inadai Taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya Shilingi **Bilioni 269.13**. Kamati inalishauri Shirika kuweka mkakati mahususi wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa, madeni haya yamekuwa mzigo kwao na yamepunguza Ukwasi wa Shirika katika kutekeleza majukumu yake msingi ipasavyo.

Vile vile, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limekosa mipango madhubuti ya ukusanyaji wa madeni jambo lililopelekea kupata hasara ya **Shilingi bilioni 2.05** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ya **bilioni 1.56**, hasara ya **Bilioni 2.05** kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na kuchelewesha kwa ulipwaji wa madeni. Kamati inalishauri Shirika kuadhaa mikakati madhubuti ya ufuatiliaji wa madeni inayodai ili kuliwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

2.2.6 Kuongezeka kwa Madeni (Payables)

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji za Taasisi na Mashirika ya Umma, Kamati imebaini kuwa imekuwa ni desturi kwa Baadhi ya Taasisi za Umma kutolipa madeni yake kwa wakati (payables) baada ya kupokea huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali na kusababisha ukuaji wa madeni hayo. Hali hii inatishia ukuaji wa mtaji wa Taasisi hizo kwa kuwa Taasisi hizo zinaweza zikatengeneza hasara kutokana na fedha nyingi kutumika katika ulipaji wa madeni. Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuwa na changamoto hiyo ni pamoja na DAWASA, Kampuni ya Huduma za Meli, GPSA, TEMESA, RUWASA, SIDO na EPZA.

Pamoja na hatua zinazochukuliwa na Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Dar es Salaam DAWASA katika kulipa madeni yake, Kamati inaona bado kuna haja ya kuwa na mpango mzuri wa ulipaji wa madeni hayo ambapo kwa Mwaka 2019/

20 Dawasa inadaiwa **Shilingi Bilioni 291.380**. Ili kuimarisha utendaji na Uwekezaji, Kamati inashauri DAWASA iweke mikakati madhubuti katika kulipa madeni yake kwa huduma wanazopatiwa ili kuweza kuepuka migogoro na watoa huduma wake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusu uwezo wa Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services) kulipa madeni ya wazabuni na watumishi umebaini kuwa, Kampuni inadaiwa madeni yanayofikia kiasi cha **Shilingi 5,339,705,339.95** ikiwa madeni ya wazabuni ni **Shilingi 5,125,158,885.75** na madeni ya Watumishi ni **Shilingi 214,546,752.20**. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, kiasi cha **Shilingi 404,236,423.14** tu cha madeni ya wazabuni ndicho kilicholipwa na hivyo kubaki **Shilingi 4,720,922,164.61** Pia, kiasi cha **Shilingi 135,298,237.24** cha madeni ya Watumishi kimekipwa na kubaki madai ya **Shilingi 79,248,514.95**. Kutokana na kasi ndogo ya ulipaji wa madeni hayo, Kamati inashauri Kampuni kuandaa mpango mkakati wa ulipaji wa madeni yote ya wazabuni na watumishi.

Aidha, Wakala wa Manunuzi Serikalini (GPSA) inafanya biashara na wadau mbalimbali. Katika mchakato wa biashara, Wakala inadaiwa kiasi kikubwa cha fedha na madeni hayo yamekuwa yakiongezeka kutoka kiasi cha **Shilingi Bilioni 50.327** mwaka 2018/2019 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 84.812** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **Asilimia 69**. Kuongezeka kwa madeni kunatokana na Wakala kuendelea kupokea fedha za wateja kwa ajili ya ununuzi wa magari (customers Deposit) huku Wakala ikichukua muda mrefu kuwapatia magari hayo wateja wao. Ili kuondoa changamoto hiyo, Kamati inashauri Wakala kuharakisha mchakato wa utoaji wa huduma kwa wateja wake na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi ili kupunguza mzigo huo wa madeni.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kwa upande wa wazabuni na watumishi, madeni yameongezeka kutoka kiasi cha **Shilingi Bilioni 26.36** mwaka 2018/19 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 33.41** mwaka 2019/20 sawa

na ongezeko la **Asilimia 26.74**. Kamati inashauri Wakala iandae mipango madhubuti ya ukusanyaji wa mapato pamoja na kulipa madeni wa wazabuni na watumishi.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa mwaka 2019/20 ilikuwa na madeni ya **Shilingi Bilioni 201.252** yote yakiwa ni madeni ya muda mfupi. Madeni haya yanajumuisha madeni ya watoa huduma (Payables and Accruals) yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 37.349** ikiwa ni sawa na asilimia 19 ya madeni yote na Mapato yaliyoahirishwa (Deferred Income) yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 163.903** ikiwa ni sawa na asilimia 81 ya madeni yote.

Taarifa zilizokaguliwa za Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) zimebainisha kuwa madeni ya Shirika yameongezeka kwa asilimia 77 kutoka **Bilioni 4.74** kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia **Bilioni 8.41** mwaka 2019/2020 na madeni haya yalitokana na kuongezeka kwa madeni ya wazabuni wa ndani wa Shirika. Kamati inalishauri Shirika kuandaa mkakati wa ulipaji wa madeni yake, vile vile Kamati inalishauri Shirika kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato ya shirika ili kuliwezesha ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kulipa madeni yake kwa wakati.

Vile vile, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Madeni ya Mamlaka ya EPZ yameongezeka kwa **asilimia 14** kutoka shilingi **bilioni 73** ya mwaka 2018/2019 hadi kufikia **bilioni 83** kwa mwaka 2019/2020. Madeni haya yalichangiwa na kuongezeka kwa madai ya malipo ya fidia pamoja na kodi ya Ardhi. Kamati inalishauri Shirika kuandaa mkakati madhubuti wa ulipaji wa madeni hayo, sambamba na hilo kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya Sheria na kuona haja kufanya marekebisho yatakayotoa msamaha kwa maeneo ya EPZA ambayo bado uwekezaji haujafanyika yasilipiwe kodi ya Ardhi mpaka pale uwekezaji utakapofanyika.

2.2.7 Taasisi kutokuwa na Mtazamo wa Kibiashara

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mashirika ya Umma zinazofanya biashara zinatakiwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu

kutokana na dhumuni la uanzishwaji wake ili ziweze kuwa shindani katika soko na kuzalisha mapato ya kutosha. Kamati imekutana na baadhi ya Taasisi za Umma zinazofanya biashara na kubaini changamoto ya Taasisi hizo ni kutokuwa na mtazamo wa kibiashara hali inasababisha kushindwa kutumia fursa za biashara walizonazo na baadhi yake kuendelea kutegemea ruzuku ya Serikali.

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) ni Taasisi inayofanya biashara na ipo katika soko lenye ushindani mkubwa. Kamati imeona kuna kila sababu ya Shirika kuwa na mtazamo wa kibiashara pamoja na kuongeza ubunifu wa utoaji wa huduma ili kuvutia wateja wengi zaidi. TTCL inatakiwa kuboresha huduma zake na kuweka mikakati ya kibiashara itakayoliwezesha kukabiliana na ushindani uliopo katika sekta ya mawasiliano.

Vile vile, Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services) ni Kampuni ambayo kimsingi inatakiwa kujiendesha kibiashara ili iweze kuzalisha mapato ya kutosha na kuongeza mtaji wa kampuni. Hata hivyo Kampuni imeshindwa kuwa na mbinu mbalimbali za kibiashara ili kuvutia wateja wakubwa na kukuza biashara yake licha ya kuwa na fursa kubwa ya kibiashara. Kamati inashauri Kampuni kuangalia fursa zote za biashara zilizopo ziwani ili kuimarisha mapato na kukusanya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yake.

2.2.8 Uwiano Usioridhisha wa Mali kwa Madeni ya Muda Mfupi

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa kina katika masuala ya kifedha ili kuhakikisha kunakuwa na uwiano mzuri wa Mali kwa Madeni. Uwiano huu unalenga kupima uwezo wa Taasisi na Mashirika ya Umma kulipa madeni yake ya muda mfupi yanapohitajika kulipwa kwa kutumia mali za muda mfupi (current ratio). Taasisi za Umma zinatakiwa ziwe na ukwasi ili ziweze kulipa madeni yake na kugharamia shughuli zake za kila siku. Kwa tafsiri nyepesi Taasisi na Mashirika ya Umma yanatakiwa kuwa na mali za muda mfupi mara mbili zaidi ya kiwango cha madeni yake (2:1).

Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya Taasisi kama GPSA, TPA, TEMESA, RUWASA, LATRA, TPDC na PSSSF kuwa na uwiano wa mali kwa madeni ya muda mfupi usioridhisha.

Kamati imechambua kwa kina taarifa za Wakala wa manunuzi Serikalini (GPSA) na kubaini uwezo mdogo wa wakala kulipa madeni yake yote pindi itakapohitajika kufanya hivyo kwa kuwa hali ilivyo sasa uwiano huu umepungua kutoka 1.19:1 mwaka 2018/2019 hadi 1.15:1 mwaka 2019/2020. Aidha, uwiano huu upo chini ya kiwango elekezi cha 2:1. Kamati inashauri Taasisi kuongeza ukwasi wake ili Taasisi iwe katika nafasi nzuri ya kulipa madeni yake ya muda mfupi na kuongeza imani kwa watoa huduma wake.

Uchambuzi uliofanywa na Kamati katika taarifa za Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) umebainisha kuwa uwiano huu umepungua kutoka 1.27:1 mwaka 2017/18 hadi 1.15:1 mwaka 2019/20. Hali ilivyo sasa, iwapo TPA italipa madeni yake yote ya muda mfupi haitakuwa na uwezo wa kugharamia shughuli zake za uendeshaji za kila siku.

Aidha, taarifa za fedha za Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) zilizowasilishwa mbele ya Kamati zimeonesha uwepo wa changamoto ya Wakala kuwa na uwezo mdogo wa kulipa madeni yake ambapo, katika mwaka 2019/20 uwiano huu ulidhoofu na kufikia 1.57:1 ikilinganishwa na uwiano wa 1.67:1 mwaka 2018/19 wakati kiwango elekezi ni 2:1. Katika eneo hili, imedhihirika kuwa, TEMESA ina uwezo mdogo wa kulipa madeni yake na kuendelea kujijendesha. Kamati inashauri TEMESA kuwa na mali za muda mfupi mara mbili zaidi ya kiwango cha madeni yake.

Katika mwaka wa Fedha 2019/2020, Mamlaka ya Maji safi na usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilikuwa na uwiano wa Mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi (Current Ratio) wa 1.47:1. Uwiano huo sio mzuri kwani upo chini ya kiwango cha chini kinachotakiwa cha 2:1, Mamlaka

inapaswa kuangalia namna ya kuboresha uwiano huo ili ifikie au izidi kiwango kilichowekwa.

Vile vile, uchambuzi wa taarifa za kifedha wa Mamlaka ya Udhhibiti usafiri Ardhini (LATRA) katika mwaka wa Fedha 2019/2020 umebainisha kuwa, Mamlaka ilikuwa na uwiano wa Mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi (Current Ratio) wa 1.7:1. Hivyo Mamlaka inapaswa kuangalia namna ya kuboresha uwiano huu ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi sambamba na ulipaji wa madeni ya haraka.

Uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa taarifa za Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) unaonesha kuwa, shirika halina uwezo wa kulipa madeni ya haraka na hivyo kuhatarisha uendelevu wa shirika kutokana na kuwa na uwiano wa 0.8:1. Uwiano uliopo si kiashiria kizuri kwa utendaji wa Shirika kwa kuwa uwezo mdogo wa ulipaji wa madeni unahatarisha uwezo wa Shirika kutekeleza majukumu yake na kukosa fedha kwa ajili ya uendeshaji (working capital)kutokana na kutokuwa na ukwasi (Liquidity) wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa uwiano wa mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi (PSSSF) si wakuridhisha ambapo taarifa za mfuko zilizokaguliwa zimebainisha kuwa kwa mwaka 2019/2020 ulikuwa na uwiano wa 1.3:1, uwiano huu upo chini ya kiwango elekezi cha 2:1. Hii ina maana kuwa, kwa kutumia mali zake za muda mfupi, Mfuko una uwezo mdogo wa kulipa madeni yake na kuendelea kujiendesha kikamilifu. Kamati inaishauri Mfuko kuweka mkakati madhubuti wa ukusanyaji wa madeni yake ili kujiweka katika nafasi ya kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kulipa madeni na kuwahudumia mwanachama pindi inapohitajika.

2.2.9 Miradi Kutokamilika kwa Wakati

Mheshimiwa Spika, kazi ya ufuatiliaji wa miradi ya uwekezaji inayofanywa na Kamati imebainisha kuwa, baadhi ya miradi

ya uwekezaji inashindwa kutekelezeka kwa wakati kutokana na michakato mingi na muda mrefu unaochukuliwa na Serikali katika kufanya maamuzi pamoja na Serikali kutopeleka fedha za utekezaji wa miradi hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na NDC kupewa majukumu mazito ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati, Serikali haijatia mkazo katika uwekezaji huo wenye maslahi mapana ya Taifa kwa kuacha kupeleka fedha za kutekeleza miradi hiyo licha ya fedha hizo kuidhinishwa na Bunge. Katika Mwaka wa fedha 2019/2020 Bunge lilidhinisha jumla ya **Shilingi Bilioni 31.2** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2020, Serikali haijapeleka kiasi chochote cha fedha katika Shirika hilo kwa ajili ya utekezaji wa miradi ya kimkakati licha ya kuwa fedha hizo ziliidhinishwa na Bunge. Kiasi kilichotumiwa na NDC katika kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kilitokana na mapato ya ndani ya Shirika ambayo ilikuwa ni **Shilingi Bilioni 8.4**.

Vile vile, imebainika kuwa, baadhi ya miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na NDC inashindwa kutekelezeka kwa wakati kutokana na michakato mingi na muda mrefu unaochukuliwa na Serikali katika kufanya maamuzi. Mfano tatizo hili lipo katika mradi wa kimkakati wa Mchuchuma na Liganga ambapo umesimama kwa muda mrefu kutokana na timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT) kuchelewa kukamilisha kazi yake.

Aidha, tatizo limeonekana katika mradi wa Kiwanda cha kuunganisha Matrekta ya URSUS kinachosimamiwa na NDC, mkataba wa mradi huu ulihusisha kuingiza **matrekta 2400**, kujenga kiwanda cha kuunganisha matrekta, kujenga vituo 8 vya kuhudumia matrekta. Utekezaji wa mradi huu unasuasua ambapo Mbia katika mradi huu Kamapuni ya URSUS S.A ya Poland ameshindwa kukamilisha utekezaji wa Mkataba wa mradi huu. Mradi ulipaswa kuwa umekamilika kufikia Juni, 2018 lakini ni **matrekta 822** tu yaliyopokelewa na hakuna kituo kilichojengwa mpaka sasa. NDC imeripoti kuwa majadiliano yanaendelea katika ya Serikali ya Tanzania na Poland kwa lengo la kuangalia njia sahihi ya kukwamua mradi huu.

Mheshimiwa Spika, NDC ni Shirika la kimkakati lililopewa jukumu kubwa la kuendeleza na kutekeleza miradi ya kiuchumi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Jitihada za makusudi zinapaswa kufanyika ili kuliokoa Shirika hilo, ili tuendeele kupata faida ya Ajira kwa Watanzania, ukuaji wa sekta ya Viwanda na mchango wa Shirika katika Mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, majadiliano yanaendelea kati ya Serikali ya Poland na Tanzania juu ya mradi wa matrekta yawekewe muda maalumu wa kukamilika ili utekelezaji wa mradi huu uendeele.

Changamoto ya miradi kutokamilika kwa wakati imetokea pia katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ambapo, hadi taarifa zake zinawasilishwa mbele ya Kamati mwezi Oktoba 2021, Kamati imebaini kuwa kazi za maboresho ya Bandari ya DSM zinazoendelea hasa katika Gati namba 6 na 7 zinasababisha gati hizo kutotumika hivyo kupunguza nafasi ya kuegesha meli nyingi kwa wakati mmoja. Mbali na hivyo meli za ujenzi nazo zinatumia sehemu ya gati za Bandari ya DSM. Kamati inashauri TPA iongeze kasi ya ukamilishaji wa miradi yake ili iweze kuboresha huduma na kuongeza watumiaji wa bandari hiyo kutoka nje ya Nchi hivyo kuongeza mapato, mnyororo wa thamani na ajira.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unatekeleza miradi mbalimbali kama sehemu ya jukumu lake la kuwekeza fedha za wanachama. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa miradi mingi inayotekelezwa na Mfuko iko nje ya muda uliopangwa wa kukamilika kwake, kuchelewa huku kunasababisha gharama za miradi kuongezeka na muda wa miradi hiyo kuanza kuzalisha faida unaongezeka. Fedha zilizotumika kuwekeza katika miradi hizo ni za wanachama na zinapaswa kuwepo pindi zitakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza jukumu lake kuu la kulipa mafao ya wanachama. Kamati inalishauri Shirika kuweka mkakati madhubuti wa kukamilisha miradi yake kwa muda uliopangwa ili kuliwezesha Shirika kutimiza malengo ya uanzishwaji wa miradi hiyo. Aidha, Kamati inalishauri Shirika kufanya tathmini na kupitia upya maeneo ya uwekezaji ili kuhakikisha linawekeza katika maeneo yenye tija na

yatakayolipatia Shirika faida na kuongeza ajira mfano katika viwanda.

2.2.10 Uhaba wa Watumishi na Vitendea Kazi

Mheshimiwa Spika, matokeo chanya ya uwekezaji wowote wenye tija unategemea pia uwekezaji katika rasilimali fedha na rasilimali watu. Uwepo wa watu wenye weledi wa kutosha katika kutekeleza majukumu ya Taasisi ni muhimu ukazingatiwa kwa taasisi zote za Umma. Vile vile, uwepo wa vitendea kazi muhimu katika Taasisi ni moja wapo ya njia za kuifanya Taasisi iweze kufikia malengo ya uanzishwaji wake. Kamati imepitia taarifa mbalimbali za utendaji na uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma na kubaini uhaba wa watumishi na vitendea kazi kwa baadhi ya Taasisi kama GPSA, TPA na RUWASA.

Wakati wa majadiliano baina ya Kamati na uongozi wa Wakala wa Manunuzi Serikalini (GPSA), Wakala umebainisha upungufu wa watumishi hali inayopunguza ufanisi na weledi katika utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi unaotakiwa. Katika mwaka 2020/2021 mahitaji ya watumishi ni **390** watumishi waliopo ni **246** tu hivyo kuwepo kwa upungufu wa watumishi **144**. Kamati inaishauri Taasisi kufuata taratibu zote za kiutumishi ili kukamilisha ikama ya watumishi kwa ajili ya utendaji wenye tija wa Taasisi.

Aidha, Taarifa iliyowasilishwa na Uongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imebainisha kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi wenye weledi wa masuala ya huduma za kibandari katika Bandari ya Dar es Salaam hasa katika kitengo cha utekelezaji. Hali hii inapelekea mitambo na vifaa vingi kuendeshwa na wafanyakazi wa muda ambao weledi na ujuzi wao ni wa viwango vya chini. Ikama ya watumishi inayotakiwa katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ni Watumishi **3196** lakini kwa sasa kuna jumla ya Watumishi **2512** ambao ni pungufu ya Watumishi **1404**

Vile vile, Bandari ya Dar es Salaam inakabiliwa na uchakavu wa vifaa vya kuhudumia shehena kutoka melini na katika

yadi. Uhaba huu unasabisha shehena kutolewa Bandarini kwa kasi ndogo na hivyo kusabisha ucheleweshaji wa meli kuingia Bandarini kutokana na ufinyu wa nafasi ya kuhudumia shehena nyingine. Kutokana na kukosekana kwa vifaa vya kisasa katika Bandari ya Dar es Salaam kunaifanya Bandari kuwa na uwezo wa kufanya kazi chini ya Asilimia 50 ya uwezo wake unaotakiwa kwani kwasasa TPA inafanya kazi kwa Asilimia 29 tu ya uwezo wake wote.

Kamati pia imebaini upungufu katika Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ambapo, mahitaji wa watumishi ni **2,754** ikiliganisha na watumishi **1,663** waliopo kwa sasa, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **1,16**. Aidha, Mamlaka inakabiliwa pia na changamoto ya uchache wa vitendea kazi kama vile magari na pipiki.

2.2.11 Serikali kukiuka Matakwa ya Kimkataba

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Kamati ni kuhakikisha kila senti iliyowekezwa na Serikali inaleta tija iliyokusudiwa. Kwa mantiki hiyo, Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa kina katika uwekezaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una tija na umefuata taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.

Katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Kamati imebaini mkwamo mkubwa katika uwekezaji unaosababishwa Serikali kushindwa kutekeleza matakwa ya kimkataba kati yake na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) ambalo linaendesha Kiwanda cha Viuwadudu cha Tanzania Biotech Products limited (TBPL) kilichopo kibaha. Kiwanda hiki ni muhimu sana kwa mustakabali ya maisha ya watu na uchumi wa Taifa. Ili tija ya uwekezaji katika kiwanda hiki iweze kuwa kubwa, NDC iliingia Mkataba wa miaka mitano wa Mauzo ya Viuadudu (Biolarvicides Offtake Agreement) kwa Wizara ya Afya, Mkataba huu uliosainiwa tarehe 11 Machi, 2015 ili kuwa na uhakika wa soko la ndani. Hata hivyo, mkataba huo haukuweza kutekelezwa kutokana na Serikali kutoweka kipaumbele na kutotenga bajeti kwenye Halmashauri zake kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kushindwa kutekeleza makubaliano yake ya kimkataba kunasababisha kupungua kwa mapato ya Shirika fedha ambazo zingeongeza uwezo wa NDC kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Licha ya Mheshimiwa Rais wa awamu ya Tano Hayati John Magufuli kutoa tamko la kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha za kununua viwadudu pindi alipotembelea kiwandani hapo tarehe 22.06.2017, Halmashauri hizi zilichukua dawa hizo mara moja tu na ulipaji wao ulikuwa wakusuasua mpaka hivi sasa kuna baadhi hazijakamilisha malipo hayo na hakuna muendelezo wa kuchukua dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali inayoendelea katika kiwanda cha Viuwadudu, Kamati inahoji juu ya nia ya Serikali kuwekeza katika kiwanda hiki, Kamati inaishauri Serikali kutafakari upya nia yake katika kiwanda hiki pamoja na kuja na mkakati madhubuti wa kukiendeleza.

2.2.12 Uwiano Usioridhisha wa Gharama za Uendeshaji kwa Mapato

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za Umma. Kamati imekuwa ikichambua na kupima kiasi cha mapato kinachotumika kugharamia matumizi ya Taasisi ili ziweze kuwa na bakaa na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kamati imebaini uwepo wa uwiano usioridhisha wa gharama kwa mapato kwa baadhi ya Taasisi za Umma kama TTCL, TPDC, NHC, TFS na SIDO.

Katika kipindi cha miaka miwili Uwiano wa Gharama za uendeshaji kwa Mapato ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) umezidi kuzorota na kufikia hadi **Asilimia 102** mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na **Asilimia 95** mwaka 2018/2019. Kuzorota kwa Uwiano huu kumetokana na matumizi kuongezeka kwa **Asilimia 15** ikilinganishwa na kasi ya kuongezeka kwa mapato kwa **Asilimia 11**. Kamati inashauri Shirika kuimarisha uwiano huu na kutozidi ukomo wa Asilimia 50 uliowekwa na Msajili wa Hazina ili Shirika liwe na fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake.

Vile vile, kwa upande wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), uwiano wa gharama kwa mapato katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kimekuwa juu kwa miaka yote ikilinganisha na ukomo wa kigezo hicho uliowekwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina wa asilimia 50. Takwimu zinaonesha katika vipindi husika kiwango cha gharama kwa Shirika kilikuwa kati ya **Asilimia 96.4** (2019/20) na **Asilimia 96.3** (2018/19). Kiasi hiki ni kikubwa sana na hivyo, Shirika linashauriwa kupunguza matumizi yake ili kuendana na ukomo wa kiwango kilichowekwa.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika mwaka wa Fedha 2019/20, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lilikuwa na uwiano wa gharama za uendeshaji kwa Mapato wa **Asilimia 74**. Uwiano huo sio mzuri kwani upo juu ya kiwango cha asilimia 50 kilichowekwa na inaashiria kwamba matumizi ya Shirika ukilinganisha na Mapato yapo juu ya uwiano uliowekwa. Kamati inashauri Shirika kufanya jitihada za kupunguza matumizi ya uendeshaji hususani matumizi ya utawala na matumizi mengine yasiyo ya lazima ili kupunguza uwiano huu na kuufanya uwe ndani ya kiwango kilichowekwa.

Vile vile, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa uwiano wa gharama za Wakala wa Misitu (TFS) kwa mapato yake upo juu ya kiwango kilichowekwa na Msajili wa Hazina ambapo umeendela kukua kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017/18 hadi 2019/20. Sababu iliyoripotiwa kuongeza uwiano huu ni kuongezeka kwa vibarua katika mashamba ya miti, Kamati inaishauri Shirika kuwa ongezeko hili liendane na ongezeko la maeneo mapya yaliyopandwa miti.

Taarifa zilizokaguliwa za SIDO zinaonyesha kuwa gharama za uendeshaji kwa mapato zimeongezeka ambapo katika mwaka wa feza 2018/19 zilikuwa asilimia 90 na ziliongezeka hadi kufikia asilimia 117 mwaka wa fedha 2019/20 kiwango hiki hakiridhishi na kipo nje ya ukomo wa kisheria uliowekwa wa asilimia 60. Uwiano huu unaonyesha kuwa matumizi ya Shirika yapo juu ya mapato, Kamati inalishauri Shirika

kuchukua jitihada za makusudi za kurekebisha uwiano huu ili uwe ndani ya kiwango kinachotakiwa.

2.2.13 Uwiano usioridhisha wa Faida kwa Mali

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiangalia uwiano wa faida kwa mali ili kupima kiasi cha faida kinachopatikana kutokana na mali zilizowekezwa kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma. Ili kuongeza tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeweka kiwango elekezi kisichopungua cha Asilimia 15. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, bado kuna baadhi ya Taasisi ambazo hazijafikia kiwango hiko elekezi.

Uwiano wa faida kwa mali za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Uwiano huu unalenga kupima kiwango cha faida kinachozalishwa na mali za Shirika. Uwiano huu umepanda kutoka asilimia hasi 7 (negative 7%) mwaka 2017/18 hadi kufikia asilimia hasi 1 (negative 1%) kwa Mwaka 2018/19 kutokana na kupungua kwa hasara ya Shirika. Aidha, uwiano huu umepanda hadi kufikia asilimia 9 kwa mwaka 2019/20, pamoja na kuwa na ukuaji wa Uwiano huu Kamati inashauri Shirika kuendelea na juhudi za kutengeneza faida ili uwiano huu uweze kufikia kiwango kilichowekwa cha **Asilimia 15** kwa mwaka. Hii itaongeza tija katika uwekezaji uliofanywa ndani ya Shirika.

Kamati pia imechambua Uwiano wa faida kwa mali wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ambapo, Katika kipindi cha mwaka 2020, Benki imekuwa na uwiano wa **Asilimia 2.33** ambao uko chini ya kiwango elekezi cha **Asilimia 15** kilichowekwa na Msajili wa Hazina. Hivyo, Kamati inashauri TADB iongeze juhudi katika kuongeza mapato na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ili kuwa na faida ya kutosha na kupandisha kiwango cha uwiano huu kufikia kiwango elekezi kilichowekwa na Msajili wa Hazina.

Vile vile, Kamati iliangalia uwiano wa faida kwa mali za Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na kubaini kuwa hauridhishi na umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka

ambapo umepungua kutoa asilimia hasi 1 2018/19 hadi kufikia asilimia hasi 3 2019/2020 kutokana na shirika kupata Hasara. Kamati inalishauri shirika kuchukua hatua za makusudi za kuliwezesha Shirika kupata faida na kufanikisha matumizi mazuri ya mali za shirika ambazo Serikali iliwekeza ili litoe faida na kujiendesha ipasavyo.

2.2.14 Uwezo wa ukusanyaji wa mapato

Mheshimiwa Spika, uwezo kukusanya mapati ya shirika ni moja ya kigezo cha kupima ufanisi wa wa Shirika, Kamati ilipima ufanisi wa Wakala wa kuhudumia Misitua (TFS) wa kukusanya mapato ya ndani na kubaini kuwa ulishuka kwa asilimia 19 ambapo kwa mwaka 2018/2019 ulikuwa kwa asilimia 103 na mwaka 2019/2020 ulikuwa asilimia 84. Uwiano huu uko ndani ya kiwango kilichowekwa na Msajili wa hazina lakini sio kiashiria kizuri, TFS inahitaji fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi unaotarajiwa lakini juhudi za kukusanya mapato zinapungua. Kamati inaishauri Wakala kuandaa mpango madhubuti wa ukusanyaji wa mapato yake ya ndani na msisitizo upo katika matumizi ya njia za kielektoniki ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato. Aidha, Kamati inaishauri TFS kuongeza vyanzo vya mapato yake ya ndani kwa kuangalia fursa mpya za uwekezaji ili kuongeza mapato yake na kuongeza mchango wake katika mfuko Mkuu wa Serikali.

2.2.15 Changamoto za Bodi za Wakurugenzi

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wakurugenzi ndicho chombo kikuu cha maamuzi katika Taasisi na Mashirika ya Umma, lakini kuna ucheleweshaji wa kupata Bodi ambapo baadhi ya taasisi zimekuwa zikiakaa kwa zaidi ya mwaka bila kupata bodi mpya jambo linalopelekea taasisi hizo kutokuwa na utendaji wa kuridhisha kwa kuwa hakuna usimamizi kwa niaba ya Serikali na pia hakuna chombo cha maamuzi. Mfano Bodi ya TIC ambayo ilimaliza muda wake tangia Septemba 2020 bado haijaundwa.

Vile vile, baadhi ya Bodi zinachangamoto ya Muudo wa Bodi za Wakurugenzi, Mfano Bodi ya EPZA ambapo wajumbe wake ni watendaji wa Serikali ambao wapo katika nafasi kubwa Serikalini ambapo Kamati imehofika upatikanaji wao kwa ajili ya vikao vya Bodi. Kamati inaishauri Serikali kufanya uteuzi wa bodi pindi unapohitajika, aidha, muda wa Wajumbe wa Bodi upishane ili kuwa muendelezo (Succession plan)

2.3 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliwasilisha Taarifa yake ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 mbele ya Bunge lako Tukufu. Taarifa hiyo ilijumuisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambayo yalikuwa ni Maazimio ya Bunge na kutakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuongeza tija na ufanisi katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha, Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa Maazimio **Tisa** yaliyotolewa kupitia kwa Msajili wa Hazina ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali.

Pamoja na ukweli kwamba, Serikali kwa kiasi kikubwa imechukua hatua katika kutekeleza maazimio ya Bunge, bado kuna baadhi ya maazimio ambayo hayajatekelezwa kikamilifu hali inayosababisha Utendaji na Uwekezaji wa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na ufanisi na tija. Katika maazimio Tisa yaliyotolewa kwa Serikali ni maazimio Matatu pekee ndiyo yaliyofanyiwa kazi kikamilifu na maazimio Sita yaliyotolewa na Bunge hayajatekelezwa kikamilifu na Serikali. Hoja ambazo utekelezaji wake haujakamilika kikamilifu ni kama ifuatavyo:-

i) Bunge liliazimia kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe kuwa Taasisi na Mashirika yote ya Umma yanazingatia matakwa ya Kifungu cha 46 cha Sheria ya Fedha Na. 16 ya Mwaka 2015 pamoja na miongozo yote inayotolewa na Msajili wa Hazina. Aidha, Sheria hii ipitiwe kwa kuweka kipengele kitakachoitaka Bodi na Menejimenti

kuachia madaraka endapo watakwenda kinyume na matakwa ya Sheria. Pamoja na azimio hilo, bado kuna baadhi ya Taasisi ambazo yanakiuka matakwa ya Sheria hiyo.

ii) Bunge liliazimia Serikali kuhakikisha changamoto zote zilizopo katika miradi yote zinaondolewa haraka iwezekanavyo na miradi yote iliyosimama inakamilishwa ili tija ya uwekezaji huo ipatikane na watakaosababisha hasara wawajibishwe.

iii) Bunge liliazimia kuitaka Serikali kuandaa miongozo maalumu kwa Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika itakayoainisha madhara yatakayopatikana kutokana na kushindwa kubuni mikakati madhubuti ya ukusanyaji na ulipaji wa madeni na itakayowajibisha watendaji watakaokiuka miongozo hiyo. Hata hivyo, bado kuna Baadhi ya Taasisi ambazo hazina mikakati ya ulipaji na ukusanyaji wa madeni.

iv) Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kushughulikia masuala yote ya kisera kuhusu upelekaji wa miundombinu muhimu katika miradi ya nyumba inayotekelezwa na Taasisi za Umma kabla ya miradi kuanza ili kuleta unafuu wa bei za nyumba kwa mlaji wa mwisho na kupunguza mzigo wa gharama kwa Taasisi zinazohusika na miradi hiyo. Vile vile, kuwe na makubaliano na mipango ya pamoja juu ya ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika maeneo ya mradi kabla ya kuanza kwa mradi husika. Kamati inaitaka Serikali kushughulikia suala hili kikamilifu.

v) Agizo la Bunge la kuitaka Serikali kupitia Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika machache yenye changamoto ya Maafisa Masuuli wanaokaimu nafasi hizo kuhakikisha watumishi ambao wanakaimu na wana uwezo wa kutumikia nafasi hizo wakiwa na sifa stahiki na weledi katika utendaji kazi wao wanathibitishwa katika nafasi hizo ili waweze kuwa na mamlaka kamili.

vi) Bunge liliazimia kuitaka Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuendelea kuzikutanisha Taasisi zilizobaki zinazodaiana na kuzisimamia ili kuhakikisha madeni yote yanalipwa na kila

Taasisi inapata inachostahili ili shughuli za msingi za Taasisi hizo ziweze kutekelezeka

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 *Maoni*

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina ili kujirihisha iwapo dhamira ya Serikali kufanya uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa inatekelezwa kikamilifu na Taasisi hizo na Serikali inapata faida stahiki kutokana na uwekezaji huo. Kutokana na uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

Utendaji wenye tija wa Taasisi na Mashirika ya Umma ni chachu ya maendeleo ya Taifa kwakuwa Serikali itanufaika na uwekezaji uliofanywa katika Taasisi za Umma kwa kuwapatia wananchi wake huduma bora za afya, elimu, maji na barabara kwa kutaja baadhi ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato yasiyo ya kodi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kamati imeona jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa mitaji ya umma iliyowekezwa na Serikali katika Taasisi mbalimbali. Mageuzi ya kiutendaji yaliyofanywa yameongeza tija na weledi katika Taasisi za Umma na kuiwezesha Serikali kukusanya mapato yasiyo ya kodi ambapo hadi kufikia tarehe 30 juni, 2021 jumla ya **Shilingi Bilioni 850.28** zilikusanywa.

Mheshimiwa Spika, matamano ya Kamati ni kuona uwekezaji unaofanywa na Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa unafanyika kwa ufanisi na tija na Taifa linanufaika kutokana na uwekezaji huo. Kamati inaipongeza Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kuzisimamia Bodi na Menejimenti za Taasisi za Umma. Hata hivyo, ipo haja ya kuendelea

kuzichukulia hatua stahiki Taasisi zote zinazokiuka taratibu na Sheria zilizoanzisha Taasisi hizo ili hatimaye uendeshaji wa Bajeti ya Serikali kwa kiasi kikubwa utegemee mapato yasiyo ya kodi.

Kutokana na changamoto mbalimbali za kiuchumi zilizoikumba Dunia ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa UVIKO 19, Mwenendo wa mapato yanayokusanywa katika Mfuko Mkuu wa Serikali umekuwa si wa kuridhisha sana kwa kuwa mapato hayo yamekuwa yakipungua. katika mwaka wa fedha 2020/21 mapato yanayotokana na gawio na michango ya Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa ni jumla ya **Shilingi Bilioni 850.28** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi Bilioni 983.1** kilichokusanywa katika Mwaka wa fedha 2019/20. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutumia fursa zote za kibiashara na kubuni mikakati madhubuti itakayoziwezesha Taasisi na Mashirika ya Umma kuongeza tija katika utendaji wake sambamba na kuongezeka kwa mapato.

Kwa muktadha huo, Kamati inaendelea kushauri na kuisisitiza Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi wa mitaji yake, kubainisha na kuondoa changamoto zote za kifedha na kiutendaji ili Bodi na Menejimenti za Taasisi zote za Umma ziweze kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu. Kwa kufanya hivyo, Serikali itapata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wakati sahihi na kwa manufaa ya Nchi yetu.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni ya jumla ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa Mitaji ya Umma, naomba kutoa mapendekezo ya kamati kama ifuatavyo:-

3.2.1 Upungufu wa Mtaji katika Taasisi za Umma

KWA KUWA, Mashirika na Taasisi za Umma zinahitaji mtaji wa kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kufanya uwekezaji wenye tija,

NA KWA KUWA, baadhi ya Mashirika na Taasisi zimeshindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji kutokana na changamoto ya kifedha inayotokana na kukosekana kwa mtaji,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaziwezesha Taasisi zote zenye changamoto ya mtaji ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisa na kuleta tija iliyokusudiwa wakati wa uanzishwaji wa Taasisi hizo. Aidha, Serikali kupitia Msajili wa Hazina izishauri vema Taasisi za Umma na kuzisimamia katika kutumia fursa mbalimbali zilizopo na kukuza mitaji ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye viwanda na Soko la Hisa.

3.2.2 Kupungua kwa Mtaji wa Uendeshaji

KWA KUWA, kumekuwa na Taasisi na Mashirika ya Umma yenye mtaji hasi wa uendeshaji (Negative Net working capital) hasa kwa Mashirika yanayojiendesha kibiashara,

NA KWA KUWA, kutokuwa kwa mtaji wa uendeshaji (working capital) unaoridhisha kunazifanya Taasisi na Mashirika hayo kushindwa kutekeleza shughuli zake za msingi kwa wakati pamoja na kushindwa kulipa madeni yake bila ya kuathiri utendaji wake,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuhakikisha Bodi na Menejimenti za Taasisi za Umma zinasimamiwa kwa karibu na kuzitaka kuwa na utendaji wenye ufanisa na tija ili Taasisi hizo ziwe na mtaji chanya wa uendeshaji.

3.2.3 Taasisi za Umma Kutofanya kazi pamoja

KWA KUWA, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya Taasisi za Umma kushindwa kusikilizana na kufanya kazi pamoja kwa maslahi mapana ya Nchi,

NA KWA KUWA, kukosekana kwa ushirikiano katika utekelezaji wa baadhi ya miradi kunakwamisha utendaji wa taasisi nyingine na kuongeza gharama za uendeshaji kama ilivyotokea kwa TANESCO kushindwa kupeleka Umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo unaosimamiwa na STAMIGOLD ambayo inamilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO),

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuhakikisha kila Taasisi inatekeleza wajibu wake kwa wakati na kwa ufanisi ili kurahisisha utekelezaji wa miradi au majukumu ya Taasisi nyingine. Vile vile, Serikali ihakikishe TANESCO inaharakisha upelekaji wa umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo pamoja na miradi mingine ya kimakakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Taasisi hizo.

3.2.4 Kuongezeka kwa Gharama za Uendeshaji

KWA KUWA, imekuwa ni desturi kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kukiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 ya kutozidi ukomo wa gharama za uendeshaji wa Asilimia 60,

NA KWA KUWA, ukikukwaji wa matakwa ya Sheria hiyo kumesababisha Taasisi hizo kushindwa kuzalisha faida na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ihakikishe inazisimamia kwa karibu zaidi kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo na kuchukua hatua stahiki Taasisi zote zinazozidisha matumizi yasiyoendana na uwekezaji.

3.2.5 Kushindwa kukusanya Madeni (Receivables)

KWA KUWA, imekuwa ni changamoto kubwa kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni pamoja na kuwa na uwezo mdogo wa kukusanya madeni yake baada ya kutoa huduma au kufanya biashara na Taasisi nyingine,

NA KWA KUWA, tatizo hili si kiashiria kizuri katika utendaji wa Taasisi hizo kwa kuwa kinapunguza mapato ya Taasisi pamoja na kupunguza uwezo wake wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ihakikishe Taasisi zote za Umma zinakuwa na mkakati madhubuti wa ukusanyaji wa madeni yake ili kuongeza mapato yake na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

3.2.6 Kuongezeka kwa Madeni (Payables)

KWA KUWA, imekuwa ni desturi kwa Baadhi ya Taasisi za Umma kutolipa madeni yake kwa wakati (payables) baada ya kupokea huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali na kusababisha ukuaji wa madeni hayo,

NA KWA KUWA, hali hii inatishia ukuaji wa mtaji wa Taasisi kwa kuwa Taasisi hizo zinaweza zikatengeneza hasara kutokana na fedha nyingi kutumika katika ulipaji wa madeni yakiwa pamoja na riba,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina

(a) Kuzikutanisha Taasisi zote za Serikali zinazodaiana ili kumaliza madeni yao na kuhakikisha madeni yote kutoka sekta binafsi yanalipwa.

(b) Kuandaa miongozo itakayoziielekeza Taasisi zote za umma kulipia huduma inazopata kutoka katika taasisi nyingine kwa wakati

(c) Serikali ilipe madeni yake yote inayodaiwa na Taasisi zake za umma

3.2.7 Taasisi kutokuwa na Mtazamo wa Kibiashara

KWA KUWA, imekuwa ni changamoto kubwa kwa Taasisi za Umma zinazofanya biashara kushindwa kuwa shindani katika

soko kutokana na kutokuwa na mtazamo wa kibiashara kwa kukosa mbinu za kisasa za kibiashara,

NA KWA KUWA, kukosekana kwa mtazamo wa kibiashara kwa kiasi kikubwa kunazifanya Taasisi hizo kushindwa kuzalisha mapato ya kutosha na kushindwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuhakikisha Taasisi zote zinazofanya biashara zinakuwa na mikakati ya kibiashara pamoja na kuzalisha mapato ya kutosha.

3.2.8 Uwiano Usioridhisha wa Mali kwa Madeni ya Muda Mfupi

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa na uwiano wa mali kwa madeni ya muda mfupi usioridhisha hali inayosababishwa na Taasisi hizo kutokuwa na ukwasi wa kutosha,

NA KWA KUWA, kutofanya vizuri kwa Taasisi katika ulipaji wa madeni kunadhohofisha ukutekelezaji wa majukumu ya kila siku ya taasisi hizo na kusababisa kutengeneza hasara,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuzisimamia kwa karibu Taasisi zake ili ziweze kukidhi matakwa na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali kuhusu uwekezaji bora na kuhakikisha zinakuwa na ukwasi wa kutosha kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake.

3.2.9 Miradi kutokamilika kwa Wakati

KWA KUWA, miradi mingi ya uwekezaji inashindwa kukamilika kwa wakati kutokana na wingi wa michakato, Serikali kuchukua muda mrefu katika kufanya maamuzi, umakini wa Serikali katika kupata wawekezaji sahihi pamoja na kutopeleka fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati,

NA KWA KUWA, kushindwa kutekelezeka kwa miradi hiyo kwa wakati kunaongeza gharama za uwekezaji hali inayoondoa tija ya uwekezaji huo pamoja na kuchelewa kupatikana kwa faida ya uwekezaji huo kama ilivyotokea katika miradi ya Liganga na Mchuchuma na mradi wa Matrekta ya URSUS inayotekelezwa na NDC,

KWA HIYO BASI, Bunge liaazimia kuwa, Serikali ihakikishe

a) Wizara ya Fedha na Mipango inapeleka fedha za utekelezaji wa miradi yote kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa Sheria,

b) Wizara ya Viwanda na Biashara ihakikishe inatoa kipaumbele kwa kutumia fedha hizo katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) badala ya kuzielekeza katika maeneo mengine ya utendaji wa Wizara kwakuwa kukamilika kwa miradi hiyo mikubwa kutainua uchumi wa Taifa letu kwa kiasi kikubwa, na

c) Serikali iharakishe mchakato wa kupitia mkataba wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambao utekelezaji wake umekwama kwa muda mrefu kutokana na kuendelea kwa majadiliano katika Kamati ya majadiliano ya Serikali (GNT), suala hili litafutiwe ufumbuzi au kuamua kuachana na mbia aliepo na kutafuta muwekezaji mwingine,

d) Kabla ya Serikali haijaingia mkataba na muwekezaji yoyote ijiridhishe na Uwezo, ufanisi na tija itakayopatikana kutokana mradi husika ili kuepuka changamoto kama tulizokabiliana nazo katika miradi mbalimbali mfano mradi wa Matrekta ya URSUS.

3.2.10 Uhaba wa Watumishi na Vitendea kazi

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi za Umma zimekuwa na changamoto ya uhaba wa watumishi na vitendea kazi kwa muda mrefu sasa,

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa ikama ya watumishi na kukosekana na vitendea kazi muhimu kunasababisha Taasisi hizo kushinda kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kufanya kazi chini ya viwango,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi za Taasisi hizo kuhakikisha tatizo la upungufu wa watumishi na vifaa linafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili kuimarisha utendaji wa Taasisi hizo.

3.2.11 Serikali Kukiuka Matakwa ya Kimkataba

KWA KUWA, Serikali imeshindwa kutekeleza makubaliano yake ya kimkataba iliyoingia na NDC kuhusu Mauzo ya Viuadudu kwa muda wa miaka mitano (Biolarvicides Offtake Agreement) na Wizara ya Afya, uliosainiwa tarehe 11 Machi, 2015 ili kuwa na uhakika wa soko la ndani.

NA KWA KUWA, kushindwa kutekeleza Mkataba huo kumesababisha kupungua kwa mapato ya Shirika fedha ambazo zingengeza uwezo wa NDC kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na kuzalisha viuadudu kwa kiasi kikubwa.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali kuhakikisha

a) Wizara ya Fedha na Mipango itenge fedha kwa ajili ya kuiwezesha Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya *technical Study* ya matumizi sahihi ya Viuwadudu na kushughulikia kupatikana kwa ithibati (pre-qualification) ya Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kiwanda cha Viuwadudu cha Tanzania Biotech Products limited (TBPL) kilichopo kibaha ili kuiwezesha Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto kutumia fedha zinazotolewa na wahisani katika ununuzi wa viuwadudu vinavyozalishwa katika kiwanda hicho,

b) Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Hazina itenge fedha mahususi katika kifungu maalumu (**ring fenced**)

kitakachotumika kulipia ununuzi wa Viuwadudu vya kuteketeza mazalia ya Mbu vinavyozalishwa katika Kiwanda cha Tanzania Biotech Products ili kukiwezesha Kiwanda hiko kupata soko la ndani la uhakika ikiwa ni pamoja na kuweza kurejesha mkopo uliotumika na Serikali katika ujenzi na uwekezaji wa kiwanda hicho,

c) Wizara ya Afya, kuhakikisha inatenga fedha (own source) kwa ajili ya ununuzi wa Viuwadudu vinavyozalishwa katika Kiwanda cha Tanzania Biotech Products ikiwa ni pamoja na kuhisha Mkataba baina yake na Shirika la Taifa la Maendeleo kuhusu ununuzi wa Viuwadudu,

d) Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) ihakikishe inaziagiza na kuzisimamia Halmashauri zake zote zenye uwezo kwa kutenga bajeti ya ununuzi wa Viuwadudu vinazolishwa katika Kiwanda cha Tanzania Biotech kulingana kiwango cha tatizo la Malaria katika Halmashauri zao, na

e) Kitengo cha Biashara katika Shirika la Taifa la Maendeleo kifanye kazi ya kutafuta masoko kwa kushirikiana na TANTRADE ili dawa zinazozalishwa katika kiwanda cha Tanzania Biotech zifahamike na uuzika katika nchi mbalimbali.

3.2.12 Uwiano Usioridhisha wa Gharama za uendeshaji kwa Mapato

KWA KUWA, kumekuwepo na baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yanayotumia kiasi kikubwa cha mapato kugharamia matumizi ya Taasisi,

NA KWA KUWA, kushindwa kudhibiti matumizi ya Taasisi hizo kulingana na mapato yanayokusanywa kumesababisha Taasisi hizo kutokuwa na bakaa na kushindwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina izisimamie Taasisi zake na ihakikishe uwiano huu unaimarika na kutozidi ukomo wa Asilimia 50 uliowekwa

na Msajili wa Hazina ili Taasisi ziwe na fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake na kuongeza Mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

3.2.13 Uwiano Usioridhisha wa Faida kwa Mali

KWA KUWA, uwiano wa faida kwa mali wa baadhi ya Taasisi za Umma umekuwa si wa kuridhisha kutokana na mali zilizowekezwa kushindwa kuzalisha faida iliyotarajiwa,

NA KWA KUWA, kutokufanya vizuri kwa uwiano huo kunaashiria kukosekana kwa tija katika uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuzitaka Taasisi zote kufikia kiwango elekezi cha uwiano wa faida kwa mali kisichopungua cha Asilimia 15 ili mali zilizowekezwa ziweze kuzalisha faida iliyotarajiwa.

3.2.14 Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi

KWA KUWA, imebainika uwepo wa baadhi za Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi,

NA KWA KUWA, kukosekana kwa bodi za Wakurugenzi ambazo ndizo chombo kikuu cha maamuzi katika utendaji wa Taasisi kumechangia utendaji usioridhisha wa Taasisi hizo,

KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe michakato ya upatikanaji wa Bodi kwa wakati mara baada ya Bodi zilizopo madarakani kumaliza muda wake. Aidha, Msajili wa Hazina afanye mapitio ya viashiria vya utendaji (KPI) na kuona kama vinatekelezeka kwa upande wa Bodi na Menejimenti ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha pindi Mashirika yanapokuwa hayafanyi vizuri.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 *Shukrani*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri na msaada kwa kipindi chote cha mwaka mzima.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa.

Vile vile, napenda kumshukuru aliyekuwa Msajili wa Hazina Ndugu Athumani S. Mbuttuka kwa ushirikiano alioutoa kwa Kamati kwa kipindi chote alichohudumu kama Msajili wa Hazina. Aidha, napenda kumpongeza Ndugu Benedicto Mgonya kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Raisi na kuteuliwa kuwa Msajili wa Hazina. Vile vile, Kamati inamshukuru kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake na kuleta tija kwa Taifa ili kukamilisha dhima ya Serikali kufanya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma wakiongozwa na Mkurugenzi Idara ya Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo

na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jerry William Silaa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. George Natany Malima, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb-Mjumbe
8. Mhe. Dorothy George Kilave, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Haji Amour Haji, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Sanya Jusa Jaffar, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Silyvestry Francis Koka, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Dr. Pius Stephen Chaya, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Condester Michael Sichwale, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nanelwa J. Mwihambi kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Shukran kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athumani Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Mswige Bisile na Makatibu wa Kamati Ndugu Zainabu Mkamba, Ndugu Mwajuma Ramadhani na Ndugu Dismas Muyanja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Modesta Kipiko. Pia

tunawashukuru Watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphine Tamba na Ndugu Matamus Fungo pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

4.2 *Hoja*

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ni matokea ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo ulete tija kwa Taifa.

Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma, na kuijadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili hatimaye Serikali iyafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Jerry William Silaa, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

16 Februari, 2022

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante hoja imeungwa mkono sasa tunaanza mjadala mchangiaji wetu wa kwanza ni Dkt. Faustine Ndugulile jandae Dkt. Christine Mnzava.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na niwapongeze sana watoa hoja wote wamewasilisha vizuri sana na mimi nilitaka nichangie katika

hotuba ambayo, imewasilishwa na Kamati ya Bajeti na hususani nataka nijielekeze katika kipengele ambacho aligusia daraja la *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakazi wa Kigamboni tuna daraja linaitwa daraja la Nyerere ama kwa jina limezoeleka kama daraja la Kigamboni. Daraja hili limeanza kutumika tangu mwaka 2015 na limekuwa ni daraja pekee ndani ya nchi yetu ambalo linatozwa tozo kwa mwananchi kuvuka. Wananchi wa Kigamboni hawana mbadala ili mwananchi wa Kigamboni afike mjini aidha apite *Ferry* ambako anapanda pantoni, analipa tozo au inabidi apite darajani kwa mguu ama kwa wale ambao wana magari na vyombo vya usafiri lazima alipe tozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, daladala moja ambayo inavuka pale inachajiwa kati ya shilingi 5,000 kwa kila *trip* ambayo inavuka pale zikiwa *trip* 10 za kwenda na kurudi hiyo ni shilingi 100,000. Kwa hiyo, wananchi wa Kigamboni wanakosa usafiri wa njia *route* ndefu ambazo wananchi wakazi wa maeneo mengine wanazipata. Mwananchi wa Kigamboni ili afike mjini anahitaji nauli tatu mpaka nne tofauti na wakazi wengine wa Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kigamboni wamenituma kuulizia wamesikia kauli ya Serikali kwamba daraja la *Tanzanite* litakuwa bure, wakati wakazi wa Kigamboni wao ambao wanajiita ni masikini wanatozwa tozo ili waweze kuvuka kwenda mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawana mbadala kama walivyo wakazi wengine wa Oysterbay na Masaki ambao, wana barabara ya *Salender* sisi ukipita kwenye Kivuko na ukipita darajani ni lazima ulipie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kigamboni wameniomba niwaulizie kwa niaba yao je, ni kwa nini tu peke yao ambao ni daraja pekee, ambao wanapaswa kulipia na wakati wananchi wa Kigamboni wanachangia katika ujenzi wa madaraja mengine. Hata kama hili daraja limejengwa

kwa mkopo wa Wakorea na ninatambua kwamba daraja lile la Kigamboni limejengwa kwa mkopo kutoka *NSSF*. Kwa nini Serikali isilibebe kama inavyobeba mikopo ya madaraja mengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali ilichukulie suala hili kwa uzito unaostahili wananchi gharama za maisha/ wananchi wa Kigamboni ni, kubwa sana na wananchi wa Kigamboni hawana mbadala wa kwenda mjini zaidi ya kupitia kwenye Kivuko na kutumia daraja. Tofauti na wakazi wengine wa Masaki, *Oysterbay* ambao wana barabara mbadala ya kuweza kupita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kwamba Serikali itafakari kuondoa tozo katika daraja lile la Kigamboni Serikali ibebe mzigo wa deni lile la *NSSF*, ili na wananchi wa Kigamboni nao wapate nafuu ya gharama za maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Dkt. Christine Mnzava jandae Subira Mgalu jandae Mheshimiwa Vuma.

MHE. DKT. CHRISTINE C. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi na mimi kuweza kuchangia katika hoja ambazo zimewasilishwa, nitakwenda kujikita kuchangia katika hoja iliyowasilishwa na Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma. Tumeona katika taarifa iliyotolewa kuna baadhi ya changamoto ambazo zinakabili haya Mashirika ya Umma ambayo yamewekeza. Katika changamoto mojawapo ni Taasisi kutofanya kazi kwa pamoja kumekuwa na sintofahamu ya Taasisi mbili za Serikali, ambazo moja imewekeza lakini moja inasaidia nyingine kuweza kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kuna Shirika la *TANESCO* pamoja na *STAMICO*. *STAMICO* tunajua kwamba ni Shirika la Serikali na limewekeza zaidi ya asilimia 99 ya mtaji

na katika ndani ya Shirika la *STAMICO*, kuna *Stamigold* ambao wana kiwanda cha madini Biharamulo. Tatizo ambalo linatokea ni kwamba *Stamigold* ili kuendesha shughuli zake linahitaji umeme mkubwa sana karibia *unit* 1,300,000. Lakini tatizo lililopo ni kwamba *Stamigold* hawajaunganishwa na *grid* ya Taifa wanajikuta kwa mwezi, gharama ya kuendesha mitambo na gharama ya uchimbaji na uchenjuaji inatumia zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kununua mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama TANESCO wangeweza kuwaunganishia umeme *grid* ya Taifa, wangeweza kuokoa takribani shilingi bilioni 8 kwa mwaka kwa gharama ya mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua kwa sasa hivi lita ya mafuta ya dizeli ni Shilingi 2,500/= *Stamigold* wanatumia zaidi ya lita 600,000, kwa mwezi kwa ajili ya kuendesha mitambo na kwa ajili ya kufua umeme ili waweze kufanya kazi zao. Sasa basi, kama kunakuwa kuna mahusiano mazuri ya Taasisi mbili za Serikali ambazo zina lengo moja kuhakikisha kwamba, Tanzania yetu inakuwa na uchumi imara TANESCO wangepanya juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba wamewaunganishia umeme kwa *grid* ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshafuatilia sana lakini hata *STAMICO* wameshafuatilia sana suala hili. Mkienda maeneo ya tukio mkienda kwenye ule mgodi wakisikia Kamati inakwenda ndio mnakuta *TANESCO*, wameanza kuweka vifaa vyao wamechimba kama futi 2 tu mkiondoka shughuli inasimama sasa tatizo ni nini? Kwa sababu, Mashirika mawili ya Umma yanapofanya kazi pamoja tija na ufanisi vinaonekana dhahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Taasisi za Serikali ambazo zinategemeana kwa namna moja ama nyingine zihakikishe kwamba, kunapokuwa kuna uhitaji wa Shirika la *STAMICO/Stamigold* wanahitaji *TANESCO* ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi basi; ni vizuri Taasisi/mamlaka ambazo zinahusika kuhakikisha kwamba wanasaidia/

wanawezesha Shirika moja kufanya kazi zao kwa ufanisi.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kabisa kwamba kunapokuwa na gharama kubwa za uendeshaji faida inakuwa kidogo. Kwa mwaka 2019/2020 *STAMICO* iliweza kutoa gawio la shilingi bilioni 1.1 kwa maana hiyo basi kama uendeshaji utapungua kwa kuwa na umeme wa uhakika, kutoka kwenye *grid* ya Taifa ni dhahiri kwamba hata gawio la Serikali litaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama *STAMICO/ Stamigold* wanatumia gharama kubwa au Shirika lingine lolote lile linatumia gharama kubwa kwenye uendeshaji, ni dhahiri kwamba lazima itapata hasara. Kwa sababu matumizi ya uendeshaji yanakuwa juu sana kwa hiyo, niwaombe sana sana Taasisi kutimiza wajibu wake kurahisisha utekelezaji wa Mashirika mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Subira Mgalu jia ndae Augustine Holle Vuma.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa hizi kwanza nawapongeza Wenyekiti wote wawili wamewasilisha vizuri. Lakini mchango wangu utajielekeza kwenye Kamati yetu ya Bajeti naunga mkono hoja, nampongeza Mwenyekiti na yote ambayo yamezungumzwa ndani ya taarifa yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu jioni ya leo utajielekeza kwenye tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha miezi sita Julai mpaka Disemba, 2021. Kupitia tathmini hii naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuweza kukusanya mapato ya zaidi ya shilingi trilion 18.11 ikiwa ni asilimia 49.6. na; katika muktadha huu nichukue fursa hii kuipongeza sana Mamlaka ya Mapato

Tanzania (*TRA*), kwa kukusanya mapato ya zaidi ya shilingi trilioni 11 ikiwa ni asilimia 98. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee kwa mwezi wa 12 kukusanya na kusajili kiwango kipya cha makusanyo ya shilingi trilioni 2.5 ambacho ni kiwango kipya, tangu Mamlaka hii imeanzishwa mwaka 1995 ni mapato ya juu kabisa kukusanywa tangu imeanzishwa miaka 26 iliyopita. Kwa hiyo, naipongeza sana *TRA* na Wizara ya Fedha kwa juhudi kubwa lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan, kwa maelekezo yake kwa Mamlaka hii ya Mapato *TRA* kukusanya mapato kwa ueledi, uadilifu na uwajibikaji. Lakini sambamba na hilo yapo mapato ambayo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliwasilisha kwenye Kamati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambazo ni za eneo hili la mapato ambazo hazijafungwa zaidi ya shilingi trilioni 356. Kwa maana hiyo Serikali yetu kupitia *TRA* na Wizara ya Fedha inayo nafasi ya kuvunja rekodi yake kila wakati, endapo itajielekeza kuhakikisha Wizara zinakusanya shilingi bilioni 546 ambazo hawajakusanya. Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 113 Taasisi za Kiserikali shilingi bilioni 6 lakini pia hata zile kesi ambazo zipo kwenye Mahakama ya juu ya Rufani za Kodi. Endapo Serikali itaiwezesha ina uwezo wa kukusanya mapato zaidi na kuiwezesha Serikali, kila wakati hii Awamu ya Sita kuvunja rekodi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kupitia Mamlaka hii ya *TRA* naomba niiombe Serikali kwa kuwa imeonyesha jitihada kubwa, za kukusanya mapato ikamilishe zoezi la ajira za wafanyakazi 1,000. Kama Balozi wa Kodi naishukuru *TRA* na Wizara ya Fedha tumetembelea Mikoa, ya Kanda ya Kaskazini tumetembelea mipaka yetu Tarakea, Holili lakini na Namanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kwa kuwa makusanyo ya mapato zaidi ya asilimia 45 yanatokana na ushuru wa forodha; na kwa kuwa chanzo hiki kinafanya kazi vizuri niiombe Serikali iboreshe miundombinu. Kwa mfano

katika mpaka wa Tarakea Rombo unayo nafasi ya kuchangia mapato kiwango cha kutosha, lakini kwa kweli miundombinu haitoshelezi ikiwemo majengo, uhaba wa watumishi na uhaba wa vitendea kazi. Lakini sambamba na hilo niendeele kuiomba Serikali kuimarisha mifumo ya kukusanya kodi kupitia TEHAMA. Natambua jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika eneo hili la TEHAMA, lakini itawezesha wananchi na walipakodi kulipa kodi kwa ueledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo tulipokea salamu za walipakodi wa Mkoa wa Arusha wakimpongeza Rais mama Samia pamoja na Mamlaka ya TRA. Kwa namna ambavyo kwa sasa hivi TRA imekuwa *facilitator* wanakaa pamoja wanazungumza, wanawezesha shughuli za kiuchumi ziendeele lakini wakati huo huo shughuli za kulipa kodi ziendeele. Kwa hiyo, nampongeza sana Kamishina wa TRA nampongeza sana Waziri wa Fedha na watendaji wote kwa kuwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwaombe watazania tuendeele kulipa kodi kwa hiyari tuendeele kudai risiti na wale wafanyabiashara waendeele kutoa risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuendeele kubainisha vitendo ambavyo vinapelekea kukwepa kodi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho niipongeze sana Serikali na Mheshimiwa Rais mahususi, kwa namna ambavyo mkopo wa shilingi trilioni 1.3 ulivyofanya kazi nzuri katika maeneo yetu. Kwa Mkoa wa Pwani tulipokea shilingi bilioni 17 tumepata madarasa 530 sasa hivi tumejielekeza kwenye miradi ya sekta ya afya, sekta ya maji.

Kwa hivyo, kwa kweli na kama Kamati ilivyosema namna ambavyo mkopo huu ulisimamiwa kila mmoja, kwa nafasi yake tunayo nafasi ya mikopo mingine nayo kutoa tija nzuri na masuala mbalimbali. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Vuma jiandae Mheshimiwa Bulaya.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii awali ya yote naunga mkono hoja zote mbili na ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwenye ziara zake hizo za Ufaransa na Ubelgiji tumeona anasaini mkataba, wa mabilioni ya shilingi ambayo tunaamini yatakuja kwenye Taifa letu na hatimaye itakuwa ni hatua muhimu sana kuwasaidia watanania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea maeneo mawili kwenye taarifa yetu eneo la kwanza ni kwenye kiwanda cha viuatilifu kile ambacho kipo kwenye Mkoa wa Pwani. Naanzia hapo kwa sababu ni kiwanda mahususi ambacho kilianzishwa kwa ajili ya kutokomeza malaria na kwa miaka kumi, ukianza mwaka, 2010 mpaka mwaka, 2020 tumepoteza watanania zaidi ya 70,000 kwa sababu ya ugonjwa wa malaria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni Majimbo kadhaa ya uchaguzi tumeyapoteza. Mwaka 2015 *NDC* Shirika letu lilichukua mkopo ambao ni takribani shilingi bilioni 50 kutoka Hazina kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa kiwanda hiki. Kiwanda ambacho kilijengwa na kukamilika mwaka 2017 kiwanda walisaini mkataba na Wizara ya Afya kwa maana ya kwamba Serikali, kupitia halmashauri itakuwa inanunua viuatilifu hivi na kwenda kupulizia huko kwenye mazalia ya mbu ili kutokomeza mbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikueleze ule mkataba haujatekelezwa, kiwanda hakiuzi viuatilifu, ni kama kimatelekezwa, tunajuliza kuna hujuma au kuna nini katika hili? *Over 50 billion!* Serikali inatumia mabilioni ya shilingi kila

mwaka kwa ajili ya kupambana na malaria. Kwa nini tusiende kununua viuatilifu hivi tukapuliza hatimaye tuondokane na tatizo la malaria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamaica wameondokana na malaria kwa sababu ya kutumia teknolojia hii ambayo walitupa nasi, tulinunua kwao. Kiwanda kile hakina faida hiyo tu kwa maana ya kwamba ni viuatilifu vya kupambana na malaria. Kamati tumetembelea pale walituambia kwamba kiwanda kile kina uwezo wa kutengeneza viudadudu (*pesticides*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inatumia mabilioni ya shilingi kila mwaka kwa ajili ya kununua viudadudu kwenye masuala mbalimbali, nchi hii inatumia bilioni 57 kila mwaka kununua viudadudu kwa ajili ya zao la pamba, inatumia bilioni 50 kwa ajili ya kununua viuatilifu kwa ajili ya zao la tumbaku na inatumia karibu bilioni 100 kila mwaka kwa ajili ya kununua viua wadudu kwa ajili ya zao la korosho. Ni mabilioni haya ambayo kila mwaka tunayapeleka nje ya nchi wakati tuna kiwanda na teknolojia hapa, kama tukikipa uwezo, tukawekeza pale, Serikali isikitelekeze, tunaweza tukaokoa mabilioni ya shilingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nigusie kidogo kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwanza Mheshimiwa Naibu Spika hongera sana kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tunajua wanafanya biashara, lakini wanaenda kuwekeza zaidi kwenye *real estate* mabilioni ya shilingi wanapeleka yote kwenye *real estate*, wanajenga majengo hata majengo yenyewe hawayamalizi, wanaenda kujenga majengo porini kama lile la Dege *Beach* kule Kigamboni ambayo *return* yake hakuna, wameshindwa na ku-*prove failure* kwenye *real estate*. Hela za Watanzania zimewekwa kule, zimefia kule. Sasa sijui ni woga, wakitoka hapo wanaenda kwenye mambo ya *investment* kwenye mambo ya *bonds* hapo wanashindana na Wabunge na Watanzania wengine

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwenda kununua *bonds*! Hawa wanapaswa wawaze vitu vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *real estate* ina *players* wengi, *TBA* wapo humo ndani, *National Housing* wapo humo ndani na akina Musukuma wapo humo ndani, akina Kishimba wapo humo ndani na wawekezaji wengine wengi, waachane na *real estate*, waende kuwekeza kwenye vitu ambavyo vina faida kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo la mbolea hapa Tanzania kila mwaka, *NSSF* wakiamua kumaliza tatizo hili wanaweza, watujengee kiwanda kikubwa cha mbolea hapa ambacho kinamaliza shida ya mbolea Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo shida ya sukari, tunazo shida kwenye mambo mbalimbali, kwa hiyo nadhani mashirika haya...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa. Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ninapenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hata hizo *real estate* zinazowekezwa na Taasisi za Serikali zinakuwa nje ya soko kwamba tunayo maeneo ndani ya mji ambayo wanaweza wakajenga na kupata wapangaji, wanazitoa wanaenda kuzi-*dump* ili wapige *deal* halafu na nyumba hazipati wateja. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuma taarifa hiyo.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea, naamua kukubali kwa sababu ni Mheshimiwa Musukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, hawa watu wajielekeze kwenye vitu, leo hii Mama amewapa hela nyingi sana, juzi tu hapa, walikuwa na madeni Serikalini, kawapa *over two trillion* siyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanatakiwa waende kumsaidia kutengeleza ajira, waende kwenye *investment, business model* ambayo inatengeneza ajira mbalimbali kwa Watanzania, haya mashirika yanayo nafasi ya kutusaidia, kumsaidia Mama kutengeneza ajira kwa Watanzania. Kwa hiyo waachane na vitu vidogo vidogo hivi ambayo hata vyenyewe vimewashinda, waende kuwekeza kwenye mambo makubwa ambayo yataleta faida ya kiuchumi pia na kuongeza ajira kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono tena hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bulaya, ajiandae Mheshimiwa Kandege.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Liganga na Mchuchuma limeongelewa tangu Bunge la Nane, tuko Bunge la Kumi na Mbili. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa maslahi ya Taifa letu tusikubali tukakamilisha kipindi chetu cha Ubunge bila Mradi wa Liganga na Mchuchuma kufanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Viwanda na Biashara ilieleza vizuri, Kamati yetu tumeeleza vizuri, huu mradi ni wa muda mrefu, leo tunaambiwa kuna Kamati inaangalia ni namna gani labda waachane na Mwekezaji au kupitia mkataba mpya. Huyu Mwekezaji ameshindwa kuwekeza hana mtaji wa dola za Kimarekani bilioni 2.9, hana! Tunabembelezana naye kwa nini? Mpaka sasa hivi tunavyozungumza alitakiwa amalize kujenga kiwanda cha chuma, alitakiwa amalize kujenga miundombinu ya umeme,

alitakiwa alipe fidia ya wananchi watakaopisha ule mradi, ameshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ipo wazi Kifungu Na. 47(1), twendeni ukurasa wa 123 unasema wazi kwamba mtu akipewa leseni ya uchimbaji anatakiwa ndani ya miezi 18 awe ameshachimba na kuendeleza, niwaulize Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ni miezi 18 mingapi imepita tangu Bunge la Nane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu sijawa Mbunge enzi ya Mama Mary Nagu tunazungumza Liganga na Mchuchuma! Mungu atupe nini? Leo hii tunaagiza chuma nje wakati chuma kipo kimelala pale, bado tunafikiria kuendelea na Mwekezaji huyu, sheria zetu za nchi zinatulinda na kwenye taarifa yetu tumesema, lazima Serikali muwe makini na kuangalia mitaji ya wawekezaji wanaokuja kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunazungumzia Kamati inaangalia! Tunamlinda nani? Hivi kweli kwenye uwekezaji mkubwa wa namna hii wenye maslahi ya Taifa letu hatujui uwezo wa mwekezaji? Zaidi ya miaka kumi inapita hana dola za Kimarekani bilioni 2.9! Wananchi kule wa Ludewa wamekaa wanashindwa kuendeleza maeneo yao. Tunaomba Bunge la Kumi na Mbili lisiingie kwenye historia zingine, twendeni tulitendee haki Taifa letu, twendeni tukaweke historia kwamba kulikuwa kuna Bunge la Kumi na Mbili lilifanya maamuzi ya kuhakikisha uchumi wa nchi yetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu tumezungumzia kuhusiana na kampuni ya uagizaji wa matrekta, hii ilikuwa tangu Awamu ya Nne, matrekta 2400 kutoka Poland, tangu enzi za Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda. Hata hivyo, mpaka leo yamekuja matrekta 800, matrekta 1,774, mabilioni ya shilingi pesa za walipakodi hayajafika. Ni aibu nikisema hapa tumeuliza kwenye Kamati wanasema, eti Kampuni imefilisika, yaani imefilisika kabla haijamaliza kuleta matrekta yetu? Tuna uwezo gani wa kugundua uwezo

wa watu tunaolingia nao mikataba? Yaani ameleta matrekta 800 kampuni imefilisika, matrekta ya Watanzania ambayo yangesaidia wakulima wa nchi hii 1,774 hayajaingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili, Kamati yetu ya uwekezaji tuliopewa jukumu la kusimamia pesa za walipakodi katika uwekezaji vitu kama hivi hatutaruhusu. Tunaitaka Serikali ije na majibu ya kina, matrekta ya Watanzania 1774 yatakuja lini? Haituingii akilini, watu wameingia tenda, wamesaini mikataba baada ya kuleta matrekta 800, baadaye kampuni ikafilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *EPZ*. Tulipiga kampeni sana na tukatoa maeneo mbalimbali, tukatenga maeneo ya uwekezaji, leo hii *EPZ* ingefanya vizuri tatizo la ajira nchi hii ingekuwa historia. Hivi ninavyoongea kati ya Kanda 15 ni Kanda tatu tu zimeweza kuwekezwa, Kanda 12 wananchi wametoa maeneo yao hawajalipwa fidia na tumeambiwa *EPZA* iko kwenye ukwasi, ni kwa sababu Serikali haipeleki pesa za kutosha kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wamesimama hawaendelezi maeneo yao. Kwa nini tunatafuta ugomvi na wananchi? Kwa nini tusiende kuchukua maeneo tunayoweza kuwekeza? Kanda 12 wananchi wamechukuliwa maeneo yao uwekezaji haujaanza halafu tunaimba ajira kwa vijana wa nchi hii wakati tunajua ni maeneo gani tunaweza tukafanya vizuri na tatizo la ajira nchi hii likapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mheshimiwa Vuma amezungumzia kwenye suala la uwekezaji, naomba nizungumzie ni namna gani Serikali hawalipi madeni, hawapeleki michango ya wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza *ATCL* tangu mwaka 2008 mpaka 2016 hajapeleka michango ya wanachama, inadaiwa bilioni 16 hawajapeleka *PSSF*. Hizi ni

pesa za watumishi wa nchi hii, walikatwa kwa ajili ya maisha yao baada ya utumishi wa nchi yao wanayoipenda sana. Nimesikia habari kwamba hawajalipa hizo pesa eti wanafanya mazungumzo wasilipe riba, *come on!* Pesa za watu walizochanga, ile siyo benki, ni pesa za wafanyakazi wa nchi hii waadilifu, wamekatwa zaidi ya miaka kadhaa ili waweze kupata manufaa baada ya kustaafu. Hapa kuna watu wamestaafu hawajalipwa pesa zao kwa sababu michango haijapelekwa, bilioni 16! Kuna watu wamekufa, kuna watu bado wanaendelea na kazi kwa uadilifu na uaminifu lakini michango yao haijapelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hili suala kwenye vyombo vya habari, nilisema hili suala kwenye maeneo mengine, tunaomba pesa za wastaafu ziende.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba tathmini ya Mifuko imefanywa na iko Serikalini huu mwezi wa Tisa hamtaki kusema *status* ya mifuko ikoje na nimepata taarifa mmeanza kupunguza madeni ya Mifuko...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante dakika saba zimekwisha. Mheshimiwa Josephat Kandege, jandae Mheshimiwa Issa Mtemvu.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami jioni ya leo niweze kuchangia. Naomba nipongeze taarifa zote za Waheshimiwa Wenyeviti, ni taarifa njema kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, nimeshiriki katika kutoa michango na kwa siku ya leo nitaomba nitoe michango katika eneo moja tu. Ni ukweli usiopingika tumekuwa tukisema Bunge la Kumi na Mbili ni lazima liache *legacy* na litaacha

legacy kwa kuhakikisha kwamba Serikali inasukumwa kwenda kuwekeza katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pato la Taifa trilioni 163.88 sekta ya kilimo imekuwa ikichangia kwa trilioni 44.8 ambayo ni sawa na asilimia 26.9 ya pato la Taifa. Ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania zaidi ya asilimia 66.3 nguvu yao yote iko kwenye kilimo. Kipekee naomba nipongeze Ubalizi wa Tanzania nchini China kwa kazi kubwa nzuri sana ambayo wamefanya katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na mkataba kati ya Tanzania na China wa kuuza zao la soya. Pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Balozi Kairuki, kazi njema sana anastahili kupongezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ya Tanzania mikoa ambayo zao la soya linastawi ni pamoja na Mikoa ya Rukwa, Katavi, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Tanga na Kagera hasa Karagwe. Matumizi ya zao la soya ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, soya inatoa *product* nzuri sana ya maziwa ya unga pia inatoa mafuta mazuri sana *first class*, pia inatoa zao wanaita soya nyama kwa wale *vegetarian* ambao hawataki kutumia nyama, pia inatoa chakula kizuri sana kwa ajili ya mifugo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba kwa ku-*concentrate* katika zao hili ambalo tayari tuna soko la uhakika nchini China, tuna soko la uhakika India na Ulaya, ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba Serikali yetu inaenda kuwekeza kwenye kilimo kwa sababu manufaa ya kulima zao hili; moja, katika eneo ambalo umelima soya kama ambavyo ipo kwenye mazao ya mikunde ni kwamba inarutubisha ardhi na hivyo kupunguza matumizi ya mbolea za kemikali kwa asilimia hamsini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majirani zetu siku ile Spika alisema siyo vizuri kuzitaja nchi jirani lakini katika mifano mizuri naomba mniruhusu niseme. Pamoja na kwamba Tanzania ndiyo ambao tuna mkataba na China na tumefanya kazi

nzuri ya kusafirisha China, lakini ni ukweli usiopingika kwamba soya nyingi imekuwa ikipatikana kutoka nchi ya Zambia na Malawi, wakati Tanzania ndiyo tuna mkataba na China kuuza zao hili. Ifike wakati Serikali kuhakikisha kwamba inawezeza katika kupata mbegu bora ili hiyo mikoa ambayo nimeitaja ambayo zao hili linastawi na uhitaji kwa Mataifa ni mkubwa sana tuhakikishe kwamba zao hili linakuwepo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba tumekuwa na tatizo kubwa sana la mafuta ya kula, tuki-*concentrate* katika zao moja tu la alizeti tukaachia soya tutakuwa hatufanyi vizuri. Naiomba Serikali na ni wakati muafaka, kwa fursa hii na mkataba ambao tumeingia na nchi ya China kwa miaka mitatu tuhakikishe kwamba dola nyingi zinaingia Tanzania kwa sababu tunauza tunapata *forex*, tunakuwa na soko la uhakika badala ya sisi kuendelea kuhangaika na zao la mahindi. Kama ambavyo nimesema inasaidia sana katika kurutubisha ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba Serikali kuhakikisha kwamba inakuwepo mbegu bora ambayo wenzetu wanazo. Kwa mfano, kwa nchi kama Zambia wana aina saba za mbegu, wana mbegu aina ya *spike*, wanayo mbegu aina ya *safari*, wanayo mbegu aina ya *dina*, Tanzania hatuna mbegu hata moja. Naomba kipekee nipongeze Wabunge ambao wamekuwa vinara akiwepo Mheshimiwa Msongozi amehangaika sana kutafuta mbegu ili kuweza ku-*supply* katika maeneo yake na Wabunge wengi ambao walikuwa na nia ya kuweza kusaidia maeneo yao, lakini kwa sababu hatuna mbegu Tanzania na tumekuwa tukikumbana na vikwazo vingi tungeweza kusaidia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Issa Mtemvu.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie sekunde hii moja kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 42, lipo jambo linazungumzwa na Kamati juu ya Daraja la Tanzanite. Daraja hili ni furaha ya Tanzania kupata mkopo wa dola milioni 121, shilingi za Kitanzania kama bilioni 243. Hili ni daraja zuri lakini tunatambua umuhimu wa daraja lile limekuwa ni mbadala wa daraja lililokuwepo siku zote pale ambalo limekuwa likisaidia wananchi, lakini vilevile palikuwa na foleni kubwa.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hili siyo daraja la kwanza kupatikana kwenye nchi yetu. Dar es Salaam lipo daraja lingine zuri Kigamboni ambapo mwaka 2015 lilijengwa chini ya Shirika letu la *NSSF* kwa shilingi bilioni 214 tofauti ya bilioni kama 30 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wengine waliotangulia kusema leo kwamba tunaendelea kuwa na mshangao juu ya faida zote ambazo zinaonekana juu ya daraja lile. Daraja la Kigamboni toka limejengwa kama mbadala wa wananchi wa kule tayari limewekewa tozo, wananchi wale upande mmoja walikuwa wakilipa tozo za kawaida vilevile daraja lilipokuja kuwa mbadala wakaendelea kulipa tozo. Sababu kubwa ilikuwa ni fedha zetu wenyewe kutoka katika Shirika letu la *NSSF* ambalo limewekeza pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la sasa hivi ni mkopo ambao tunajua bilioni 243 linaenda kuwa deni la Serikali, deni ambalo kila Mtanzania ana nafasi ya kulilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sababu kama mbili tu au tatu za kutofautisha watu wa Kigamboni na lile daraja la pale na wale watu wanaopita, kuna hali kama mbili. Moja, ni umasikini. Ukiangalia upande wa Kigamboni, viashiria vyote vya kimasikini vipo kule. Hali ya umasikini, hata matumizi ya kaya kwa siku, utaweza kutofautisha na watu wa *Oysterbay*, Masaki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama waliotangulia walivyosema na kushauri, ni vizuri. Mimi nishauri katika eneo hili; kama Kigamboni katika nyanja zote hizo mbili, madaraja yote mawili, wanalipa tozo, basi na huku walipe tozo. *Option* ya pili, kama ni lazima sana, au sisi ambao hatujui kwa huku hawalipi na kule wanalipa, basi wananchi wa upande wa kule kwenye kaya nyingi za masikini wasilipe tozo katika upande mmoja; na upande wa daraja waendeleo kulipa yale magari yanayopita. Inaweza ikawa ni njia nzuri ya kusaidia malalamiko makubwa ya watu wa Dar es Salaam na wananchi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze sana kwenye upande wa *TARURA*. Wakati wa nyuma hapa kidogo katika kutafuta mapato kwa ajili ya barabara zetu vijijini na mijini chini ya *TARURA*, tuliingiza tozo ya mafuta (petroli na dizeli) shilingi 100/=, tukatarajia kupata shilingi bilioni 322. Ni kweli katika fedha hizo mpaka sasa zimeshatumika, zimetolewa takribani 43%, jambo zuri na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha hazitoshi. Mpaka juzi hapa, Bunge letu hapa likatoa kauli, *TARURA* waje na tathmini ya nchi nzima kwa kuokoa hali ya barabara zilizoharibika. Tathmini imekuja na Kamati imeeleza, takribani shilingi bilioni 119 wanazihitaji, lakini shilingi bilioni 119 wanazitoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 wamepangiwa shilingi bilioni saba na nyongeza ya shilingi bilioni moja ambayo wametoa katika *reallocation* ya ndani ambayo kwa kuongezea wamefikia shilingi bilioni nane. Hii ndiyo dharura kwenye bajeti ambayo tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona hali ya hatari ambayo tunayo kwenye barabara zetu. Sasa Kamati inaeleza, ongezeko ni shilingi bilioni 111, zinatoka wapi? Maana yake nini? Zinaenda kudhuru bajeti iliyopitishwa na Bunge hili. Shilingi bilioni 111 ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kwa sababu hatuwezi kuendelea hivi kudhuru bajeti ambazo tunakaa kama Taifa tunapitisha, lakini leo tukafanye *reallocation between votes*, tukanyang'anye katika mafungu mengine ya Wizara ili tuweze kufanya jambo la dharura katika hili. Sasa, nini cha kufanya? Kuna mambo mawili: Moja, katika eneo hili ni vizuri tupeleke fedha zaidi ya shilingi bilioni 100 kwenye bajeti yetu inayokuja 2022/2023 kama dharura; eneo la pili kwa sentensi moja, ni kutafuta vyanzo vingine. Dar es Salaam kule tunahitaji *GN...*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Malizia malizia.

MHE. ISSA J. MTEMVU: ...ije haraka ili tuweze kutatua barabara za ndani kama ilivyo miji 45 katika mikoa mingine ambavyo wametatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Dkt. Oscar Kikoyo, jandae Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Abdallah.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami niungane na Wabunge wengine kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Katika ripoti yetu tumeangalia mashirika mengi, lakini nasikitika kusema mashirika yetu mengi hayafanyi kazi vizuri. Tatizo mojawapo, katika ripoti yetu tumeainisha, ukosefu wa mtaji ni tatizo kubwa kwenye mashirika yetu na nijikite kwenye *TPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPA* kwa uchumi wa nchi yetu na kulingana na jiografia yetu na nchi zinazotuzunguka,

kusema kweli ni *cash cow* yetu. Hata hivyo, ukiangalia mtaji walionao na uwekezaji wetu na jiografia yetu, nchi zilizotuzunguka zinazohitaji huduma yetu, kulingana na ripoti yetu ambayo tumewasilisha hapa, tumesema *TPA* utendaji kazi wake ni mdogo kwa sababu hawana mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia vifaa walivyonavyo ni vya karne iliyopita, siyo vya karne hii. Tanzania siyo peke yetu; au Bandari ya Dar es Salaam siyo peke yake katika ukanda huu. Tunazo bandari nyingi ambazo tunashindana nazo. Kama tuna vifaa hafifu ambavyo vina teknolojia hafifu, hatuwezi kushindana na bandari za nchi zilizo karibu kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Tutaachwa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, Serikali i-*commit* hela ya kutosha kwenye Bandari ya Dar es Salaam ili tuweze kuhudumia mizigo ambayo nchi jirani wanapitisha kwetu. Vinginevyo washindani wetu watatuacha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, bandari hiyo ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Ikama yao ni wafanyakazi 3,196, lakini waliopo mpaka leo tunapoongea ni wafanyakazi 2,512. Wanao upungufu wa wafanyakazi 1,404 tunashindwa wapi? Kama hiki ndicho kitega uchumi cha uhakika tulichonacho, tukiwekeza vya kutosha, tuna uhakika wa kutengeneza fedha za kutosha kutusaidia kupunguza matatizo kwenye bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishakuwa na wafanyakazi wachache, ukawa na mtaji mdogo, madhara yake ni kwamba tunatumia muda mwingi kuhudumia meli na matokeo yake hawa tunaowachelewesha kupakua mizigo yao, tunawalipa fidia na hizo gharama zote zinapelekwa kwa mlaji na matokeo yake ni nini? Bidhaa inayopitia kwenye Bandari ya Dar es Salaam haiwezi kushindana na bidhaa nyingine. Itakuwa ni ya bei ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie na Taasisi inayoitwa *TASAC*. Wakati Sheria ya *TASAC* inapitishwa hapa, wengi tuliipigia kelele, lakini tukaipitisha kama Bunge. *TASAC* anafanya kazi ya udhibiti, lakini wakati huo huo anafanya kazi ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani hii. Kwetu huku tunasema ni sawa sawa na kuchukua rubisi ukachanganya na konyagi, haiwezekani. Kama ni mdhibiti, afanye kazi ya udhibiti na tuunde taasisi nyingine ya kufanya biashara ambayo inafanywa na *TASAC*. Mdhibiti afanye kazi ya udhibiti na tuwe na kampuni nyingine tofauti na *TASAC* ambayo itafanya kazi ya *clearance*, kazi za kusafirisha kidogo kidogo na kutoa mizigo, lakini hizi kazi mbili lazima tuzitenganishe, hatuwezi kuendelea hivi. Vinginevyo tunabaki kama kichekesho tu katika uchumi wa soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond, jandae Mheshimiwa Hamida Abdallah.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia jioni hii. Kipekee nakupongeza sana kwa nafasi hiyo ya Unaibu Spika, kwa kweli Kiti kimepata mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa ajili ya jambo moja tu; mengi ningeweza nikayasemea, lakini hili naliona ni muhimu sana, nalo ni lile la *Universal Health Coverage Insurance*. Toka lile Bunge lililopita tulizungumza hapa kwamba Serikali italeta Muswada ili tuweze kupitisha sheria ya kuwa na Bima ya Afya kwa Wote. Jambo hili limeleta kigugumizi, hatuoni kama Serikali iko tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba, kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amejitahidi kutoa na zile fedha za *UVIKO 19* zikaenda kumalizia zile *dispensaries*, vituo vya afya na kuboresha hospitali zetu, lakini jambo hili la *insurance*

kwa wote limeleta kigugumizi. Kwa kupata fedha zile na kumaliza majengo bado hakutakuwa na sababu yoyote, yaani hakutakuwa na *impact*. Unaweza ukawa na majengo mazuri na hospitali nzuri, lakini wale watu wanaopatiwa huduma wasipatiwe; na wengi wao ni wananchi wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *data* zilizoko kwenye nchi yetu, tunaambiwa kwamba *National Health Insurance Fund* ni 8% na hii ni lazima, anakulipia mwajiri na wewe mwenyewe unachangia. Ikija kwenye *CHF* ni 23%, hiyo iko kwenye Halmashauri, tayari kuna watu wamejiunga kwenye vikundi vya Vikoba, watu wamejiunga kwenye vikundi vya Kiarano, vikundi vidogo vidogo, lakini wanapata shida kupata huduma. Inakuwaje hiyo? *Private sector* ni 1% tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuiomba Serikali yangu Sikivu, jambo hili lifikiwe kwa kina, tutakapokuja Bunge lijalo sasa, Muswada huo uje hapa Bungeni tuweze kupitisha hii sheria. Wote hapa nyie Wabunge wenzangu ni mashahidi, kwa siku mnapata simu nyingi kusaidia matibabu kwa wananchi wenu. (*Hapa alikohoa kidogo*)

MBUNGE FULANI: Pole.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa na *insurance* hili lisingekuwa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga hoja mkono. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Hamida, halafu ajiandae Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa kuwa Msaidizi wa Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja zote za Kamati mbili ambazo zimewasilishwa. Pia nawapongeza Wenyeviti wote wawili kwa namna ambavyo wameweza kuwasilisha taarifa ya kazi ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *EPZ* ambalo mwanangu pale Mheshimiwa Ester Bulaya amelizungumzia, nami naomba niunge mkono hoja hiyo. Nizungumzie upande wa muundo wa Bodi ya *EPZ*. Ukiangalia muundo wa bodi namna ambavyo upo utaona kwamba, Kamati nzima ya bodi ina watu ambao ni wazoefu, wamebobeza katika taasisi mbalimbali. Utaona ya kwamba wameshindwa kuisaidia *EPZ* iweze kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasomee Waheshimiwa Wabunge waweze kujua. Mwenyekiti wa Bodi ni Waziri wa Viwanda na Biashara. Wajumbe wa Bodi; kuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Katibu Mkuu TAMISEMI, Katibu Mkuu Nishati, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Kamishna wa *TRA*, Kamishna wa Ardhi, Kamishna wa *TPSF* na Rais wa *TCCIA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaona namna ambavyo hawa ndugu zetu wanashindwa kuisimamia *EPZ*. Tunaamini kwamba, watu hawa Serikali iliwateua kwa kuwaona kwamba wangekuwa msaada mkubwa katika mamlaka hii ya *EPZ*, lakini tunaona namna ambavyo *EPZ* inashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPZ* ina miaka mitatu mfululizo haijapata fedha kutika Serikali kuu ya matumizi mengineyo. Sasa tunashindwa kuelewa chombo hiki Serikali imedhamiria kuwekeza viwanda mbalimbali ambapo vitazalisha bidhaa ambazo zingeweza kuingia katika ushindani wa masoko ndani ya nchi na nje ya nchi, lakini tunaona kwamba ajira kubwa kwa vijana ingeweza kuwepo katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPZ* wanashindwa kufanya kazi kwa sababu hawana fedha za kuwekeza katika *zones*

ambazo tayari walishajipanga nazo. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba, wanautazama upya muundo wa bodi, waone namna gani wataisaidia EPZ iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie katika suala la viwanda vidogo vidogo *(SIDO)*. *SIDO* imekuwa msaada mkubwa sana kwetu na tumeona namna ambavyo imewezeshwa wajasiriamali wengi kuingia katika uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo. Mwanzoni tumeona kwamba *SIDO* ilikuwa inafanya vizuri sana, lakini tunakokwenda *SIDO* inaonesha sasa maendeleo yake kushuka kwa sababu wanakosa fedha, vyanzo vyao vya mapato ni makusanyo yale ya ndani. Kutoka Serikali Kuu, kinachokwedna ni mishahara tu ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaona kuna kila namna sasa Serikali iitazame kwa macho mawili *SIDO*, kuhakikisha kwamba wanapewa fedha za kutosha ili waende kutoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali ili wananchi wetu waweze kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo. Pia tumeona uchakavu mkubwa katika maeneo ya majengo yao ambayo wanayakodisha. Kwa hiyo, tunaona sasa Serikali ina umuhimu wa kuwasaidia ndugu zetu wa *SIDO* ili waweze kwenda vizuri na waendeleo kutusaidia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongea sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ametutafutia fedha nyingi. Nami Jimboni kwangu nimepata fedha karibia shilingi bilioni 18 kutekeleza miradi ya maji, madarasa kwa maana ya sekta ya elimu, sekta ya afya na sekta ya barabara. Kwa hiyo, tuendeleo kumuunga mkono na kumwomba kwa Mwenyezi Mungu ili aendeleo kumuimarisha ili aweze kutekeleza mipango yake ya kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, jiandae Mheshimiwa Kwagilwa akifuatiwa na Mheshimiwa George Malima.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia kwenye taarifa hizi mbili za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nawapongeza Wenyeviti wetu wote kwa ripoti nzuri kabisa ambazo wamezi-*table* hapa. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na nitaenda kujielekeza kwenye *MSD*, pale ambapo Kamati ya Bajeti tulitembelea tukagundua changamoto mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa kwamba Taifa letu limekuwa likikumbwa na upungufu wa dawa kwenye hospitali na vituo mbalimbali vya kutolea huduma na suluhisho mojawapo ni haya ambayo nitaenda kuyasema, wala siyo yale ambayo Waziri alisema sijui kuondoa maduka ya dawa kwa mita 500. Unaweza kuondoa mpaka kilometa mbili, lakini bado kukawa na changamoto ya upungufu wa dawa, kama haya hayataweza kufanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo tumeshuhudia mlolongo wa utaratibu mzima wa ununuzi unachukua muda mrefu sana. Ni kwamba, mchakato wa zabuni tu unachukua miezi mitatu, baada ya pale kama unaagiza vitu kutoka nje itachukua miezi mitatu tena kufika baada ya kumaliza mchakato wa zabuni. Kama ni ndani ya nchi itachukua miezi miwili. Sasa ukijumlisha ni miezi mitano mpaka sita ili uweze kupata dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili tuweze kuepukana na huu mlolongo mrefu nilikuwa nashauri: moja, tuhakikishe Serikali inapeleka fedha kwa miezi minne walau mfululizo ili kukabiliana na huu mchakato mzima uweze kuji-*absorb* ndani kwa ndani kuhakikisha kwamba tunakuwa na *consistency* ya ku-*supply* dawa kwenye vituo vyetu vya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhakikisha kwamba, walau tuweze kubadilisha sheria ili kwa dawa zile muhimu. Mchakato wa zabuni usichukue miezi mitatu, ungechukua hata mwezi mmoja kuhakikisha upatikanaji wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, Sheria yetu ya Manunuzi ya Umma pia inatambua kwamba mzabuni mwenye gharama nafuu ndiye atakayepewa tenda, yaani bila kuangalia uhalisia wa bei ya gharama husika kwenye soko. Hii inasababisha baadhi ya wazabuni kuweza hata kula njama, *just a syndicate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, labda nataka ni-*supply let say, X-Ray machines* nyingi kwenye hospitali fulani na ninajua kabisa na John anafanya biashara hiyo na mwingine; unaweza ukawa na *syndicate* tu. Bei halisi kwenye soko unakuta labda ni shilingi milioni 50 kwa *X-Ray* moja, lakini sisi tuka-*bid*; nikaweka shilingi milioni 100, John akaweka shilingi milioni 120, mwingine akaweka shilingi milioni 130. Mimi wa shilingi milioni 100 nikachukuliwa wakati kiuhalisia bado tume-*inflate* bei, imekuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *MSD* wakalalamika sana kwamba wamefanya tafiti na wamegundua kabisa, unapokuwa unachukua ile *tender*, pamoja na kwamba inaonekana ni *the lowest bidder*, lakini kwenye uhalisia kwenye *market* unakuta wame-*inflate price*. Unaweza ukanunua kwa shilingi milioni 120 wakati kwenye *market* unakuta kitu kinauzwa shilingi milioni 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri pia tuangalie hili, tubadilishe Sheria ya Manunuzi ya Umma walauo iweze ku-*accommodate* kipengele kiongezeke pale kwamba, sawa ni *the lowest bidder*, lakini tuangalie na uhalisia wa bei kwenye soko inakuwa ni kiasi gani? Vinginevyo tutakuwa tunapeleka gharama kwa walaji ambao ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna huu mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao (*Tanzania Electronic Procurement System*). Huu mfumo una upungufu ambapo unasababisha gharama kwa *MSD*. Huu mfumo unatambua lugha mbili tu; Kiswahili na Kiingereza. Sasa ukiangalia watengenezaji wakubwa wa vifaa hivi, kwa mfano, *MRI, CT-Scan, sijui X-Ray*, na kadhalia, kwa mfano, ni Spain, Russia, German *and the alike*. Wachina ambao hii lugha ya Kiingereza siyo lugha yao ya mwanzo ukiingia kwenye mifumo yao ya *system*; kwa hiyo, inasababisha mwanya kwa huyu *MSD* asiweze kununua *straight from the manufacturer*, inabidi anunue *from the supplier* ambaye ana-act kama *an agent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu *supplier* anaweza akanunua kwa sababu yeye mfumo unakubaliana; anajua Kiingereza na Kiswahili; ananunua kwa *producer* au *manufacturer* kitu ambacho tungeweza kukinunua sisi *straight*; let say kwa shilingi bilioni mbili, yeye anakuja anatuuzia kwa shilingi bilioni 2.5 au shilingi bilioni 2.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie huu mfumo wetu tuurekebishe uweze ku-*accommodate* lugha zote ambazo tunajua kwamba tunanunua vifaa hivi vya hospitalini kuweza kupunguza gharama kinyume cha hapo tunatoa mwanya mkubwa na gharama kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tulipotembelea pale tuliona kabisa kwamba kuna vifaa ambavyo vinatozwa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya maendeleo ya reli. Mathalani vifaa vya vifungashio vya madawa panadol, PVC unakuta vinatozwa kodi unakuta pia vinatozwa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vipuli ambavyo ni vipuli vya muhimu sana au kwenye mashine ya vitendanishi ambavyo vinasaidia mathalani kwenye kutoa huduma ya uchujaji wa damu *dialysis*. Hivi ukitoza hivyo unapelekea bei inakuwa kubwa sana na watanzania wengi hawawezi waka-*afford* bei hizi za huduma ya uchujaji wa damu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri na ukitegemea Tanzania ili tuweze kuvutia wawekezaji nchi yetu ya Tanzania mojawapo ni kutoa hizi *tax incentive*. Kwa sababu vivutio vingine *like* umeme, ni shida bado kwetu hapa hatuna umeme ambao ni *reliable* muda wote ili wawekezaji waweze kuja achilia mbali hili taasisi ambayo ni ya Serikali. Maji pia ni shida miundombinu ya barabara na vingine vyote ni shida, sasa pale ambapo tunaona kuna umuhimu kwa maslahi ya Taifa kama hivi nilivyoeleza hapa hatuwezi kutoa *exemption* yaani tuondoe hii kodi ya ongezeko la thamani nah ii kodi ya maendeleo ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani kwa hawa wa Keko hawa *MSD* ambao wanasema ukiviweka hivyo inakuwa ni gharama sana sasa kwa kuanzia tuondoe hiyo tuone sasa tukishaondoa hii ambayo inaenda kupunguza gharama uzalishaji utaongezeka vipi kwa viwanda ambavyo ni vya Serikali. Tukishaona baada ya muda sasa tuweze kukaribisha na sekta binafsi kupitia PPP ili waweze kuingia na wenyewe kwa kufanya hivyo ina maana tutakuwa na viwanda vingi ambavyo vinazalisha madawa haya na tutaenda kupunguza ukosefu wa madawa kwenye vituo vya afya, kwenye hospitali na kuweza kuokoa maisha ya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kwa haraka haraka Mheshimiwa Naibu Spika na wewe ulikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje *by then* Ulinzi na Usalama, na tulikuwa na kikao Kamati ya Uongozi moja ya *issue* ambayo ilijitokeza zaidi ilikuwa ni fidia ambazo wanatakiwa walipwe watanzania wanaopisha maeneo kwa ajili ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na katika Kamati ya Uongozi siku zile tuliazimia na Serikali ikasema kabisa inaenda kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi yale maeneo yaliyoainishwa ya Viruti, sijui Kikombo, Nyabange na maeneo mengine ambayo pia yaliahidiwa kwamba yangeweza kutekelezwa *by then* mpaka kufikia muda huu ikiwepo Tarime ambayo kila siku nasimama naongea hapa tunaomba Serikali muweze kufanya fidia ili hawa wananchi

watanzania hawa waweze kuondoka kwenye hayo maeneo waende kwingine wakafanye shughuli za maendeleo wamekuwa wamekaa kama watumwa kwa muda mrefu sana mnafanya tathmini muda unapita muda unapita unarudi tena kufanya tathmini. Si sawa kabisa tunaomba kabisa kama vile ambavyo kamati imeainisha na kikao kilikaa Serikali iweze kupeleka fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni hili pendekezo la kuhakikisha kwamba tunaongeza fedha kwa ajili ya *TARURA* na hii imekuwa ni vilio sana hatuna muunganiko kwenye maeneo yetu huko si vijijini si mjini hata hapa Dodoma ukipita kwenye barabara hizi ambazo ziko *under TARURA* ni *disaster*. Sasa Serikali iweze kulichukua hii ihakikishe imeongeza hizo walau bilioni 111.3 kwa Kunzia kwa kuweka *installment* mwezi huu na mwezi ule ili uhakikishe kwamba tunaweza kurekebisha hizi barabara.

Lakini in *future* kama ambavyo Waziri wa TAMISEMI hapa juzi aliongea tuhakikishe kwamba haitokezi hii kitu muweze *for cast* muone kabisa kwamba huwa mvua ikitokea barabara zinaharibika kwa hiyo mtengeneze kwa kiwango ambacho kinakubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa...

NAIBU SPIKA: Ya mwisho hiyo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mbona ya kwanza haijapigwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Awile mundu imekwisha hiyo Mheshimiwa Kwagilwa jiandae Mheshimiwa George Malima jiandae Mheshimiwa Mabula.

MHE. KWAGILWA R. NHAMILO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana niungane na wenzangu kukupongeza

kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kamati yako ya bajeti pamoja na Bunge kwa ujumla tulifanya *Amendment of the Road and Fuel Tolls Act Cap. 220*. Marekebisho haya yalilenga kuipatia *TARURA* fedha kwa ajili ya barabara zetu za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe taswira ndogo sana ya *TARURA* tunapozungumza *TARURA* ili angalau tufanye mapinduzi kwenye eneo hili la barabara zetu za vijijini. Handeni hususan Jimbo la Handeni mjini barabara zetu za *TARURA* barabara za vumbi ni 88%. Kwa Mkoa wa Tanga barabara zetu za *TARURA*, barabara za vumbi ni 79% na kwa Tanzania nzima *TARURA* ina mtandao wa barabara unaofika kilometa 144,429 zinahudumiwa na *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizo 76% ni barabara za vumbi kwa maana ya kilometa 111,197, *TANROADS* inahudumia barabara zote kilometa 36,000 na katika hizo zenye lami ni kilometa 11,000 *what is the myth* ni kitu gani cha ajabu kwenye hiki ninachotaribu kukizungumza tumeipa *TARURA* jukumu kubwa sana lakini hatujaweka juhudi kubwa za kibajeti na za kitaasisi za kiteknolojia na kwa nguvu zote kujaribu kuibadilisha ili iweze kuhudumia barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi nilizotoa hapa ndiyo kusema kwamba barabara nyingi mtandao mkubwa wa barabara Tanzania uko chini ya *TARURA*. Sasa *the opposite* ndiyo tunachokifanya tunapeleka nguvu kubwa sana *TANROADS* na natambua kwamba barabara wanazohudumia ni za lami, lakini haiondoi *fact* kwamba kilometa hizi 144,429 ndiko ambako Tanzania waliko na ndiko ambako uchumi uliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni nini ninachotaka kusema ni kwamba lazima tufanye mapinduzi ya namna ya *approach* ya kutengeneza barabara zetu kuanzia kwenye bajeti yetu inayokuja lazima tufikirie kwa

namna ya tofauti. Tathmini ya dharura iliyofanywa juzi kwa uharibifu unaofanywa na mvua uliosababishwa na mvua tathmini iliyofanywa ya haraka inahitajika bilioni 120 kufanya tu marekebisho .(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia sasa ile *amendment* tuliyo fanya ya kutoka bilioni 322 na hizo kwa hakika hatutaweza kuzikusanya zote, 120 yote inaenda kufanya marekebisho yaliyosababishwa na mvua. *Which means* tunakwenda ku-*miss target* yetu ambayo tulijiwekea kufungua barabara zetu za vijijini ninachotaka kusisitiza kama ambavyo tumefanya jitihada za makusudi kwenye SGR, jitihada za makusudi kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere, vivyo hivyo moyo wa uchumi wa nchi yetu ni hizi barabara hizi kilometa 144,000 ambazo ziko chini ya *TARURA*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima tufanye mapinduzi ya namna ya kufikiri na lazima tufanye mapinduzi ya namna ya kutenga bajeti yetu. Tusii-*treat TARURA* kama kachombo kadhaifu dhaifu hivi ambako kako chini ya Wizara ya TAMISEMI ambako hata hivyo hata kwenye hiyo Wizara yenyewe tuna Waziri wa TAMISEMI na Manaibu Waziri wawili mmoja anajulikana ni wa afya na mwingine anajulikana ni wa elimu. Yaani hata hiyo *TARURA* pale huioni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ni lazima tufanye mapinduzi bajeti inayokuja tutenge fedha nyingi lakini zienda angalau zikabadilishe barabara zetu zitoke kuwa za vumbi ziende kwenda kuwa changarawe. Lakini na siku za usoni siku za baadae tujifunze teknolojia kwa wenzetu tutengeneze barabara zetu kwa teknolojia ambayo ni *cheap*.

NAIBU SPIKA: Malizia malizia

MHE. KWAGILWA R. NHAMILO: Kama ambavyo alishauri Mheshimiwa Rais barabara zetu tuzifanyie mapinduzi tuende kwenye teknolojia ya kati ambayo siyo gharama sana lakini barabara tuzijenge ziweze ku-*survive* na ku-*sustain* kwa muda mrefu.

NAIBU SPIKA: Vingine unaweza ukaandika yatapokelewa

MHE. KWAGILWA R. NHAMILO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Malima jandae Mheshimiwa Stanslaus Mabula, jandae Mheshimiwa Mpina.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa ajili ya kunipa nafasi ya kuchangia hoja zote mbili. Mashirika mengi ya umma hayafanyi vizuri yote ambayo tumeyapitia hayafanyi vizuri kabisa na hasa katika maeneo yafuatayo. Kwanza mashirika mengi ya umma yanadaiwa yana mzigo mkubwa sana wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mashirika haya hayana uwezo wa kukusanya madeni yao, unakuta shirika linadaiwa lakini pia linawadai watu pesa nyingi sana na mimi nitatoa mfano hapa mmoja Shirika la SIDO. SIDO lina mzigo mkubwa sana wa madeni mwaka 2018/2019 ilikuwa inadaiwa bilioni 4.7 lakini 2019/2020 deni lake limefikia bilioni 8 ongezeko la 77% unaangalia unaona kwamba sasa hili deni wanadai bilioni 5 wao wangekusanya hizo bilioni 5 wangeweza ku-*offset* hili deni angalau lingekuwa limebaki kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawana uwezo wa kukusanya madeni yao lakini vilevile hawana uwezo wa kulipa madeni yao, na Shirika hili tunalitarajia sana lingeweza kuwa mkombozi wa uchumi wa nchi hii kwa sababu kazi yake kubwa ni ku-*support* viwanda vidogo vidogo. Lakini kama linaendeshwa katika mtindo huu, haliwezi kuleta tija yoyoe inayokusudiwa. Serikali lazima iangalie sana kwa ukaribu uendeshaji wa shirika hili kupitia ofisi ya msajili. Bila hivyo hii SIDO haitokuwa na maana yoyote Serikali itaendelea kutoa ruzuku na itaendeshwa na itapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka 2018/2019 Shirika lilitengeneza faida ya bilioni 1.56 lakini 2019/2020

limetengeneza hasara ya bilioni 2 sasa unaweza kuona uendeshaji wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri sana Mashirika haya yajitahidi sana kwanza yawe na utamaduni wa kulipa madeni yao mara wanapopata huduma au wanapofanya biashara walipe madeni hata kama kwa kidogo kidogo. Pia wawe na mikakati mahsusi ya kukusanya madeni kwa wale wanaowadai hiyo itawasaidia kuendesha mashirika yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia matumizi sheria imewekwa ya fedha Na. 16 ya mwaka 2015 ambayo inaweka ukomo wa kutumia mwisho 60% kuna kitu gani mashirika mengi yamepita 60% kuna tatizo gani katika Serikali kuhakikisha kwamba inasimamia hii sheria kila shirika likaenda kama sheria inavyotaka. Kwa sababu kila shirika unaloliona utakuta limevuka hiyo sheria limevuka huo ukomo wa 60% kwa nini Serikali haisimamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nashauri sana Serikali kupitia Msajili wa Hazina mashirika haya yabanwe yaweze kutekeleza sheria hii ya fedha Na. 16 hii itasaidia hata matumizi yale yasiyo ya lazima yataweza kuepukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna shida ya miradi mingi kutokukamilika kwa wakati lakini ukiangalia sababu kubwa ziko moja kwanza ni michakato mingi kila wakati shirika liko kwenye mchakato mipango iko kwenye mchakato litaanza yako mashirika tumeyakuta wana miradi imepita hata miaka 10 haijakamilika. Mfano hata mradi wa Liganga na Mchuchuma kila wakati mnaambiwa michakato inaendelea, lakini pia Serikali haitoi maamuzi kwa wakati au haitoi maamuzi mapema kwamba mradi huu uanze wakati fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nayo ni shida nyingine kwamba maamuzi hayafanyiki halafu fedha zinaendelea kutumika mradi haujaanza na hizi fedha za wananchi walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hata ile iliyoanza kidogo Serikali haipeleki fedha ili miradi ile iendeleo kutekelezwa kwa wakati. Kwa hiyo, tuna tatizo hilo kwamba mashirika yetu tusipokuwa waangalifu hayawezi kutuletea tija tunayoikusudia. Tunategemea kila shirika liwe na uwezo wa kutoa mchango katika mfuko mkuu wa Serikali. Lakini sasa hivi mengi hayana huo uwezo ama yanachangia kidogo sana ama mengine hayachangii kabisa lakini kwa sababu hatujawa *serious* katika maeneo haya. Mashirika haya lazima tuyasimamie vizuri tukitaka tukuze uchumi wa nchi hii tukitaka tupate tija, tukitaka Serikali ipate gawio ni lazima tuwe na utaratibu wa kuyasimamia kwa karibu. Serikali, *TR* lazima isimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mabula jiandae Mheshimiwa Mpina, jiandae Mheshimiwa Dkt. Danielson Pallangyo.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa hizi dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na nikupongeze wewe lakini nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Ofisi ya Msajili ya Hazina ambao sisi kama wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma tunafanya nao kazi kwa ukaribu sana na hata uzuri ripoti yako unayoiona na uliyoisikia leo ni kwa sababu ya wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie pale ambapo ameishia Mheshimiwa Malima jambo kubwa sana ambalo Serikali inabidi ilifanyie kazi kwa umakini mkubwa ni namna ya kuangalia mashirika haya ambayo tumeyapa nafasi ya kufanya kazi na usimamizi wake kwa namna moja au nyingine tunakuwa na miradi isiyokamilika kwa wakati na kwa mfano mzuri sana ni miradi ambayo iko kwenye shirika la nyumba la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna miradi imeanza muda mrefu lakini iko miradi ambayo imesha-*takeoff* sasa inakwenda vizuri. Lakini ni kwa nini miradi ambayo bado haijaanza kuchukuliwa hatua mpaka leo takriban miaka 10 haitakiwi kuanzishwa na kuendelezwa mpaka sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi ya mfano pale Kawe wanaoishi Dar es Salaam watakuwa wanajua 711 Kawe na ile *Golden Premier Licence* Kawe. Hapa kuna mbia lakini huyu mbia kila siku anaingilia hapa anatokea hapa niombe sana Serikali iingilie kati fedha zilizowekwa pale ni fedha za walipa kodi na kama tutaacha hivi tutakuwa tumetupa fedha na hatutakuwa hatuwasaidii watu wa *National Housing*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini fedha zinazokuja wakati wa gawio ni moja ya chanzo kizuri sana cha mapato kama taasisi hizi zitafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kuhusu kiwanda cha viudadu kama tulivyoambiwa hapa na wenzangu waliopita kiwanda hiki ni mali ya Serikali kupitia *NDC* kwa asilimia 100. Serikali yetu inapata fedha nyingi sana kwenye mfuko kutoka mataifa na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kushughulikia malaria asilimia 98 fedha hizi zinashughulikia ugonjwa wa malaria na sisi tumepata bahati ya kuwa na kiwanda hapa ndani bahati mbaya sana asilimia hizi 98 ya fedha kutoka *Global Fund* hatuwezi kuzitumia kununua dawa kwenye kiwanda chetu cha viudadu kwa sababu dawa hizi zinazozalishwa hazijaidhinishwa na ithibati ya *WHO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuna dhamira ya dhati ya kupambana na ugonjwa wa malaria ni lazima tufike sehemu tukubali *NDC*, Serikali pamoja na hao ambao ni *radio farm* kutoka Cuba ambao ndiyo wenye hati miliki ya hivi viudadu wakikaa pamoja shida ya hawa ni shilingi 6% itakayowafanya wao wawasaidie kwenye kiwanda hiki kupeleka *WBHO* waidhinishhe ili dawa hizi zitakazokuwa zinatumiwa zikubalike kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo pale Uganda wameanzisha ujenzi wa kiwanda cha viaadudu kama hiki tulichonacho sisi hapa *NDC*. Hebu niambie kikamilika dawa hizi tutauza wapi? Tutabaki kuhangaika na halmashauri zetu ambazo tumeshatoa maelekezo lukuki lakini hayazingatiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana na niombe sana Serikali hivi viwanda tunavyovianzisha kwa nia njema kama hatutakuwa na mpango mahususi wa kuwekeza nguvu na usimamizi mzuri nimesema hapa *TR* anafanya kazi nzuri sana lakini wakati mwingine kwa namna moja au nyingine anaweza akazidiwa asifikie malengo yake. Kwa sababu kama walivyosema aki pia huku watu wanatokea huku ni kitu gani kinachoshindikana kiwanda hiki ithibati hii iende *WHO* ithibitishwe na dawa hizi katika asilimia 98 ya dawa tunazopata kutoka kwenye *Global Fund* zikija hapa tutakuwa tumevuka lengo la tumeokoa watanzania wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mpina, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi ambayo umenipa ili niweze kuchangia hizi hotuba mbili, Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* pamoja na Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Kwa ujumla wenyeviti wote hawa wawili wametoa hotuba nzuri sana hapa Bungeni, na kwa kweli tunawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nizungumzie Mashirika ya Umma ambayo Mwenyekiti pamoja na Kamati nzima ni vizuri kwenda kuisimamia Serikali kule ili kuhakikisha kwamba *TR* anajengewa uwezo mkubwa wa kifedha na rasilimali watu ili aweze kuyasimamia mashirika haya kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kwamba hapa tunazungumzia mapato ya Serikali. Kwenye taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ukurasa wa 31 ameeleza *performance* ya ukusanyaji wetu wa mapato. Pale kwenye mapato yasiyo ya kodi tuna asilimia 36 tu, yaani hadi mwezi wa 12 tuna asilimia 36; kwa hiyo ni *likely* kwamba hatuwezi kufikia asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliomba tuletewe jedwali la wizara na taasisi zote zinazohusika na ukusanyaji ili tujue ni nani ambaye hakusanyi vizuri na sababu zake. Kwa bahati mbaya sana mpaka tunawasilisha hotuba hii hatukuweza kuletewa jedwali hilo. Lakini bado tunasisitiza kwamba jedwali la wakusanyaji wote wa kodi liletwe tulione na tuone ni nani ambaye anashindwa kukusanya mapato ya Serikali sawasawa, kwa sababu pale nyuma walikuwa wanasingizia Corona haipo, sasa kwa nini wameshindwa kukusanya mapato kama ilivyotakiwa kwenye Bajeti ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ninalotaka kulizungumzia, wengi wamezungia ajira za Watanzania hapa. Ni ukweli usiopingika kabisa kwamba tusipojipanga vizuri kuhakikisa kwamba tunalinda ajira za Watanzania, na Watanzania hawa milioni 60 wasiposhiriki kikamilifu katika uchumi wao hatuwezi kupata maendeleo, hata tungefanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hujuma nyingi zinazofanywa, nyingine zinafanywa hata na Serikali yenyewe. Kwa mfano kwenye manunuzi, inakuwaje mpaka leo hii Serikali inaenda kununua bidhaa na huduma nje ya nchi ilhali ina viwanda hapa nchini ambavyo vinazalisha bidhaa hiyo? Mfano sasa hivi Serikali imeanza kununua dawa za kuogesha mifugo katika bajeti ya mwaka 2021/2022, wameanza kununua dawa za kuogesha mifugo kwa wazabuni wanaoingiza kutoka nje ya nchi ili hali hapa nchini tuna kiwanda kinachozalisha dawa nyingi za kutosha kuhudumia mifugo ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, bado hadi leo hii Wizara ya Ujenzi inaajiri mkandarasi na mshauri mwelekezi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kujenga barabara ya kilometa 11 za lami; ili hali kuna Watanzania wenye uwezo wa kujenga mradi huo na wana weledi wa kutekeleza mradi huo. hivi ni kwa nini tufikie hapo? Haya yote yamefanyika na Bunge hili lipo na Serikali ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili ambalo tumelizungumza sana, nalo hili ni sababu kubwa ya kukosesha Watanzania ajira, katakata ya umeme. Katakata ya umeme imeelezwa kwenye Bunge lako, na jana ilizungumzwa na Bunge lako Kamati husika ilipowasilisha, na majibu ya Serikali yaliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kushauri hapa, kwa majibu ya aliyotolewa na Serikali na taarifa ya Kamati ya Nishati iliyowasilishwa, na majibu yaliyotolewa zamani na Serikali kwenye Bunge hili, ninaomba jambo hili tulifikishe mwisho. Tulishawahi kuyafikisha mwisho mambo mengi magumu. Tuliwahi ufikisha *Richmond, ESCROW*; na hili kwa majibu ya mkanganyiko yanayotolewa na Serikali kuhusu katakata ya umeme na kuwasababishia Watanzania kuingia kwenye dhiki kubwa, viwanda vnafungwa, uzalishaji unashuka na inaleta mfumuko mkubwa wa bei...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ningependa kumpa taarifa mzungumzaji kuhusiana na suala la katakata ya umeme. Nimpe taarifa tu kwamba Mheshimiwa ukiendelea kuliongelea suala hili na wewe utaambiwa kama nillivyojibiwa mimi, kwamba sikupenda Mama Samia awe Rais au yeye awe Waziri. Ni hiyo tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mpina hiyo si taarifa, endelea.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan asiingizwe katika mambo haya, Rais wetu asiingizwe katika udhaifu wa utendaji wa baadhi ya Mawaziri, wamuache Rais wetu afanye kazi nzuri ya Watanzania. Udhaifu wa Waziri autetee mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuyasema haya, kwanini nataka tume teule ya Bunge iundwe? Kuchunguza suala hili la katika katika ya umeme na kuchelewa kwa mradi wa Mwalimu Nyerere, ziko sababu!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 mapato ya *TANESCO* yalikuwa bilioni 72, tulisimamia yakapanda mpaka yakafikia bilioni 160 kwa mwezi, na sasa imewasilishwa mwaka 2021 mapato ya *TANESCO* yamefika trilioni 2.4. sababu za kushindwa kufanya ukarabati na matengenezo zinatoka wapi? Hawa hawa *TANESCO* walikuwa na madeni sugu yaliyofikia bilioni 272, yakasimamiwa yakapungua mpaka yakawa bilioni 49, sababu ya kushindwa kufanya matengenezo yanatoka wapi? *TANESCO* hawa wameweza kufanya kazi nzuri mpaka tukazima mitambo ya mafuta ya *IPTL*, *AGRECO* na *Symbion* ambayo yalikuwa yanagharimu bilioni 719 kwa mwaka; na sasa gharama hizo wameziokoa, sababu za kushindwa kufanya ukarabati wa mitambo inatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ilikuwa inafanyiwa ukarabati, tulikamilisha miradi mipya kutoka mwaka 2015 mpaka 2020, tumekamilisha miradi mipya iliyokuwa haijakamilishwa, tukaweza kupanua njia na kusafisha njia za usafirishaji wa umeme na mpaka tukasababisha vijiji ambavyo vilikuwa na umeme kutoka 2018 mpaka 10,312. Upanuzi huo wote umefanyika. Leo hii *TANESCO* sababu za katakata ya umeme zinatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Bunge lako liambiwe ukweli, na kama miaka mitano, kama inavyozungumzwa, ni kama miaka sita kama inavyozungumzwa, kwamba ukarabati ulikuwa haufanyiki, kwa nini sasa umeme ulikuwa haukatiki? Kwa nini umeme ukatike leo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Watanzania waambiwe ukweli, majibu ya bla bla katika jambo hili hatuwezi kukubali katika Bunge hili. Ukikosa umeme kwenye Taifa; Mheshimiwa Rais wetu leo hii anahangaika sana kutafuta wawekezaji ndani na nje ya nchi, utamleta mwekezaji wa nani anayeambiwa kwamba Taifa halitakuwa na umeme mpaka uwe na trilion mbili. Ina maana kwamba tusipopata umeme hauwezi kuwaka?...

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. LUHAGA J. MPINA: ... na utaendelea kukatakata...

NAIBU SPIKA: Ahsante!

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili lisikubali, na tume teule ya Bunge iundwe, ichunguze jambo hili pamoja na lile...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, Mheshimiwa Alli Hassan King pamoja na Mheshimiwa Eric Shigongo wajiandae.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi nimesimama kuunga mkono hoja zote mbili, ukizingatia pia kwamba mimi

ni mjumbe wa Kamati ya *PIC*, lakini pia nimekuwa wa ili kutoka mwisho kuchangia, kwa hiyo, mengi yameshazunguzwa na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana wenyeviti wote wawili kwa hotuba zao nzuri ambazo zimejaa na zimesheheni kila tulichokuwa tunakihitaji. Lakini pia nikupongeze wewe na Mheshimiwa Spika kwa kuaminiwa na chama chetu na majina yenu yakarudi hapa nasi tukafanya kweli, na sasa hivi ninyi ndio viongozi wa kuu wa huu mhimili muhimu wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee sana nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana mama yetu na kumpongeza kwa kazi nzuri ambazo Mheshimiwa Rais anawafanyia Watanzania, kwa uongozi mahiri. Kwa kweli amefanya makubwa. Mwaka jana ametengeneza historia kwa Watanzania, madara 15,000 kwenye sekta ya elimu si jambo dogo; lakini pia kule Arumeru Mashariki nasi tulipata madara 70 ambayo kwakweli ametua mzigo mkubwa sana kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si sekta ya elimu tu, hata sekta nyingine alifanya kazi nzuri mno, zile fedha za UVICO 19 alizotuletea na kuzisambaza kwa uwazi mkubwa zimeweka historia kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hizo salamu za pongezi naomba sasa nirudi kwenye hoja, na nitazungumzia mambo mawili kwa ufupi sana. Nazungumzia changamoto za bodi za wakurugenzi za mashirika na taasisi zetu za umma. Lakini pia nitazungumzia upungufu wa mitaji kwa taasisi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekutana na mashirika kadhaa ambayo yalikuwa na matatizo ya bodi, kwamba bodi haipo na kama ipo *composition* yake ina matatizo. Kwa mfano *EPZA* na *TIC*, na *TIC* haikuwa na bodi, lakini pia watendaji wakuu na waliokuwa wameshika nafasi zile nyeti walikuwa wanakaimu. Sasa hii kukaimu na kutokuwa na bodi kunafifisha utendaji kazi wa hizi taasisi zetu. Tunaomba Serikali

iangalie kwa jicho tofauti kidogo maeneo haya na kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinakuwa na utawala ambao ni timilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa mitaji, tulishuhudia kwamba kuna taasisi na mashirika kadhaa ambayo hayana mitaji ya kutosha. Kwa mfano *TTCL, TPDC, TADB* pamoja na *EPZA*. Mashirika haya yameanzishwa na Serikali na yalitegemea kuwa *funded fully* kwa sababu umiliki ni wa Serikali kamili. Mashirika haya, kwa mfano *EPZA* kwa miaka mitatu Serikali haijatoa fedha. Matunda yake ni kwamba *EPZA* imekuwa inafanya kazi zake kwa kusuasua. Zone pekee ambayo inaonekana inafanya kazi vizuri ni ya Benjamin William Mkapa iliyoko kule Mabibo, huku kwingine kote wanasuasua na sehemu nyingine kwa sababu wana nguvu ya kisheria ya kuchukua ardhi ya wananchi na kuwafidia, wameshindwa kuchukua lakini wakasababisha taharuki, kwamba wanachukua lakini hatimaye hawapi fedha lakini wameshatia doa kwenye maisha ya wananchi kwamba wanayang'anywa maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itazame vizuri na kuhakikisha kwamba taasisi hizi wakati zinaanzishwa ziwe *funded fully*, pamoja na *TADB* lakini tunashukuru na tunaipongeza Serikali kwamba iliweza kutoa shilingi bilioni 208 mwezi Disemba.

NAIBU SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele imelia, basi niseme tu kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ally Hassan King, Eric Shigongo na Mheshimiwa Tarimba wajianda.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nikupongeze kwa kupata uteuzi huo wa Naibu Spika, nakupongeza sana. Pia tunakupongeza kwa

kuwa mgeni juzi siku ya Jumapili pale, na tukaona kwamba ile kutoa mkono wako kama Mgeni rasmi ilisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika hoja moja, nayo ni bandari, Kamati ya Bajeti wameizungumzia Bandari, lakini pia Kamati ya Mitaji ya Umma nao wameisemea. Kwa hiyo, nijikite moja kwa moja katika upakuaji wa mafuta bandarini. Tunafahamu mafuta yanapakuliwa pale bandarini na anayeshughulikia hili pale ni *TPDC*. Lakini pia kuna *PURA* naye huwa anasaidia. Sasa, tunapakua mafuta kwa ajili ya nchi tofauti. Yako yanayokwenda Rwanda, Burundi, Malawi pamoja na Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa bahati mbaya kuna tozo. *TPDC* na *PURA* wanaitoza *ZPDC* na *ZURA* tozo ambayo hizi nchi nyingine hawatozwi. Sasa hii tozo imegeuka wakati mwingine inaweza kuwa deni; Sasa nielezee nini athari yake? Athari za tozo hizi ni mbili. Moja, *ZPDC* na *ZURA* yaani wanakaa kama watalipa hiki kitu, inamaana kwamba kule Zanzibar bei ya mafuta itakuwa imebaki ileile, lakini *TPDC* yeye ataandika kama ni deni, lakini litakuwa ni deni hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na athari nyingine, *ZPDC* na *ZURA* walikilipa tozo hii moja kwa moja itakuwa kwamba *TPDC* na *PURA* wamepata pesa lakini kule Zanzibar bei ya mafuta itaongezeka. Sasa haya yote mawili yanaweza yakatokea. Ninalizungumzia hili katika muktadha kwamba Serikali ilianganalie na walete sheria iliyompa mamlaka hayo *TPDC* kwamba yeye awe anawatoza kodi watu wote. Kwa hiyo kitu hicho angalau kidogo kitakuwa kimekaa vizuri; kwa hiyo walete sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tukibadilisha sheria hiyo ina maana kwamba *ZPDC* na *ZURA* hawatatozwa tozo na *TPDC* kwa sababu hawatozi tozo Rwanda, Burundi wala Malawi, na haya mafuta yanapita hapa kama ni *transit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemu unasema kwamba ajizi ni nyumba ya njaa, na chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako. Tumelizungumzia hili, Tanzania sasa

hivi miundombinu ya upakuaji mizigo ni mizuri, lakini kasoro moja iliyopo ni kwamba hatuna mfumo mmoja kwa taasisi zote zinazoshughulika na pale bandarini. Pale pana *TPA*, *TRA*, wako na *regulators* stofauti ambao wanafika mpaka 12. Hawa *regulators* mpaka wakimaliza *documentation* ule mzigo kutoka pale unachelewa, na sisi uchumi wetu tunapitia Bandari ya Dar es Salaam. Tukisema kwamba tunachelewa kutoa mzigo ina maana tunaipunguzia ushindani bandari yetu. Kwa sababu tumezungukwa na bandari nyingine za nchi Jirani, kwa hiyo ili bandari yetu iwe *competitive* ina maana kwamba tuwe na mfumo mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeleza kwenye Kamati ya Bajeti kwamba tulikwenda kutembelea bandari ambako walisema kwamba wanatengeneza mfumo wa pamoja. Hata hivyo ni mwaka sasa mfumo huu wa pamoja haujafanya, ndipo nikasema kwamba ajizi ni nyumba ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kine, kuna kitu kinaitwa *TICTS* ambao wameingia mkataba na Serikali juu ya kutoa mizigo pale bandarini. Hata hivyo wakati mwingine kila ukiitazama hii *TICS* tunaona kama vile kuna vituu kidogo havielekei. Tunaiomba Serikali, *TICS* wana mkataba ambao wana *automatic renew*. Kwamba watakapokuwa wameteteleza kigezo fulani mkataba ule unajirudia tena. Lakini bandari sasa hivi inaelekea kujitegemea na inafanya mapinduzi makubwa. Kuwa na *TICS* pale, na hivi vigezo tunavyompa, akifika kwenye asilimia ile ina maana kwamba bandari haveze kumingilia *TICS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali huu mkataba utenguliwe, kwa sababu mkataba huu ni kama umewalenga watu kuwa na maisha yao yote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwenye mambo matatu. Bajeti, kwa utekelezaji wake kwenye makudanyo, kwenye sheria ya fedha kulisikiliza Buunge, lakini pia katika kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja zote mbili.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Shigongo, jilandae Mheshimiwa Tarimba.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa sababu ya ufinyu wa muda nianze kwa kukupongeza wewe kwa kupata nafasi ya kuwa Naibu Spika wetu, lakini nichukue nafasi hii poa kumpongeza sana Jirani yangu, dada yangu, Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa nafasi hii ambayo ameteuliwa kuliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza pia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa inayoendelea hapa nchini; kwenye miundombinu, afya, kwa kweli mimi binafsi ninaridhika kabisa kwamba kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 8(1) (a) inasema; Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi. Hapa inamaana kazi kubwa ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaustawi katika afya, katika uchumi, katika miundombinu, katika elimu na mambo mengine yote. Ni kazi ya Serikali nadhani nizungumzie suala moja juu ya uwezeshaji wa wazawa kiuchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili kwa sababu sisi tulioko hapa ndani tumebahatika kuwa Wabunge, tumebahatika kuwa na Maisha tulioyonayo lakini wako watu wenzetu wengi sana huko nje bado wanaishi Maisha duni na kwenye umasikini mkubwa. Bajeti ya Taifa letu kwa mwaka ni tirioni 34.88 najiuliza swali kila siku, tirioni 34.88 ngapi zimerudi kwa wananchi na ngapi zinaenda nje ya nchi yetu. Nimesimama hapa kuzungumza kwa niaba ya watanзания wazawa na ninaposema wazawa simaanishi rangi namaanisha watu wenye asili ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watanzania wanatakiwa wanastahili kunufaika kabisa na fedha hizi tirioni 34.8 inakuwaje fedha hizi sehemu kubwa zinaenda nje ya nchi badala ya kuwasaidia wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa sababu Bunge lako tukufu mwaka 1994 lilitunga Sheria ya uwezesaji wazawa kiuchumi na ilisainiwa na Marehemu Rais Benjamini William Mkapu tarehe 19 Januari, 2005 ya kwamba nchi hii itawawezesha wazawa weweze kushikilia vyanzo vya uchumi vya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo ninaposimama hapa bajeti ya miundombinu ya Taifa hili ni tirion 3 nataka nijjulize tirioni 3 hizi za kutengeneza barabara ya miundombinu gapi zinabaki kwa watanzania bajeti hii ya miundombinu peke yake ni trioni 3 ni gapi zinabaki kwetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wanaendelea masikini mabilionea ni wale wale toka miaka ile na wajibu wa Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Napenda kuona wazawa wengi wanafanikiwa kiuchumi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani na sitaki kutaja nchi yoyote kama alivyozungumza Rafiki yangu Mpina haiwezekani tirioni 3 za barabara fedha inayoenda kwa wazawa ni asilimia 20 peke yake nyingi zinaenda kwa wageni wanaokuja hapa na magegi peke yake baada ya miaka mitano wamekuwa mabilionea na wanatuona sisi wazawa hatuna akili haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kukuomba wewe na kuomba Bunge hili tukufu kwa sheria hii ya Mwaka 1994 ya kuwawezesha wazawa kiuchumi, wazawa wapewe kipaumbele ni nchi gani duniani ambayo hakuna mning'ono wa Taifa ni lazima Taifa hili linong'one na kusema ya kwamba biashara ya kiwango hiki itaenda kwa wazawa, barabara ya kilomita hizi zitaenda kwa wazawa, haiwezekani tukawaachia wageni kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema hayo siyo kwamba nachukia wageni nchi yangu inahitaji sana mitaji kutoka nje, lakini pamoja na kuhitaji mitaji kutoka nje bado tuwe na uwezo wa *kuwa-protect* watu wetu na kuwapa watu wetu kipaumbele ya kwamba tumezungumza hapa ndani nataka haya mambo yaende nje ya kwamba *tender* za aina fulani zitaenda kwa watu wetu hata kama hatuzungumzi, hata kama hatuandiki kwenye magazeti, hatakama hatusemi huko nje tunajua nitakapo tenda mimi na akatenda na huyu kutoka nje nitapewa mimi kwa sababu fedha hizo zitazunguka hapa hapa nchini kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lizingatiwe kwa sababu wataanzania wamechoka kuona wageni wanaendelea kutajirika wao wanaendelea kuwa maskini. Ni lazima wao wapewe nafasi ya kutajirika kwenye nchi yao nah ii nchi ni ya kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaandika kwa maandishi mambo yote ninayoyazungumza ahsante kwa kunipa nafasi nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Tarimba, Jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri wa Biashara.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kuhusu taarifa za kamati ambazo zimewasilishwa leo. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja hizi lakini nianze vile vile kwa kumtaja Mwenyezi Mungu na niruhusu niseme Bismillah Rahman Rahim. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia maji kama ilivyokwenye ukurasa 27 nikipata muda nitazungumzia page 12 taarifa ya Kamati ya Bajeti. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya bajeti na kwa hali hii nazungumza mambo ambayo nayafahamu vizuri zaidi. Juzi tulikuwa na mazungumzo na Mheshimiwa Waziri wa Maji na katika Mazungumzo yale tulizungumzia masuala ya *RUWASA*, tukaona ugumu wa

matatizo ya maji ambayo yako vijiji, tutakaa miaka mingi sana bila ya matatizo ya maji kuweza kupatiwa ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Tanzania hii na Bunge hili hakuna siku ambayo inapita bila Mbunge yoyote kusimama kuzungumzia habari ya maji maswali ya maji yamekuwa ni mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali na kwenye hili tuige mfano mzuri wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan alipokwenda kutuletea fedha za mkopo ambazo zimeondoa matatizo ya shule za Sekondari katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwambia Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba hebu nendeni kwenye kila Wilaya angalieni mahitaji ya maji, angalieni vyanzo vya maji viko wapi tengenezeni mpango ambao utaiangalia Tanzania nzima ni wapi kwenye matatizo ya maji ni wapi maji yanapatikana hata kama ni kumshauri Mheshimiwa Rais akope fedha tumalize masuala ya maji, Bunge hili linaweza likaweka alama kubwa sana Bunge la Kumi na Mbili kwamba angalau asilimia 80, 90 ya matatizo ya maji yanaweza kwenda kumalizwa, tukope, kuna hasara gani ya kwenda kukopa kwa ajili ya mtanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba iingie katika Kumbukumbu na Mheshimiwa Waziri wa Maji sijui kama yuko hapa, lakini hachukue hilo kwamba Bunge hili kwamba limechoka kusikiliza maswali ya maji kila siku wakati tunaweza kupunga tukayaondoa matatizo ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine kuna kitu ambacho nashangaa sana mwaka 2015 na hili linahusiana na *page* 12 ambayo inahusiana na hushirikishwaji hafifu wa sekta binafsi. Serikali haifanyi biashara, Serikali kazi yake kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara ili iweze *ika-collect Government Revenue* fedha kutokana na kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015/2016 walitengeneza kitu kinaitwa *Blue Print* na wakakitoa mwaka 2018 mwezi mei na ikaeleza vizuri sana ni jinsi gani inavyokwenda kuboresha maslahi ya ufanyaji biashara kwa madhumuni ya kupata fedha ya kutosha katika *Government Revenue*. Na wakati ule *easy way of doing business*, watanzania sisi tulikuwa ni nchi ya 131 mwaka 2015 wakati ikitolewa hii ripoti tulikuwa sisi ya watu 141 katika nchi 190. Maana yake ni nini? Tulikuwa bora kabla ya *Blue Print* haijatengeneza *Blue Print* imetengenezwa ndiyo tumeanguka na tatizo lake kamati inasema mpaka leo hii wingi ya mamlaka za udhibiti zinaendelea kuongezewa kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia tozo zimejaa, ukiangalia ada kwenye biashara moja zimejaa, ukiangalia huku matatizo ya kodi siyo rafiki, mimi najjuliza ni kwanini basi tulitumia fedha kutengeneza *Blue Print* halafu ni sawa saw ana mtu uchonge kinyago halafu kile kinyango ukikiangalia unakiogopa eeh, tunatengeneza *Blue Print* tumeweka kwenye kabati hatuitumii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ituletee taarifa kamili ya jinsi ilivyotekeleza *Blue Print* katika kipindi chote hicho ili tuweze kufanya tathimini na kujuliza ni kwanini hatutoki katika idadi ile ya 142.

NAIBU SPIKA: Ahsante!

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru *message send*. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, sasa namuita Naibu Waziri Mheshimiwa Kigahe, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika taarifa hizi za kamati hizi mbili ambazo zimeletwa mbele ya Bunge lako. Kuna mengi yameongelewa

ambayo ni ya kujenga kwa hiyo niendeleo kushukuru kwa michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge lakini mahususi kwa kamati hizi mbili ambazo zinaendelea kuhisimamia na kuielekeza Serikali katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, yameongelewa mengi lakini kubwa ni kuona namna gani kuboresha au kuziwezesha taasisi ambazo zinatoa huduma katika maeneo tofauti tofauti ikiwemo taasisi yetu ya *ABZA CAMATEC, SIDO, TEMDO, TIC* na taasisi zingine ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. Tunachukua mawazo haya ya Waheshimiwa Wabunge lakini kamati hizi mbili kwa umakini mkubwa kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu hayo ili tuweze kunufaisha Taifa hili kupitia huduma zinazotolewa katika Taasisi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa suala la utekelezaji wa *Blue Print* ambalo Mheshimiwa Tarimba amemaliza sasa Serikali inaendelea kuhakikisha kutekeleza hilo lakini tunaangalia na mapungufu mengine ambayo yanaendelea kujitokeza wakati tunatekeleza. Siyo kweli kwamba tunafungia katika kabati lakini tunaendelea kutekeleza hatua kwa hatua na nikuhakikishie Bunge lako liwe na imani nia ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ni kuona tunaweka mazingira wezeshi na bora Zaidi ili kuwahakikisha sekta binafsi inakuwa ni kiongozi katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumeongelewa mambo mengi kuhusiana na miradi ya kimkakati ambayo inatekelezwa chini ya Taasisi zetu. Serikali inaendelea kufanya bidi na haraka zaidi lakini kwa uweledi ili miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa haraka lakini kwa tija kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Imeongelewa miradi ya Mchuchuma na Linganga, lakini kuhusu viuwadudu na mengine tutahakikisha tunatekeleza miradi hii kwa uweledi lakini kuona maslahi mabana ya nchi yanazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tunachukua maoni yote na tuhakikishie Waheshimiwa Wabunge lakini kamati zetu mbili ambazo zinatusimamia kwamba tutatekeleza maoni yao na ushauri wao na tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kamati hizi mbili. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Chande.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii lakini awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu ambaye amepitisha mjadala huu katika hali nzuri na usimamizi wako mzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kushukuru sana kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwapongeze pia watoa hoja wenyeviti wote wawili ambao yaani Mwenyekiti wa bajeti na mwenyekiti wa PAC ambao wamewasilisha ripoti zao hapa au taarifa zao ziko vizuri niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kupunguza mzigo kwa wananchi wake wa Tanzania, dhamira hiyo inaendelea katika kuonekana utekelezaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika suala ambalo hoja imezungumzwa ama maoni yametolewa na kamati ya bajeti kuhusu riba. Naomba niongelee hapo kwamba Serikali inachukua hatua mbalimbali katika kupunguza mzigo kwa wananchi wake hasa wale wakopaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuagiza sekta ya bank na taasisi ya fedha kuweka mikakati ya kupunguza gharama za uendeshaji ikiwemo kuhamasisha matumizi ya teknolojia

katika kutoa huduma za fedha kwa lengo la kupunguzia mzigo mteja na kuhakikisha viwango vya riba vinashuka kufikia tarakimu moja tu yaani *single digit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kupitia benki kuu inatoa taaluma kwa wateja mbalimbali au kwa wananchi mbalimbali ili kududi wawe na maamuzi sahihi wakati wa kuingia katika mikopo hiyo. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kutatua changamoto na miongoni mwa hatua hizo mwezi Julai, 2021 hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa unafuu wa kisheria katika kiasi cha amana ambacho bank na taasisi ya fedha zinatakiwa kuweka benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kurekebisha kauli za usajili wakala wa benki kwa kuondoa sharti la kuwa na uzoefu wa miezi 18 katika eneo la biashara, jambo la tatu kupunguza kiwango cha riba kinachotolewa kinachotolewa katika *account* za wateja watoa huduma za fedha kwa njia za simu za mkononi. Lakini benki imechukua hatua ya kuhakikisha benki kuu imeanzisha mfuko maalum wa shilingi trioni moja kwa riba ya asilimia 3 kwa mwaka. Benki Kuu imepunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuweka na benki za biashara kwa ajili ya kuweza kutoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhakikisha kuwa uwiano wa gharama za uwendeshaji na mapato ya benki kuzidi asilimia 55 na mikopo chechefe isiyozidi asilimia 5, kushirikiana na umoja wa mabenki katika kusimamia maadili ya watendaji, kushirikiana mabenki pamoja na taasisi ya fedha, kufanya ukaguzi maalumu kwa wastaafu yote haya ni matarajio yetu kwa muendelezo huo zote hizi zitasaidia kuendelea kupungua kwa riba za mikopo nchini. Hivi karibuni tumeshuhudia benki kubwa za kibiashara zikipunguza riba kutoka asilimia 20 hadi asilimia 9 katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pendekezo la kuanzisha Ofisi ya kupokea malalamiko ya kodi mapendekezo haya pia tumeyachukua kwa sababu pendekezo la muundo wa Taasisi ya kanuni za uwendeshaji zimeandaliwa tayari na

zimekwisha andaliwa na kupelekwa kwa ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa *evening*, tunatarajia hivi karibu kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha itakuwa idhini hiyo tumeshaipa na muundo utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nijielekeze katika hoja ya pili ambayo imetokewa na Kamati ya *PIC* ambayo inazungumzia miradi kutokamilika kwa wakati. Serikali inatekeleza bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge hadi kufikia mwezi Disemba, 2021 kiasi cha shilingi bilioni 585.1 zimetolea kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo sawa na asilimia 86.2 ya lengo nunu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 5194.3 na fedha za ndani ni shilingi bilioni 167.1 fedha za nje. Aidha shilingi bilioni 443.7 ni fedha za washirika wa maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sasa namuita Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, mtoa hoja. (*Makofi*)

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niweze kuwapongeza sana Wabunge wote waliochangia na kwa bahati nzuri wote wameunga mkono hoja. Kwa hiyo, hatuna hoja ya kujibu, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yameongelewa mengi wamechangia Wabunge wapatao kumi kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti, ambao ni Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Dkt.

Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Ali King, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa pamoja na Mheshimiwa Tarimba Abbas. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi yamezungumzwa naomba nisiyarudie yote lakini nitoe msisitizo kwa mambo machache. La kwanza, ni mahitaji ya fedha za dharura kwa ajili ya barabara za vijijini imefanyika tathimini inatakiwa Shilingi bilioni 111.3, ili kurejesha hali ya mawasiliano katika barabara zetu vijijini. Kwa hiyo, tunaomba tena Serikali ijielekeze kuhakikisha kwamba hili linafanyika ili watanzania, waweze kuendelea na huduma mbalimbali za wawasiliano kwa maana ya usafiri na usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kufanya marejeo kwenye viwango vya Mfuko wa Jimbo. Mfuko huu wa Jimbo fedha hizi za miaka 20 iliyopita leo hii mfuko wa *cement* ni shilingi 18,000 mpaka shilingi 25,000 lakini wakati ule ulikuwa shilingi 10,000 mpaka shilingi 15,000. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ifanye marejeo ili kuongeza fedha za Mfuko wa Jimbo liendane na hali halisi ya uchumi wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kubwa ni kununua *cargo scanners* kwenye mipaka yetu. Tuna mipaka kama tisa mikubwa tumeenda Namanga pale hakuna *cargo scanner*, msururu wa mabasi, wa malori ni mkubwa sana na gharama ya usafirishaji inakuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, tuiombe sana Serikali iweze kununua *cargo scanners*, kwa ajili ya kusaidia mizigo kutoka lakini pia itaongeza mapato ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ajira kwa TRA upungufu wa *staff* wa TRA umefanya walipakodi wengi kutokufikiwa hasa kwenye maeneo ya *Tax Audit* pamoja na *Block Management*. *Tax Audit* ni *truly for voluntary tax compliance* kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa TRA kuajiri wafanyakazi wa kutosha ili sasa waweze kufanya *Tax Audit* pamoja na *Block Management* ili *ku-enhance voluntary tax compliance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni bima ya afya kwa wote. Watanzania wanaotumia bima leo ni chini ya asilimia 20 kwa hiyo, kuna haja kubwa sana Serikali ikajielekeza ikaleta Sera na Sheria, ili sasa Watanzania waweze kuingia kwenye bima ya afya kwa wote ili kuwasaidia Watanzania kupata huduma za afya katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa habari ya daraja la *Tanzanite* nadhani Wabunge wamechangia sana kwa nguvu kubwa kabisa. Nadhani ni vyema basi Serikali ikajielekeza ikaangalia umuhimu na uwezekano wa daraja hili kuwa *toll bridge* ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya kuendesha mkopo huu wa Shilingi bilioni 243.8 waliotoa kwenye Serikali ya Korea Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamesemwa lakini hasa hili la *TARURA* ameongea Mheshimiwa Reuben kwa msisitizo mkubwa sana. Kwa kweli tulitenga bajeti hii ya tozo shilingi bilioni 322, lakini tunapotoa leo dharura shilingi bilioni 111 tumeharibu utaratibu wa bajeti. Naomba Serikali ilianganalie hili kwa umakini mkubwa sana ili bajeti yetu iende vizuri, watanzania wapate huduma ambazo wanatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili waliochangia, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ameongelea habari ya *Blue Print*. Tunaomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri hili mlizingatie sana ili kurahisisha ufanyaji biashara hapa nchini, kupunguza mlolongo mkubwa sana wa taasisi zetu za Serikali. Katika ufanyaji wa biashara na ili biashara ziwe rahisi watanzania wafanye shughuli za kiuchumi waweze kulipa kodi na kuwanufaisha watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri wetu wa Fedha ameongea habari ya riba kwa wakopaji. Hili kwa kweli walianganalie kwa mfano mikopo kama ya watu binafsi *risk* ni ndogo sana kwa hiyo, waanganalie kwa ukaribu ili watanzania waweze kukopa kutoka benki yao ya biashara. Waweze

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuwekeza na shughuli za kiuchumi ziendele walipe kodi kwa manufaa makubwa na mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Ofisi ya mpokeaji wa malalamiko ya kodi *Tax Imbursement* ni miaka mitatu sasa tumetunga sheria lakini bado haijaanza ofisi hii, malalamiko ya walipa kodi ni mengi sana mtaani. Naomba sana Serikali ijielekeze kuhakikisha kwamba Ofisi hii inaanza ili kupunguza malalamiko ya walipa kodi wetu ili walipe kodi kwa hiari na nchi yetu iweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nawapongeza sana wote lakini niombe sana wenzetu upande wa Serikali wachukue haya yote maoni ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti; na sisi kama kamati tutaendelea kusimamia na kuishauri Serikali kila hatua ili tuweze kuwa na bajeti bora kwa manufaa mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na baada ya maelezo haya naomba kutoa hoja ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ISSA J. MTEMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Hoja imetolewa, sasa nitawahoji. Kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu shughuli za Kamati ya Mwaka 2021.

Wote mmeafiki. Sasa hii ni Taarifa rasmi siyo ya kamati ni ya Bunge kwenda Serikalini, nakushukuru sana Mwenyekiti kwa kazi nzuri uliyoifanya. Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya uwekezaji wa Mitaa ya Umma *PIC*.

MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru

wote, tumepata wachangiaji 20 ambao wamechangia hoja zote mbili lakini katika hoja ya Kamati ya Bajeti wametaja mashirika ambayo na sisi tunasimamia kwa haraka haraka Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Christine Mnzava, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Hyuma, Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Joseph Kandege, Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, Mheshimiwa ShallyRaymond, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, Mheshimiwa Stansalaus Mabula, Mheshimiwa Luhanga Mpina, DKT. John Pallangyo, Mheshimiwa Ally Hassan King, Mheshimiwa Abbas Tarimba na Naibu Mawaziri wawili; Naibu wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Kigahe na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango - Mheshimiwa Chande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyoko kwenye taarifa ya kamati naomba kama walivyosema wachangiaji wengi niseme mambo machache yafuatayo; niombe tuipongeze sana Serikali na tumpongeze kipekee Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuweka mtaji mkubwa kwenye benki yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa yetu tumeelezea mwezi disemba Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 208 kama mtaji kwa benki hii na juzi tumeona ufaransa benki hii imesaini *euro* milioni 80 sawa na shillilingi bilioni 210 tunaamini fedha hizi zitaenda kuleta tija kubwa kwenye sekta ya kilimo kupitia benki yetu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa mwongozo wako kwenye kikao cha leo lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Acskon, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumshukuru Katibu wetu ndugu Nanelwa Mwiambi, Mkurugenzi wa Idara ndugu Athumani Hussein, Kaimu Mkurugenzi msaidizi ndugu Bisile, makatibu wa kamati yetu wakiongozwa na Zainabu Mkamba, washauri wetu wa mambo ya sheria na wataalamu wengine kwa ushirikiano mzuri wanaotupa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati yetu inafanya kazi na Msajili wa Hazina ndugu Mgonya Benedict, tunamshukuru sana kwa kazi kubwa anayotusaidia na wataalamu wake ambao anafanya nao kazi, tuwataje ndugu Lightness Mauki, Mkurugenzi wekezaji wa umma, na Linus Kwakesigabo, Mhasibu Msaidizi wambao wamekuwa wakitusaidia sana kwenye kazi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wamezungumza mambo yale tuliyoyatoa kwenye maoni na mapendekezo itoshekusema tu maeneo yote mliyotaja ya *APZA, NHIF, MSB, TARURA, NHC, TPA*, kwenye maeneo ya *TICTS* na kule kwenye uyejushaji wa mafuta, RUWASA, yote tutayafanyia kazi kwa mashirika yale tunayoyasimamia na tunaamini Msajili wa Hazina atatengeneza utaratibu mzuri wa kamati yetu kuweza kufanya kazi ya kusimamia uwekezaji wa mitaji ya umma na mashirika haya yaweze kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwenye taarifa yetu kwamba gawiwo la mashirika haya ni moja kati ya chanzo kikubwa cha mapato kwenye mfuko wa Taifa, Kamati yetu itaendelea kufanya kazi kwa moyo na uwadilifu wa hali ya juu katika kuishauri Serikali kuweza kuwezesha mashirika haya yaweze kufanya kazi vyema katika kuleta tija na ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho siyo kwa umuhimu niwashukuru sana wajumbe wa kamati Makamu mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima na wajumbe wote kwa ufinyu wa muda naomba majina yao yaliyokwenye kamati yaingie kwenye Kumbu kumbu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC)

Wote wameafiki nakupongeza Mwenyekiti, kwa kazi nzuri hii nayo ni taarifa rasmi ya Bunge kwenda Serikalini kwenda kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, wote kwamba kutakuwa na semina inayohusu majukumu na utendaji kazi kwa wakala wa barabara na vijijini na mjini *TARURA* kesho tarehe 17 Februari, 2022 siku ya Alhamis katika ukumbi wa Pius Msekwa saa tano asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria.

(Saa 12.45 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 17 Februari, 2022 Saa 08.00 Mchana)